**2 SEPTEMBA, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Tano – Tarehe 2 Septemba, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption (Amendments) Bill, 2024)*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)*.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu:-

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption (Amendments) Bill, 2024)*.

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)*.

**MHE. BONIFACE N. BUTONDO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Maoni na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Neema Lugangira.

Na. 69

**Kanuni za Maadili katika Uchaguzi**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza: -

Je, lini Kanuni za Maadili ya Uchaguzi zitakuwa tayari baada ya makosa ya ukatili wa kijinsia kuongezwa kwenye Sheria za Uchaguzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 162 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2024 kinaeleza kuwa, Tume baada ya kushauriana na vyama vyote vya Siasa itaandaa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi. Aidha, kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 1.2 ya Kanuni za Maadili ya Uchaguzi za mwaka 2020, Maadili ya Uchaguzi yatatumika katika Uchaguzi Mkuu na katika chaguzi ndogo. Kwa msingi huo, maadili mapya ya uchaguzi huandaliwa kila mwaka wa Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunaelekea katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, wakati ukifika Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushauriana na vyama vyote vya siasa itaandaa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maelezo mazuri ya Serikali na natambua kwamba Kanuni za Maadili ya Uchaguzi huwa zinaandaliwa mwaka wa uchaguzi, lakini kwa kuzingatia unyeti na upekee wa makosa ya ukatili wa kijinsia katika uchaguzi yaliyoongezwa ningependa kujua, je, Serikali haioni umuhimu wa kuandaa kanuni hizi mapema zaidi ili wananchi wapate muda wa kutosha wa kuelimishwa kuhusu kanuni hizi na wale ambao watakuwa wanagombea wajue ni hatua gani za kuchukua pale ambapo wanapitia matukio ya ukatili wa kijinsia katika uchaguzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Neema kwa namna ambavyo amelisema suala hili la ukatili wa kijinsia. Pia nimwambie kwamba ushauri wake tumeupokea, tutaendelea kuufanyia kazi. Pia niwatoe wasiwasi Watanzania kwamba tupo vizuri na tutaendelea kuhakikisha kwamba kanuni hizi zinafahamika kwa wananchi wote. Vile vile tutaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali, mashirika yasiyo ya kiserikali, Asasi za Kidini, vyombo vya habari na maeneo tofauti tofauti ili kuweza kutoa elimu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais. Mheshimiwa Genzabuke.

Na. 70

**Upungufu wa Watumishi kwenye Zahanati – Kigoma**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la upungufu wa watumishi kwenye zahanati – Kigoma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuajiri wataalamu wa Kada mbalimbali za afya ambapo katika kipindi cha miaka mitatu (2021 - 2023), Serikali imeajiri jumla ya watumishi 18,418 wa kada mbalimbali za afya na kuwapangia vituo kote nchini ukiwemo Mkoa wa Kigoma uliopangiwa wataalamu wa kada za afya 658.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kupitia Sekretariati ya Ajira, imetangaza ajira ambapo jumla ya vibali 9,483 vya ajira za wataalamu wa afya vimetolewa na taratibu za ajira zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pindi taratibu za ajira hizi zitakapokamilika, wataalamu wa afya walioajiriwa watapangwa kwenye vituo vyenye upungufu mkubwa kote nchini, ikiwemo Mkoa wa Kigoma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Zahanati ya Kijiji cha Mvinza katika Kata ya Kagera Nkanda, Halmashauri ya *Kasulu DC* ina watumishi wawili tu na watumishi hao wakati mwingine huwa hawafiki wote kwa pamoja katika kituo hicho cha kazi. Je, Serikali ina mpango gani, kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya *Kasulu DC* kupeleka mtumishi katika kijiji hicho cha Mvinza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Zahanati ya Mvinza kuna upungufu wa watumishi, lakini Serikali imeendelea kupeleka wataalamu wa afya katika Mkoa wa Kigoma. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna orodha ya vituo vyote vyenye watumishi wachache zaidi ikiwemo zahanati hii ya Mvinza na baada ya ajira hizi kukamilika tutahakikisha tunapeleka mtaalamu kule kwa ajili ya kuongeza nguvu kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kasulu ikiwa wanaweza kupata mtumishi mwingine kwa kipindi hiki cha muda mfupi na kumpeleka pale itakuwa ni jambo jema ili kuongeza nguvu kazi ya watumishi katika zahanati hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Zahanati ya Welu ambayo ipo Jimbo la Kalenga inahudumia zaidi ya vijiji vinne na kuna changamoto ya wauguzi na madaktari. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha tunapata wauguzi na daktari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni kuendelea kuajiri watumishi wa Sekta ya Afya na kuwapangia kwenye vituo vyote vyenye upungufu wa watumishi ikiwemo zahanati hii ya Welu. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pindi hizi ajira zitakapokamilika tutahakikisha pia tunaongeza watumishi kwenye zahanati ya Welu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Upungufu wa watumishi wa afya Wilaya ya Chemba ni zaidi ya 62%. Nini kauli ya Serikali juu ya hawa watumishi wapya watakaoajiriwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa watumishi katika Halmashauri ya Chemba na maeneo mengine umesababishwa pia na kasi nzuri ya ujenzi wa vituo vya huduma za afya, lakini Serikali katika miaka hii mitatu imeshaajiri watumishi zaidi ya 14,000 na kuwapangia katika Halmashauri ya Chemba na maeneo mengine kote nchini. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Monni kwamba katika ajira hizi ambazo zinaendelea na utaratibu kwa sasa, tutahakikisha pia zahanati hiyo inapata watumishi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Abdallah Chaurembo kwa niaba ya Mheshimiwa Kilave.

Na. 71

**Ujenzi wa Barabara za Kata ya Chamazi – Mbagala**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE K.n.y. MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza: -

Je, lini Barabara za Tinyango, Machimbo, Kisiwani, Mapemba, *Federation*, Kwa Mzala na Kwa Masista, Kata ya Chamazi zitajengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza ujenzi wa barabara hizi, ambapo kwa mwaka 2022/2023 barabara ya Machimbo yenye urefu wa kilometa 1.35 ilijengwa kwa zege urefu mita 240 kwa gharama ya shilingi milioni 73.8 na kuwekewa changarawe mita 800 ambapo shilingi milioni 36 zilitumika na mwaka 2024/2025 imepangwa kujengwa kwa zege mita 100 kwa gharama ya shilingi milioni 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 barabara zifuatazo ziko kwenye mpango ambapo barabara ya Tinyango (kilometa 1.14) imepangwa kujengwa kwa zege urefu wa mita 500 kwa gharama ya shilingi milioni 350 na barabara ya Transfoma Kwa Mzala (kilometa mbili) itajengwa kwa zege mita 100 sambamba na kufanyiwa matengenezo ya sehemu korofi ambapo shilingi milioni 94 zimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara za Molemole Kwa Masista (kilometa 1.28), *Federation* (kilomita 0.58), Mapemba (kilometa 0.8) na Kisiwani (kilometa 1.0) kwa mwaka 2024/2025 zimepangwa kufanyiwa matengenezo ya sehemu korofi kwa kuweka changarawe na kuchongwa ambapo shilingi milioni 300 zitatekeleza kazi hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, wakati tunasubiri mpango wa Serikali wa hizi barabara nyingine kujengwa, je, hamuoni ipo sababu ya kurudisha mawasiliano katika barabara ya Tinyango kwa sababu kuna uharibifu mkubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Mama Kibonge katika Kata ya Buza Jimboni Temeke?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri sana yenye lengo la kutetea wananchi, lakini kuhusiana na swali lake la kwanza naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ya Tinyango itajengwa kwa kutumia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke pamoja na Meneja wa *TARURA* wa Temeke kuhakikisha kwamba wanatangaza kazi zote zile zilizobakia ambazo ni za matengenezo na zinatokana na fedha ya mapato ya ndani katika halmashauri wazitangaze haraka iwezekanavyo ili wakandarasi wapatikane waanze kuzijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, barabara hii ya Tinyango ni miongoni mwa barabara moja ambayo ipo katika utaratibu huo na kwa wakati huu naomba niendelee kusisitiza kwamba wananchi waweze kutumia njia mbadala ambazo zimewekwa. Kuna njia mbili; kuna njia ile ya Mbande - Kisiwani, lakini kuna ile ya Uvikiuta – Tinyango. Kwa hiyo, mpaka ile barabara ya Tinyango itakaporudishiwa mawasiliano wananchi waweze kutumia barabara hii. Namwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke aharakishe utaratibu wa kuanza ujenzi wa barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka wa bajeti kuhakikisha inafanya matengenezo na kuboresha barabara zetu hizi za wilaya. Nimhakikishie kwamba barabara yake hii ambayo ipo Buza na yenyewe ipo katika utaratibu wa kufanyiwa

matengenezo katika mwaka huu wa fedha. Namwahidi itatengenezwa, itarekebishwa na wananchi wake wataweza kuitumia kwa manufaa mapana ya kiuchumi na ya kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Issaay

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kazi ya ujenzi wa barabara katikati ya Mji wa Mbulu na daraja limesimama kwa muda wa miezi miwili sasa na hali hiyo imeathiri sana shughuli za wafanyabiashara katika Mji wa Mbulu. Je, ni lini mkandarasi yule atalipwa fedha ili akamilishe kazi aliyokuwa amepangiwa?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa ujenzi wa barabara zetu hizi za *TARURA* ikiwemo ukamilishaji wa barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge na hasa katika daraja hili aliliolitaja. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tutaendelea kuweka msukumo ili kuhakikisha ujenzi wa daraja na barabara unakamilika ili uweze kuleta manufaa kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua.

Na. 72

**Ujenzi wa Mabwalo ya Chakula Shule za Sekondari Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Mabwalo ya Chakula katika Shule za Sekondari za Mvungwe, Seuta, Mkindi Kikunde na Kimbe katika Jimbo la Kilindi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2022/2023 na 2023/2024 Serikali ilipeleka shilingi bilioni 2.2 katika shule za Sekondari za Mvungwe, Seuta, Mkindi Kikunde na Kimbe zilizo katika Jimbo la Kilindi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo mabwalo ya chakula katika shule za Sekondari za Mvungwe, Seuta, Mkindi Kikunde na Kimbe Jimbo la Kilindi kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Serikali na kuishukuru sana kwa kutupa kiasi hicho cha fedha ambacho kwa kweli kwa kiasi kikubwa kimeweza kusaidia miundombinu katika Jimbo langu la Wilaya ya Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja tu. Hizi shule zote ambazo nimezitaja hapa ni shule za Kidato cha Tano na cha Sita lakini zina uhitaji mkubwa sana sana hususan shule ya Sekondari ya Mkindi na Shule ya Sekondari Vungwe. Hizi shule tuna wanafunzi na kila shule ina wanafunzi 600 na hawana bwalo la kulia chakula. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kuiona hii kama ni dharura ili kuweza kurahisisha kupata huduma kwa wanafunzi hawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli amekuwa akifuatilia

sana maslahi mazuri na mapana ya wanafunzi katika jimbo lake kwa kuhakikisha anaendeleza miundombinu hii katika shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tayari Serikali imeshaanza na kila mwaka inatenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu hii. Naomba nimtoe hofu kwamba Serikali inalichukua hili na tutalifanyia kazi kwa ukaribu. Tutazungumza mimi na wewe tuone ni namna gani tunaweza kuhakikisha miundombinu hii muhimu inapatikana kwa ajili ya wanafunzi wetu hawa katika shule hizi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Sekondari ya Kata ya Bulamatamu haina mabweni na kuna mazingira magumu sana. Ni lini Serikali itapeleka mabweni kwenye shule ya sekondari hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kuwasemea wananchi wake ili kuhakikisha wanapata miundombinu bora kabisa katika shule hizi na hasa hii ya sekondari aliyoitaja ambayo iko Kata ya Bulamata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kila mwaka inatenga fedha kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri na kupitia Serikali Kuu kwa ajili ya kuendeleza muindombinu katika shule zetu hizi. Pia, Serikali imekuwa ikiendeleza hii miundombinu kwa awamu. Kwa awamu ya kwanza, tayari majengo yamejengwa ambayo yamewezesha udahili wa wanafunzi na wameanza kuyatumia majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa awamu inayofuata tutaendelea kwa kadiri fedha zinavyokuwa zinapatikana na zinavyotengwa kwenye bajeti, tutazileta kwa ajili ya kuhakikisha tunakamilisha miundombinu mingine iliyobakia, hususan hii uliyoitaja katika Shule hii ya Bulamata. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari Maili Sita watoto wanatembea umbali mrefu sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga bweni na bwalo? Tayari tumeshaandaa eneo la kutosha na wananchi wako tayari kushirikiana na Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kuwasemea wananchi wake ili kuhakikisha wanapata miundombinu iliyo bora kabisa katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali tayari ilianza; imejenga shule mpaka kwa ngazi iliyofikia. Namhakikishia kwa kadiri tutakavyokuwa tunapata fedha, awamu inayofuata tutaangalia ni namna gani nzuri ya kuleta fedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu hii ya bweni na bwalo kwa kushirikiana na Halmashauri, kwa maana ya mapato ya ndani na kwa kutumia fedha kutoka katika Mfuko wa Serikali Kuu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Serikali ya Isongole haina mabweni kabisa kwa *form five* na *form six*

ukizingatia shule hiyo inafanya vizuri sana. Je, ni lini Serikali itajenga mabweni kwenye shule hiyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiweka kipaumbele kikubwa sana kujenga mabweni kwa ajili ya kuruhusu udahili na kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano na cha Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imekuwa ikifanya hivyo kwa awamu. Kwa hiyo, Serikali itaendelea na utaratibu huo Shule hii ya Isongole iweze kupata mabweni, ili iweze kupandishwa hadhi kuwa Kidato cha Tano na cha Sita, wanafunzi wetu wapate sehemu nzuri ya kusomea na walimu wapete sehemu nzuri ya kufundishia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Mwanahamisi Kassim Said, kwa niaba.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwanahamisi Kassim, naomba sasa swali lake…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko. *(Kicheko)*

Na. 73

**Usiri wa Ugawaji wa Taulo za Kike**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuweka usiri katika ugawaji wa taulo za kike shuleni na vyuoni ili kudumisha silka na utamaduni wa Mtanzania? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inatambua vyema mila, desturi na utamaduni wa nchi yetu kuhusu suala la hedhi salama. Utafiti uliofanywa na *NIMR* Mwaka 2021 ulibaini kwa kiasi kikubwa wanafunzi wamekuwa wakishindwa kuhudhuria masomo kutokana na ukosefu wa bidhaa za hedhi kwa siku tano hadi siku saba kwa mwezi, sawa na siku 50 au 70 kwa muda wa masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaweka jitihada kuhakikisha jamii inatambua umuhimu wa hedhi salama na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya hedhi kwa wasichana. Lengo ni kuwezesha uwepo wa vifaa sahihi vya kujisitiri, upatikanaji wa maji safi, sabuni pamoja na sehemu sahihi ya kuhifadhia au kutupa vifaa ambavyo tayari vimetumika. Serikali itaendelea kuzingatia suala la usiri kwa kuhakikisha kuwa, kunakuwa na chumba maalum shuleni kwa wanafunzi wa kike kujisitiri wakati wa hedhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni kweli kabisa, kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema, kumekuwa na *drop out* au ku-*miss* kuhudhuria masomo kwa wanafunzi kati ya siku tatu mpaka tano na wakati mwingine inaenda mpaka siku saba. Je, ni kwa nini sasa Serikali isiweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba, inagawa hizi *sanitary pads* kwa shule zote kwa usawa ili watoto ambao wamefikia umri wa kuingia kwenye siku zao waweze kuhudhuria masomo bila kukatisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Serikali imeelekeza kwamba, wana mkakati wa kujenga chumba maalum, lakini pia, kumekuwa hakuna usiri, kwani watoto wanachanganyika, wengine ni wa umri mkubwa na wengine umri ndogo. Kwa hiyo, wanavyoenda kufanya *changes* kule inakuwa ni kama vile inaleta *embarrassment*. Ni kwa nini Serikali isiweke mkakati madhubuti sasa hivi wa kuhakikisha kwamba, wanarekebisha vyoo vyote vinakuwa na chumba maalum, kwa ajili ya watoto wetu kwenda kubadilishia *pads* wakiwa katika siku zao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, yote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ana hoja ya msingi. Kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, Serikali inatambua uhitaji wa vifaa vya kujisitiri watoto hawa na ndiyo maana imevunja ukimya na imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba jamii inatambua umuhimu wa hedhi salama na kusaidia kupatikana kwa vifaa vya hedhi kwa wasichana.

Kwa hiyo, Serikali tayari imekuwa inatoa vifaa hivi kwa ajili ya watoto kuvitumia pindi wanapokuwa kwenye hedhi, lakini imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali katika jitihada hizi ili kuhakikisha kunakuwa na mazingira mazuri kwa watoto wetu kujihifadhi kipindi wanapokuwa kwenye hedhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la chumba maalum. Kama nilivyojibu hapo mwanzo kwamba, Serikali imetoa Mwongozo na mpaka wakati huu katika ujenzi wa miundombinu ya shule, ramani zinazingatia kuwepo kwa chumba maalum kwa ajili ya watoto kujisitiri pindi wanapokuwa kwenye hedhi. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inaendelea na

jitihada hizo ili kuhakikisha watoto wetu hawakosi kwenda shule kwa sababu wako kwenye hedhi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali iliondoa tozo katika taulo za kike na baadaye ikairudisha. Ni lini tutakaa tena na kuweza kuondoa tozo hizo ili kusaidia watoto wa kike kuzipata kwa bei ya chini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, suala hilo ni la kikodi. Ni hoja ambayo wenzetu wa Wizara ya Fedha nadhani watakuwa wameisikia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, wewe lichukue. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mimi nalichukua kwa niaba yao. Nitalifikisha.

**NAIBU SPIKA:** Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly.

Na. 74

**Waathirika wa Mwongozo wa Miaka Minne wa Upandishaji Madaraja**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE** aliuliza:-

Je, Serikali inawasaidiaje waliioguswa na Mwongozo wa Waraka wa miaka minne baada ya Serikali kurejea Mwongozo wa Upandaji Madaraja kwa miaka mitatu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi wa Kada Mbalimbali *(Scheme of Services)* na miongozo mingine, muda wa watumishi kutumikia cheo kimoja kabla ya kupandishwa cheo kwa watumishi walioajiriwa kwa mara ya kwanza katika Utumishi wa Umma ni angalau kipindi cha miaka mitatu. Hata hivyo, katika kipindi cha zoezi la uhakiki wa vyeti feki na watumishi hewa, baadhi ya watumishi walichelewa kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imechukua jitihada mbalimbali za kuoanisha na kuwianisha upandaji vyeo wa watumishi ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imewapandisha vyeo watumishi 180,000 wakiwemo watumishi walioathirika na zoezi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika utekelezaji wa Ikama na Bajeti ya Mwaka 2023/2024, Serikali imewapandisha vyeo watumishi zaidi ya 216,000 wakiwemo walioathirika na zoezi la uhakiki wa vyeti feki na watumishi hewa. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nawapongeza kwa juhudi ambazo Serikali inafanya kwa watumishi, lakini kama mmepandisha bila kukumbuka muda wa miaka minne wa hawa watumishi ambao walipoteza

hamjui kwamba mtiririko wao wa kiutumishi kwenye sifa za kupanda vyeo utakuwa umepotea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali namba mbili. Je, hamuoni kwamba sasa badala ya kutoa tatizo tutaenda kuleta tatizo la watumishi wengi kulundikana kwenye cheo kimoja kwa sababu, waliokuja kwenye miaka mitatu na miaka minne wote wamekutana hapo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Janejelly kwa namna ambavyo amekuwa mstari wa mbele kuwapigania watumishi wa umma. Pia, nitamjibu maswali yake yote mawili kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na pia, kuwatambua wale waliosahaulika katika zoezi hili la uhakiki wa vyeti feki. Naomba nimtoe shaka kwamba katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga takribani shilingi bilioni 252.7 kwa ajili ya kupandisha vyeo watumishi 219,924. Kwa hiyo, katika zoezi hili, Serikali imezingatia hayo mambo mawili aliyoyasema ikiwemo kuwasawaza ili waweze kufanana na wenzao. Kwa hiyo, namwondoa shaka kwamba bajeti hii iliyopitishwa itazingatia jambo hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa upandishaji wa madaraja unasababisha watumishi kudai nyongeza ya mishahara na *arrears* zao, ni nini kauli ya Serikali juu ya kuwalipa *arrears* zao kwa wakati? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba, upandishaji wa vyeo pia unasababisha malimbikizo ya *arrears* kama hakulipwa malimbikizo yake. Naomba nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali katika bajeti hii ya mwaka 2024/2025 imepitisha kiasi cha shilingi trilioni 8.3. Katika bajeti hiyo fedha kwa ajili ya malimbikizo pia imo ndani. Kwa hiyo, wale wote ambao waliathirika katika upandishwaji vyeo watalipwa malimbikizo yao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Madini. Mheshimiwa Ally Mlaghila aulize swali lake.

Na. 75

**Malipo kwa Wafanyakazi wa *Kiwira Coal Mine***

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza:-

Je, mchakato wa kuwalipa waliokuwa Wafanyakazi wa *Kiwira Coal Mine* umefikia hatua gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la Wafanyakazi wa Kiwira lilitokana na malalamiko ya mapunjo ya mafao kutoka kwa waliokuwa wafanyakazi wa mgodi huo kabla ya ubinafsishaji. Baada ya Chama cha Wafanyakazi Mgodini *(TAMICO)* kuwasilisha malalamiko ya mapunjo hayo Serikalini, Serikali ilifanya Ukaguzi Maalum kupitia kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*

Novemba, 2008 na baadaye Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali *(Internal Audit General)* alihakiki madeni hayo, Agosti, 2021.

Uhakiki wa madeni hayo ulibaini madai ya wafanyakazi yalikuwa ni shilingi 1,240,000,000 kwa wafanyakazi 893; na madeni ya wazabuni, wakiwemo watoa huduma ya ulinzi, yalikuwa ni shilingi milioni 496; na kufanya deni lote kuwa jumla ya shilingi 1,520,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uhakiki huo kukamilika, Serikali ililitambua deni hilo na kulipeleka Hazina kwa ajili ya hatua za kuweza kulipwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka 15 sasa tangu mchakato huu umeanza na katika mchakato huu kuna wananchi wengine mpaka sasa hivi wameshapoteza maisha. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuharakisha hili zoezi ili hawa wananchi walipwe fedha yao? Wananchi hawa wanatia huruma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Naishukuru sana Serikali kwa kuanzisha kiwanda bora kabisa pale *STAMICO* ambacho kwa sasa kitatoa makaa ya kupikia kwa kutumia makaa ya mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha makaa ya mawe na makaa haya ya kupikia ambayo ni bora zaidi yanawafikia wananchi wa Rungwe, Kyela na Ileje? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Ally kwa maswali yake mazuri. Ninakiri kwamba, kweli deni hili la wafanyakazi hawa limechukua muda mrefu. Pia sisi kama Wizara, hata kupitia ziara ya Kamati ambayo

ilitutembelea miezi michache iliyopita, tulipewa jukumu la kulifuatilia Hazina. Namwahidi kwamba, baada ya kujibu maswali hapa niko tayari kuungana naye tuendelee kufuatilia deni hili ili liweze kulipwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, kuhusu makaa ya mawe ambayo yanachakatwa Kiwira kwa mtambo ambao uliwekwa na Serikali, namjulisha kwamba, kwanza mtambo huo umekamilika na tunavyoongea mzabuni yuko *site* kwa ajili ya *commissioning* na uzalishaji wa majaribio umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango uliowekwa na Serikali ili kusambaza makaa haya kupitia Shirika letu la *STAMICO* ni kwamba, wazabuni, wasambazaji *(distributers),* walikuwa wanatafutwa nchi nzima na mpaka sasa hivi wamepatikana wasambazaji 52. Pia nitumie fursa hii kuwaasa wananchi wa Kyela waunde vikundi, wapeleke maombi ya kuwa mawakala wa kusambaza makaa hayo ambayo yanaitwa *Rafiki Briquettes* ili waweze kutumia makaa hayo ambayo ni safi na salama na itanusuru misitu yetu na mazingira kuharibiwa na wakata mkaa. Maana yake ni kwamba haya makaa sasa ni mbadala wa kuharibu mazingira. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Neema Mwandabila aulize swali lake. Mheshimiwa Shally Raymond kwa niaba yake.

Na. 76

**Kufanya Utafiti Katika Msimu wa Kilimo Kubaini Changamoto**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kufanya utafiti kwa mazao ya kilimo na biashara ili kubaini uwepo wa changamoto katika msimu husika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania *(TARI)* inaendelea kufanya *survey* za changamoto zinazokabili uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, hasa afya ya udongo, magonjwa na wadudu ili kubaini viashiria vya hatari kwa msimu husika na kutoa ushauri kwa wadau wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imeendelea kuitengea *TARI* bajeti ya kiasi cha shilingi bilioni 31, kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu mbalimbali, ununuzi wa vifaa vya kisasa na mafunzo kwa wataalam wa maabara na watafiti ili kuendelea kugundua teknolojia mbalimbali zinazokabiliana na mabadiliko ya tabia-nchi, hususan afya ya udongo, mbegu zinazohimili ukame, wadudu na magonjwa. Aidha, Serikali itaendelea kusambaza kwa wakulima teknolojia zinazogunduliwa na watafiti ili waweze kutambua zinazofaa katika msimu husika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Wizara yaliyoletwa na Mheshimiwa Waziri. Katika muktadha huo, basi kuna mazao ambayo sasa hivi imekuwa ni vigumu kuyauza, ikiwemo vanila inayolimwa Uru Kusini, pamoja na kahawa ambayo imekosa soko kutokana na *deforestation*. Mheshimiwa Naibu Waziri, unawaeleza nini wananchi wa Uru Kusini kuhusu jambo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Bei ya kahawa imekuwa ikiyumba kila siku iitwayo siku. Nini hasa hatua ya Serikali kusaidia bei hiyo i-*stabilize? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa, Mama Shally, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto ya Sheria iliyopitishwa na *EU* ya *Deforestation*, hatua inayoichukua Serikali sasa hivi ni kwamba, Bodi ya Kahawa imeanza kufanya *survey* na kuanza utaratibu wa *certification* na kuwapatia wakulima na mashamba yao hati za ithibati ambazo zitasaidia uuzaji wa mazao ya kahawa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linafanywa kwa mazao ya kahawa, zao la *cocoa*, *soya beans* na mazao mengine. Kuna mazao sita ambayo kwa mujibu wa Sheria iliyopitishwa na Bunge la *EU,* ni lazima kama Taifa na dunia nzima, tuweze ku-*meet* hiyo *standard* na Serikali inachukua hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezuia kampuni binafsi kujichukulia shughuli hii. Jambo hili litafanywa na Serikali na tunaendelea kulifanya kwa sababu, bila ya hivyo wakulima wadogo hawataweza kulipia gharama za *certification.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto ya zao la vanila, naomba tu nikuhakikishie kuwa sasa hivi, kama Serikali tunafanya mazungumzo ya mwisho na nchi kama India na *delegation* itakayoondoka na Mheshimiwa Rais ambayo Naibu Waziri atakuwemo, moja ya mkataba utakaosainiwa China ni pilipili pamoja na zao la vanila. Kwa hiyo, itatuondolea matatizo yanayotukabili katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *stabilization* ya bei ya kahawa, kwanza nataka tu nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wakulima wa kahawa wote kwamba, hali ya kahawa na ongezeko la bei ya zao la kahawa ya Arabika hata Robusta katika msimu unaokuja inaonesha taswira itakuwa nzuri. Sasa hivi kama nchi tumeji-*register* katika *platform* kubwa ambazo tunapata *price discovery* wenyewe na kuweza ku-*determine* bei itakayotokea kwa wakulima. Kwa hiyo, pale panapotokea changamoto, tutaweza kukabiliana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lako Tukufu mlitupitishia Sheria *(Agricultural Development Fund)* mwaka 2023 na sasa tumeanza kuitengenezea vyanzo vya mapato. Mojawapo ya jukumu la Mfuko huu wa Maendeleo ya Kilimo itakuwa ni kutengeneza mfumo wa kutengeneza *stabilization system* ya kuweza kuwalinda wakulima huko mbele ambapo tutakuwa tunakabiliana na anguko la bei ya mazao ya wakulima. Tunaendelea kuujenga ushirika na tunaendelea kuujenga mfumo wa *TMX* ili tuweze kuwalinda wakulima na changamoto zinazowakabili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kuiuliza Serikali, ni nini mkakati wao kuhakikisha kwamba mazao yetu kwa zile mbegu za asili yanaendelea kuimarishwa katika vyuo vya utafiti ili kuepuka adha wanayoipata sasa hivi kwa kutumia mbegu za kisasa ambazo mkulima anakuwa tegemezi, kila mwaka lazima anunue mbegu mpya badala ile ya zamani ambayo ilikuwa unaweza ukapanda hata misimu sita hadi saba? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mabula, Mbunge wa Ilemela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama Serikali sasa hivi tumeshakusanya aina 330 za mbegu zetu za asili na tumeanza kuzifanyia mchakato wa kuzisafisha na kufanyia *characterization*. Vilevile tumefanya mabadiliko ya Kanuni ya Sheria ya Mbegu ili kuruhusu mbegu zetu za asili ziweze kuingia madukani kama *certified seeds* kama nyingine zilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwamba baada ya mwaka mmoja kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mbegu zetu za asili zitakuwa madukani kama zinavyoonekana *hybrid seed* au *OPV seed. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu wetu wa *TARI* tayari wameshakusanya mbegu zaidi ya 300 zinafanyiwa *characterization*, zinasafishwa na tutaanza kuzifanyia *multiplication* na kuzigonga muhuri wa *TOSCI* na kuziingiza madukani ili Mtanzania aweze kuzipata kama anavyohitaji mbegu nyingine zozote.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ili wakulima wa kahawa wanufaike na hasa Mkoa wa Kagera ni kuacha kuuza kahawa ghafi, waanze kuongeza thamani kwenye hizo kahawa. Nataka kujua mkakati wa Serikali kuzisaidia *AMCOS* kuweza ku-*access machine* ili waweze kukoboa wauze kahawa safi badala ya kuuza kahawa za maganda kama ilivyo sasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Anatropia kwamba mwelekeo wa

kuuza mazao ya kilimo katika *raw form* siyo mwelekeo *sustainable* kwa muda mrefu. Sasa hivi kama Wizara tumeanza kwanza kufanyia *feasibilty study* Kiwanda cha *TANICA* ambacho kitatugharimu fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *study* ipo hatua ya mwisho tukishirikiana na *TADB* na tutaanza kutenga fedha kwa ajili ya ku-*revive* kile kiwanda kiweze kufanya kazi kwa sababu ni mali ya ushirika na Serikali ndiyo ina *ownership* sasa hivi, kina hali mbaya. Lakini mchakato wa kufanya *value addition* ndiyo mwelekeo wa Serikali, ni hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba ni jambo ambalo lipo kwenye *priority* ya Serikali, linahitaji uwekezaji. Tutalipa kipaumbele kama inavyostahili ili wakulima waongeze thamani ya mazao yao na waweze kuondoka kwenye kuuza malighafi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Hivi karibuni kumekuwa na sintofahamu kwenye suala zima la zao la mbaazi. Mheshimiwa Waziri, zao la mbaazi sasa hivi linauzwa shilingi 1,300 mpaka shilingi 1,400; lakini pili, hao wanunuzi wanaonunua hiyo mbaazi nao wamegoma kununua mbaazi kwa sababu wanasema hawana mahali pa kupeleka. Kwa hiyo, wakulima wetu wamebakia *stranded,* hawajui mbaazi wapeleke wapi, lakini na bei pia hawaelewi ni bei ya namna gani inanunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala zima la wanunuzi hao? Pili, bei elekezi ni ipi sasa? Serikali inamsaidiaje mkulima kujua bei elekezi ya zao la mbaazi hususan Wilaya ya Chemba na Kondoa?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kauli ya kwamba hakuna pa kupeleka mbaazi siyo sahihi, ni kauli ambayo inasemwa na madalali ili kuweza kuiangusha bei ya mbaazi. Pili, ni kauli ambayo inasemwa kwa sababu watu hawataki kwenda kwenye Mfumo wa Stakabadhi ya Ghala na kupitia Vyama vya Msingi vya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tumeweka mguu chini, mbaazi, ufuta na mazao tuliyoyatangaza kupitia *COPRA* ni lazima yauzwe kupitia stakabadhi ya ghala na lazima yauzwe kupitia Vyama vya Msingi vya Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nikwambie leo hii sisi kama nchi tayari tumeji-*register* kupitia *TMX* kwenye *Commodity Exchange Market* za dunia. Bei ya mbaazi leo India ni dola 810, hatutarajii kwenye mnada bei ya mbaazi idondoke kati ya shilingi 1,700/=, au shilingi 1,800/= kupitia mnadani. Kwa hiyo, huo ndiyo mwelekeo wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaombe wakulima wa Kondoa, Chemba na maeneo hayo kuwa changamoto hii katika nchi yetu ipo maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni Chemba kwa maana ya Wilaya ya Kondoa yote. Suala la stakabadhi imekuwa ni changamoto...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi *please*.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kusukuma ajenda ya Stakabadhi Ghalani kwa sababu kupitia *TMX* ndiyo inayotusaidia kupata *price discovery*. Kuna matatizo kwamba wanunuzi wa kati hawataki, lakini ni lazima twende huko. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Magessa.

Na. 77

**Kuruhusu Wananchi Kufanya Shughuli za Kiuchumi Hifadhi ya Misitu kati ya Geita na Katoro**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza:-

Je, lini *TFS* itawaruhusu Wananchi wa Busanda kufanya shughuli za kiuchumi katika hifadhi ya misitu iliyopo kati ya Geita na Katoro kwani haina miti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Msitu Geita ilihifadhiwa rasmi mwaka 1953 na inasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Hifadhi hiyo yenye ukubwa wa hekta 50,836.535 ilifanyiwa mapitio ya mipaka yake kupitia Tangazo la Serikali Na. 717 la Mwaka 2018 kwa lengo la kupunguza maeneo yaliyokuwa yamevamiwa na wananchi au kutoa maeneo yaliyoombwa kwa shughuli za maendeleo kwa vijiji na mitaa inayopakana na hifadhi hiyo. Mabadiliko hayo ya mipaka yalisababisha kupungua kwa eneo la hekta 4,522.95 kwa malengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia uharibifu uliofanyika katika hifadhi ya msitu huo, Serikali imeweka mpango wa kurejesha uoto wa asili uliopotea na kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Serikali imetenga fedha za kupanda miti kwenye hekta 100. Hivyo kwa kipindi hiki ambacho Serikali inafanya jitihada za kurejesha uoto wa asili uliopotea, jitihada zozote za kuruhusu kufanyika shughuli za kibinadamu/kiuchumi zitafifisha jitihada za Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wananchi takribani 400,000 kutoka kata sita za Jimbo la Busanda wanaofanya shughuli za kiuchumi kwenye maeneo haya kwa sababu hayana miti, lakini Serikali imesema wazi kwamba inakwenda kuanza kupanda hekta 100 kati ya hekta 50,000. Kwa hiyo, hekta karibu 50,000 zinabaki hazijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili. Kwa nini Serikali isiruhusu eneo fulani litumiwe na wananchi kwa shughuli za kiuchumi ikiwemo kilimo kwa sababu hekta 50,000 zitakuwa zimebaki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa nini wananchi wasigaiwe miche na *TFS* ili waanze kupanda miche hiyo wakati wakiendelea na shughuli za kiuchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge yote kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la msitu lililoharibika ni hekta 2,000 na siyo hekta 50,000 kama Mheshimiwa alivyokuwa anasema, lakini kwa sababu jambo analolishauri lipo katika taratibu zetu, pale ambapo tuna mpango wa kupanda miti huwa tunatoa ridhaa kwa wananchi kushiriki kwenye kupanda miti kwenye maeneo hayo, lakini vilevile kufanya shughuli za kilimo kwenye maeneo yale ambayo yamepandwa miti. Pale inapotokea kwamba miti hiyo imeshakua mikubwa, wananchi wanaacha kufanya shughuli hiyo ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili tunalichukua, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili tuweze kuweka mkakati utakaokuwa jumuishi kwa wananchi wote wanaohitaji kufanya shughuli hii na kuona mahitaji ya miche ya miti inayohitajika ili tuweze kujipanga na kuweza kutoa ridhaa na kuwasaidia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kembaki.

Na. 78

**Uingizaji wa Bidhaa Bandia Nchini**

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuzuia uingizaji wa bidhaa bandia kutoka nje ya nchi ambazo ni hatari kwa watumiaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Serikali kupitia Tume ya Ushindani *(FCC)* inachukua hatua mbalimbali ikiwa ni mkakati wa kukabiliana na uingizaji wa bidhaa bandia kama ifuatavyo:-

(i) Kuimarisha ukaguzi katika bandari na mipaka ikiwa ni pamoja na ufunguaji wa Ofisi mpya katika Kanda ya Magharibi (Kigoma) na Kanda ya Kusini (Mtwara);

(ii) Kuimarisha shughuli za ufuatiliaji katika soko na utoaji wa elimu kwa wadau ili kutambua na kuondoa bidhaa bandia sokoni;

(iii) Kushughulikia malalamiko juu ya uwepo wa bidhaa bandia sokoni kwa kufanya kaguzi za kushitukiza katika maeneo na maduka yanayodhaniwa kuwa na bidhaa bandia;

(iv) Kuimarisha ushirikiano na wadau wa biashara, ikiwa ni pamoja na Jumuiya za Wafanyabiashara hususan katika Soko la Kariakoo, wasambazaji na wauzaji ili kuunda umoja dhidi ya bidhaa bandia; na

(v) Kuimarisha mfumo wa kisheria unaohusiana na hatua za kudhibiti bidhaa bandia ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya sheria iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kusimamia uzalishaji na uingizaji bidhaa kwa kuzingatia ubora, usahihi wa alama na mahitaji ya nchi ili kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi na jamii, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kembaki.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali ambayo bado mimi sijaridhika nayo, ukienda katika maduka mengi ukitafuta bidhaa *genuine* huwezi kuipata. Je, maana yake ni kwamba Serikali haioni bidhaa hizi katika maduka yetu na katika soko ambalo lipo katika mitaa yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kumekuwa na viwanda vingi bubu ambavyo vipo katika mitaa yetu, vingine vinatengeneza *oil* chafu ambayo tunatumia kuweka kwenye magari yetu. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba viwanda hivi ambavyo vinatengeneza bidhaa ambazo hazikidhi viwango vinadhibitiwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Kembaki kwa kufuatilia masuala yanayohusiana na bidhaa bandia au bidhaa ambazo hazikidhi mahitaji katika soko letu. Ni kweli bado tuna changamoto ya bidhaa bandia, lakini siyo kweli pia kwamba hakuna bidhaa *genuine* katika maduka yetu kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge. Bidhaa zote zipo na niseme kuna watu ambao wanatumia nafasi hii moja kuingiza bidhaa hizi ikiwa ni sehemu ya kukwepa kodi na kufanya mambo mengine ambayo hayafai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bidhaa *genuine* zipo lakini pia na bidhaa bandia zipo na ndiyo maana tuna Sheria ya Ushindani ili kuhakikisha tunafuatilia na kukagua kwenye maduka ili tubaini. Hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa kwenye bidhaa ambazo ni bandia na tunashukuru kwamba wafanyabiashara na wazalishaji wanashirikiana na Serikali ili kutambua bidhaa ambazo siyo *genuine* katika maduka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili, viwanda bubu ambavyo vinaingiza na kuzalisha bidhaa bandia tayari hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa, moja ikiwa ni kuwakamata na kuchukua hatua kali dhidi yao. Haya yamekuwepo siyo tu katika bidhaa alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, lakini pia hata kwenye vinywaji.

Kwa hiyo, kuna wengine wanachukua vifungashio vya viwanda fulani halafu wanaweka bidhaa humo na kuanza kuuza mitaani. Kwa hiyo hatua zimekuwa zikichukuliwa ili kukabiliana na changamoto hii ya viwanda bubu, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Bahati Ndingo.

Na. 79

**Miradi ya Maji Jimbo la Mbarali**

**MHE. MASACHE N. KASAKA K.n.y. MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa Serikali kuhakikisha miradi ya maji katika Jimbo la Mbarali inakamilika kwa wakati ili kuondoa changamoto ya maji iliyopo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama Wilayani Mbarali umeongezeka kutoka wastani wa 54% mwaka 2023 na kufikia 58.4% mwaka 2024. Hali hiyo imechagizwa kutokana na kukamilika kwa utekelezaji wa miradi ya maji Kibaoni, Matebete, Luduga - Mawindi, Mkunywa Awamu ya Kwanza, Miyombweni na Utengule - Usangu. Kukamilika kwa miradi hiyo kumesaidia wananchi wapatao 70,582 waishio kwenye maeneo hayo kupata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji Chimala, Ruiwa na Igurusi Awamu ya Kwanza ambapo miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024 na kunufaisha wananchi 79,653 wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali itaanza utekelezaji wa Miradi ya Maji ya *Ilongo Group* Awamu ya Kwanza, Mbuyuni Awamu ya Kwanza, Itamboleo Awamu ya Pili, Iwalanje, Warumba, Vikaye, Isunura - Ikanutwa na Igunda - Muungano wilayani Mbarali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mahususi wa Serikali ni kuhakikisha inapeleka fedha zinazohitajika kwa wakati sambamba na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maji kote nchini ikiwemo Wilaya ya Mbarali ili miradi hiyo iweze kukamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji ya Chimala pamoja na Ruiwa, pamoja na kwamba utekelezaji wake umeanza, lakini unakwenda kwa kusuasua. Je, ni lini Serikali itatoa fedha ya kutosha ili miradi hii iweze kukamilika kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwenye Wilaya ya Chunya Serikali iliweza kuchimba visima 16 na tunashukuru kwa hilo. Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha kwenye Vijiji vya *STAMICO*, Upendo, Lualaje, *Supermarket*, Sipa na Nkwangu ili miradi hii iweze kutekelezeka na wananchi hawa waweze kunufaika na mradi wa maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Kasaka kwa swali ambalo ameuliza, lakini pia kuhusu upande wa Chunya amekuwa akifuatilia sana maeneo haya kuhakikisha kwamba katika vile visima 16, basi vinaendelea kutoa maji lakini katika vijiji ambavyo amevitaja, tunaendelea kuviweka katika mpango kuhakikisha kwamba vinapata huduma safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Chimala, kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, Serikali inaendelea kupeleka fedha kwa kadiri zinavyopatikana ili kuhakikisha kwamba miradi yote nchini ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji inakamilika na kuanza kutoa huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mradi mkubwa wa kisima kirefu cha maji cha Alailalai Kata ya Gelai Lubwa Wilayani Longido ulitengewa fedha tangu mwaka 2023 na mkandarasi alipatikana, lakini mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea. Je, nini mpango wa Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Catherine alishaulizia huu Mradi wa Longido na maeneo mengine ya Mkoa wa Arusha. Nampongeza sana kwa kuwa karibu na kufuatilia kwa ukaribu miradi ya maji katika Mkoa wa Arusha. Ni kweli kabisa mkandarasi hajaingia na sasa tupo katika hatua za mwisho kabisa kuhakikisha kwamba mkandarasi anaingia *site* na kuanza utekelezaji wa mradi huo, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Kumuyange na Ntobeye Wilaya ya Ngara hadi leo mkandarasi hajafika *site*. Je, ni lini utekelezaji wa mradi huo utaanza ili kuwatua ndoo wakina mama wa Kata ya Ntobeye na Kata ya Kigina?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum Kagera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera akiwemo Mheshimiwa Oliver kwa kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kwa kutetea miradi hii ambayo inaendelea kutekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upekee kabisa Mheshimiwa Semuguruka amekuwa karibu sana na kutusaidia mpaka kuainisha maeneo ambayo yanaweza yakawa na vyanzo vya maji ambavyo vinaweza kutusaidia kuhakikisha kwamba wananchi wa Ngara na Mkoa wa Kagera wanaendelea kupata huduma ya maji safi na salama. Mkandarasi huyu yupo katika hatua za mwisho za *mobilization* ili kuhakikisha kwamba anaingia *site* na kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mradi unaanza mara moja, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kijiji cha Sambaru Kata ya Mang'onyi Jimbo la Singida Mashariki ni miongoni mwa vijiji ambavyo ni vikubwa sana na kimsingi kilitakiwa hata kiwe kata, lakini akina mama wa Sambaru wanatumia muda mrefu sana na wanateseka sana kutafuta maji. Je, ni lini Serikali itapeleka mradi wa maji katika Kijiji cha Sambaru Kata ya Mang'onyi Jimbo la Singida Mashariki? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba tunamtua mama ndoo kichwani. Nampongeza

sana Mheshimiwa Nusrat kwa taarifa hii, na nimhakikishie tu kwamba baada ya Bunge lako hili, tutaonana ili anipe taarifa ya kina ili tuweze kuona ni sehemu gani hasa ambayo inahitaji huduma hiyo, nasi tutume wataalam wetu wakafanye usanifu na kujiridhisha kwamba mradi huo utahitaji kiasi gani, tuweze kuingiza kwenye mpango kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Saputu.

Na. 80

**Kukamilisha Miradi ya Maji Mikubwa na Midogo Nchini**

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani mahsusi kukamilisha miradi ya maji mikubwa na midogo nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini ambapo kupitia bajeti ya 2024/2025 jumla ya miradi 1,095 inatarajiwa kutekelezwa vijijini na miradi 247 mijini. Miradi hiyo inatekelezwa ili kufikia malengo ya Serikali ya kufikisha huduma ya majisafi na salama kwa asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha miradi ya maji yote mikubwa na midogo iliyopangwa kutekelezwa na inayoendelea na utekelezaji nchini inakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi. Mkakati mahsusi wa Serikali ni kuhakikisha inapeleka fedha zinazohitajika kwenye utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati sanjari na kusimamia utekelezaji wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali aliyoyatoa, nitakuwa na maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna miradi ya maji katika Kata za Oldonyosambu, Oldonyowas, Kimnyaki, Tarakwa, Siwandeki, Kiranyi, Oljoro na Naroi wakandarasi hawajalipwa fedha, ni lini sasa Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi hao ili miradi hiyo iweze kukamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, kwa kuwa miradi mingi ya maji hapa nchini imekwama kwa muda mrefu, kuna mingine yenye miaka miwili mpaka mitano, Serikali haioni ni wakati muafaka kuweka mkakati mahsusi kupata vyanzo vya uhakika vya fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo hapa nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saputu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Saputu kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya na aliweza kufuatilia kwa ukaribu sana maeneo ya Oldonyosambu na Siwandeti pamoja na Tarakwa. Napenda kutumia fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari imepeleka kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya hii Kata ya Oldonyosambu. Vilevile fedha hizi baada ya kupelekwa, tayari kuna mabomba ya chuma ambayo yamepelekwa pale kwa ajili ya kutandaza karibia kilomita tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Siwandeti, mzabuni anaendelea kuleta mabomba ya *plastic* na tunaratajia katika hizi

Kata za Siwandeti pamoja na Tarakwa mradi utakamilika ifikapo Desemba 2024, na kwa upande wa Olmuro *RUWASA*, mradi huu tayari umeshafikia asilimia 28 na tunaamini kabisa kwamba madai yale ambayo mkandarasi anaitwa *Help Desk* tayari amelipwa hati ya madai tarehe 28 mwezi wa Sita na tunaamini kabisa kwamba tayari ameshadudi *site* na tunamwomba ahakikishe mradi huu unakamilika kwa wakati kama ulivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upande wa miradi ambayo imekwama. Ni kweli kabisa tunatambua kuna miradi mingi ambayo ilianzishwa nchini na haijakamilika. Serikali kupitia Wizara ya Maji, na kwa kupitia Waziri wetu, tumeelekeza kuwa hakuna haja ya kuanza kutangaza miradi mipya na kupeleka pesa wakati kuna miradi ambayo imeshafikia 70% au 80% ama 90% inaachwa ina-*hang* halafu tunaanzisha mradi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelekeza Mameneja wote wa Mikoa wa *RUWASA* na Mameneja wote wa mamlaka mbalimbali wahakikishe miradi yote ambayo iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji inapelekewa fedha na kukamilika kwanza kabla ya kuanza kutangaza miradi mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo mkakati wa sasa ambao tunahakikisha kwamba tunaufuatilia kwa ukaribu ili kuhakikisha kwamba tunakamilisha miradi yote.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itaanza kuweka miundombinu katika visima ambavyo vimejengwa katika Kijiji cha Mtandika na Kituo cha Afya cha Ruaha Mbuyuni, kwa sababu muda mrefu vimechimbwa lakini hakuna miundombinu yoyote ya mabomba wala usambazaji?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika Kijiji cha Mtandika kuna hii changamoto na tunatambua kwamba kuna kisima Serikali imeshakichimba pale. Nimhakikishie kwamba Serikali tayari imeshajipanga kwenda kuhakikisha kwamba miradi yote inaenda kuwekewa miundombinu ili kuhakikisha kwamba inatoa maji safi na salama, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Paresso, kwa niaba ya Mheshimiwa Matiko.

Na. 81

**Mradi wa Maji Kijiji cha Mang'ola Juu – Karatu**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji uliokwama kwa muda mrefu katika Kijiji cha Mang'ola Juu Wilayani Karatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Kijiji cha Mang'ola Juu Wilayani Karatu. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa matenki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 270,000, ulazaji wa mtandao wa mabomba umbali wa kilometa 30, ujenzi wa vituo 25 vya kuchotea maji, ujenzi wa Ofisi ya *CBWSO*, ujenzi wa nyumba ya kuendeshea mitambo *(pump house)* na ujenzi wa mbauti tatu za kunyweshea mifugo *(cattle trough)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 30% ambapo umeanza kutoa huduma kwenye baadhi ya maeneo kupitia vituo saba vilivyokamilika wakati utekelezaji ukiendelea. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024 na kunufaisha wananchi 5,616 waishio kwenye vijiji cha Mang'ola Juu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ila niseme tu nasikitishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Ni kweli kabisa kwamba mradi huu wa Mang'ola Juu umeanza ni takribani miaka mitatu sasa na umekuwa ukisuasua, umefikia 30% tu. Je, Serikali haioni kwamba mradi huu unakosa *value for money?* Serikali inachukua hatua gani za dharura kuhakikisha kwamba wananchi wa Mang'ola Juu wanapata maji kwa wakati kama ilivyokusudiwa hapo awali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, tuna mradi wa maji wa Ziwa Victoria ambao unatoka kwa wananchi wa Rorya, Tarime Mjini na baadhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, lakini mradi huu nao utekelezaji wake umekuwa ukisuasua na ulitarajiwa kukamilika mwaka 2025, lakini mpaka sasa hivi ni 12.5% tu zimetekelezeka na mkandarasi ameondoka *site* kwa sababu ame-*rise certificate* ya *4.3 billion,* hajalipwa mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inakuwa na uhalisia wa utekelezaji wa miradi hii ya maji ili wananchi wa Tarime wajue kwamba kufikia 2025 ni kweli mradi huu unaenda kutekelezeka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ambavyo limeulizwa na Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi unapoanza, tunaanza na *feasibility study* na baada ya hapo tunafanya usanifu na baada ya hatua zote hizo ni utekelezaji wa mradi. Unapoanza kwenye upembuzi yakinifu, usanifu, hizo zote ni hatua, lakini sasa tunapokuja kwenye *execution* ya mradi ndipo sasa tunapoona kwamba zile asilimia zinapofikia tunaelewa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa, nakiri kwamba mradi huu ulianza miaka mitatu iliyopita, lakini kuanza rasmi ujenzi wenyewe hauna muda mrefu kama ambavyo Mheshimiwa ameugusia. Ninachotaka kusema ni kwamba Serikali imejidhatiti kuhakikisha kwamba miradi hii, kwa sababu lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunaendelea na falsafa ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani, tutahakikisha mradi huu wa Mang'ola Juu unakamilika kwa wakati na wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo linaenda sambamba na suala la mradi wa Ziwa Victoria kutokea kule Rorya. Ni kweli nakiri kabisa kwamba tulipata changamoto na mkandarasi hapa katikati, lakini tayari tuko kwenye mazungumzo naye ili kuhakikisha kwamba anarudi *site* na kuhakikisha kwamba mradi unaendelea wakati mahitaji yake na madai yake yanaendelea kufanyiwa kazi na Serikali, kwa sababu tunajua kabisa kwamba Tanzania hii tutaijenga sisi wote na wakandarasi ni Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Waziri, jibu maswali kwa kifupi sana. Mheshimiwa Maleko.

**MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate nafasi kwa swali namba 84.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Je, ni lini mradi unaoendelea katika Kata ya Mwika Kusini utakamilika? Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari tuongozane mguu kwa mguu kwenda kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa sababu wananchi hawa wanateseka sana kwa shida ya maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kuongozana mguu kwa mguu, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Chaya.

Na. 82

**Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo Sanza na Kintinku**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Mahakama za Mwanzo za Sanza na Kintinku?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Chaya kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Tanzania inaendelea kutekeleza mpango wake wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama kwa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 katika ngazi mbalimbali za Mahakama. Kutokana na uhaba wa majengo ya Mahakama, majengo haya yanajengwa na kukarabatiwa kwa

awamu kwa kuzingatia mpango huo na kadri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu unatarajia kukamilika mwaka 2025/2026 na sasa hatua za kuuhuisha zinaendelea ambapo majengo ya Mahakama ya Mwanzo Sanza na Kintinku yatajumuishwa katika mpango huo. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunafahamu wananchi wanapata adha kubwa sana ya kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya kufuata huduma za Mahakama katika Makao Makuu ya Wilaya na kwa kuwa tuna uhaba wa Mahakama za Mwanzo, nini mkakati wa Serikali wa kuweka mifumo ya TEHAMA katika Mahakama za Mwanzo ili kupunguza adha ya kusafiri na kutumia gharama kubwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Swali la pili, kwa kuwa mpango wa kujenga Mahakama za Mwanzo utaanza mwakani kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Naibu Waziri, nini sasa mkakati wa Serikali wa kutumia *mobile court* (Mahakama Tembezi) kwa maeneo ambayo ni *hard to reach* ili tuwawezeshe wananchi wanaokaa maeneo ya mbali waweze kupata hii huduma? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umuhimu wa kuweka TEHAMA katika Mahakama za Mwanzo, nakiri kwamba hiyo hali ndiyo mwelekeo wetu wa Idara yetu ya Mahakama ambapo kwa Mahakama za Mwanzo zilizopo katika miji kwa maana mijini kama *Primary Courts in the cities* na

kwenye *municipalities* tayari wameshaunga na mfumo wa TEHAMA, lakini kule vijijini changamoto tunayokutanayo ni kwamba Mkongo wa Taifa haujafika kwenye maeneo yale, kwa hiyo, kadri Serikali inavyoendelea kupanua huduma za Mkongo wa Taifa na umeme vijijini na kuzifikia sehemu zenye Mahakama za Mwanzo, Mahakama pia zitaingiza utaratibu wa TEHAMA ili kuwarahisishia wananchi kufanya mawasiliano na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *mobile courts,* tunatambua kwamba yapo maeneo kweli ni makubwa na hayana majengo ya Mahakama na *mobile courts* hizi zinahitajika ili kuwafikia wananchi. Ni kwa kutambua hilo hivi sasa Mahakama imeshanunua *mobile courts* sita na zitakapokuwa zimewasili zitapelekwa kwenye maeneo yenye mtawanyiko mkubwa kama Manyoni kwa Mheshimiwa Mbunge ili wananchi walioko maeneo ya mbali waweze kufikiwa, na kadri hali ya fedha itakavyoimarika *courts* hizo pia zitanunuliwa na maeneo mengine yaweze kufikiwa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Mganga Nicodemas.

Na. 83

**Ahadi ya Kuchimba Malambo - Mbogwe**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuchimba malambo kwa ajili ya mifugo ili kurahisisha shughuli za ufugaji Mbogwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo mbalimbali

hapa nchini ikiwemo katika Jimbo la Mbogwe. Aidha, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kujenga mabwawa na kuchimba visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo, bado mahitaji ni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuchimba malambo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe lipo kwenye Mipango ya Serikali. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti halikuweza kuzingatiwa kuingizwa kwenye vipaumbele vya mwaka 2024/2025. Pamoja na hayo, Serikali inaendelea kuliweka suala hili kwenye mipango ijayo ya utekelezaji wa bajeti kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nashukuru kwa majibu ya Serikali japokuwa sijaridhika, naomba kuuliza maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2021 aliyekuwa Waziri wa Mifugo alikuja Lulembela Namasumbo akawaahidi wananchi wa Mbogwe kwamba atatekeleza bajeti ya 2023. Je, lini Serikali itachimba hayo malambo yaliyoahidiwa na Serikali mwaka 2021?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ukurasa wa 54 tuliwaahidi wananchi wafugaji wa Mbogwe kwamba tutatenga maeneo kwenye hifadhi zetu ya Kigosi maeneo ya kufugia, lini sasa hiyo ahadi itatekelezwa ili wananchi waweze kupewa hayo maeneo ya kuchungia ng'ombe? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Waziri Mstaafu wa Mifugo Mheshimiwa Mashimba Ndaki alipotembelea mwaka 2021/2022 kule kwenye Jimbo la Mheshimiwa Maganga alitoa ahadi ya kuchimba

mabwawa kwenye maeneo ya wafugaji na baada ya hapo Wizara ilichokifanya ilichukua ahadi hizo na kuziingiza kwenye mpango wa Serikali. Ndiyo maana nimesema katika jibu la msingi kwamba mpango wa Serikali upo na tunatambua ukame mkubwa uliopo katika Jimbo la Mbogwe, Nyangw'ale pamoja na Bukombe. Huo ukanda wote una hali ngumu sana ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo yetu na baada ya hapo tuliingiza kwenye mpango, na mpango huo baada ya upatikanaji wa fedha tutakwenda kutekeleza uchimbaji wa mabwawa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inao mpango wa kwenda kuchimba mabwawa katika maeneo hayo, hivyo awe na subira, tutakwenda kuchimba kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake hili la pili la kutenga maeneo ya wafugaji. Jambo hili liko chini ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa sababu hawa ndio wenye maeneo ambapo wanao uwezo wa kupanga kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi, kwamba Serikali za Vijiji sasa zinaweza zikaamua kwamba eneo hili wafuge, eneo hili walime na eneo hili wafanye kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbogwe akae na wataalam wake watenge maeneo ya wafugaji ili wafugaji hao waweze kupata maeneo ya malisho kadri ambavyo maeneo hayo yanavyowaruhusu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Mahawanga.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, naomba swali lake namba 84 lipatiwe majibu ya Serikali.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Wewe vipi mimi nimeleta karatasi.

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini, Mheshimiwa Anatropia. Mheshimiwa Dkt. Ntara.

Na. 84

**Ujenzi wa *Fly Over* kuanzia Magomeni – Jangwani – *Fire***

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza rasmi ujenzi wa Daraja kuanzia Magomeni - Jangwani - *Fire* ili kuondoa adha wanayopata Wananchi wakati wa mvua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TANROADS* imepanga kujenga daraja katika eneo la Jangwani lenye urefu wa mita 390 na kimo cha mita 15. Ujenzi wa daraja hili utatumia fedha za mkopo nafuu wa Benki ya Dunia. Taratibu za manunuzi ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa daraja hilo zipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba na unatarajiwa kuwa umesainiwa ndani ya mwezi Septemba, 2024, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu hayo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo: -

Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa mradi wa Bonde la Mto Msimbazi *(Dar es Salaam Metropolitan Development Project Phase Two)*?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali imejipangaje kuwalipa fidia wananchi wanaoishi katika eneo la mradi wa ujenzi wa Daraja la Jangwani kuanzia Magomeni, Jangwani hadi *Fire?* Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ujenzi wa Daraja la Jangwani tunafanya kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa maana ya ujenzi wa kingo za Mto Msimbazi pamoja na maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Suala la fidia linaenda sambamba na jitihada hizi za ujenzi kupitia Mradi wa *DMDP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, Serikali tumejipanga, Wizara ya Ujenzi wakati tunajenga Daraja. Pia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia mradi wa *DMDP* tutashirikiana kuhakikisha ujenzi unaenda sambamba na fidia kwa wananchi, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Barabara ya Itoni - Lusitu ambayo imesimamisha ujenzi kwa takribani 10, na miezi mitatu ijayo mvua itakuwa imeanza. Kwa hiyo, barabara hii kama haitaanza kujengwa, mwaka mzima mkandarasi yupo *offsite* hakuna kinachoendelea, Serikali ina mpango gani kuendeleza ujenzi wa barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Mwanyika, ameulizia barabara ya Itoni – Lusitu. Habari iliyo njema ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge pochi

ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imeanza kufunguka. Tumeanza kupokea fedha kwa ajili ya *advance payment* ikiwemo barabara hii ya Itoni – Lusitu. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, mmefuatilia *advance payment* kwa muda mrefu. Sasa hivi pochi ya mama imefunguka, tutaanza kutoa *advance payment* kwenye barabara hii pamoja na barabara nyingine, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Barabara ya kutoka Mogabiri – Nyamongo – Serengeti, Mkandarasi ametoa vifaa *site* na anaidai Serikali shilingi bilioni 7.8. Barabara hii inahudumia Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Serengeti. Mheshimiwa Waziri, nini kauli ya Serikali juu ya ujenzi wa barabara hii kuendelea ili kutoa matumaini kwa watu wa Tarime?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waitara, amekuwa akiifuatilia barabara hii kwa ukaribu sana na habari iliyo njema ni kwamba, zile *advance payment* tulizozipata, barabara hii pia ni miongoni mwa hizo barabara. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waitara kwa ufuatiliaji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu umekwenda, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mtanda.

Na. 85

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege – Newala**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga upya Uwanja wa Ndege wa Newala ambao umeharibika kwa kiasi kikubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Newala ipo katika hatua za kufanya tathmini ya uchaguzi wa eneo jipya kufuatia eneo la sasa kutofaa kwa ujenzi wa kiwanja cha ndege. Baada ya kukamilika kwa tathmini ya eneo hilo ambalo tayari limeshajumuishwa kwenye Ramani ya Mipango Miji Na.03/NEW/31/04/2021, taratibu za utwaaji na umilikishwaji wa ardhi zitafanyika. Taratibu za utwaaji na ukamilishaji zitakapokamilika, fedha za ujenzi wa kiwanja cha ndege zitatengwa kwa ajili ya bajeti husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naishukuru Serikali kwamba imeona umuhimu wa uwanja ule kwa sababu ni uwanja ambao ulitumika kukomboa nchi za Kusini mwa Afrika na ule ni miongoni mwa viwanja hivyo. Kwa hiyo, nataka kujua kama Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kwenda Newala ili kuona hali ya uwanja ule?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kwamba, ni zaidi ya miezi mitatu sasa imepita tangu mkataba wa jengo la abiria kwenye uwanja wa Mtwara usainiwe, lakini mkandarasi hajalipwa *advance payment* ili ujenzi huo uanze. Je, ni lini Serikali italipa *advance payment* ili ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa Mtwara uanze kujengwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali napokea shukurani, na ninaomba shukrani hizi ziende kwa Rais wetu mpendwa ambaye anajenga viwanja takribani nchi nzima. Pia, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya kutembelea eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili amezungumza kuhusiana na jengo la abiria Mtwara. Serikali katika awamu ya kwanza imefanya kazi kubwa ya kujenga *runway* katika uwanja wa Mtwara, kuweka taa za barabarani, maegesho, na kadhalika. katika hatua ya pili Serikali imeshasaini mkataba wa takribani shilingi bilioni 67 ambapo tunajenga jengo la abiria, *control tower*, jengo la zimamoto, hali ya hewa, na kadhalika. Vilevile, hivi ninavyozungumza tayari mkandarasi amekabidhiwa *site* na ujenzi unaanza mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, muda wetu umekwenda na tuna Miswada miwili. Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Mkenge kwa niaba ya Mheshimiwa Mbogo.

Na. 86

**Mgogoro wa Ardhi Kata ya Kala, Ninde na Wampembe - Nkasi Kusini**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE K.n.y. MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaenda kutatua migogoro ya ardhi ya Kata ya Kala, Ninde na Wampembe - Nkasi Kusini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Nkasi Kusini ni moja ya majimbo yaliyonufaika na Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Milki za Ardhi nchini *(Land Tenure Improvement Project - LTIP)* unaotekelezwa na Wizara kupitia mkopo wa Benki ya Dunia, ambapo Kata ya Kala ni moja kati ya Kata nufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Kala awali ilikuwa na mgogoro na hifadhi ya msitu wa Loasi kutokana na vijiji vya Kilambo, Mlambo, King'ombe na Mpasa vilivyokuwa katika Kata hiyo kuanzishwa ndani ya Hifadhi. Migogoro ya vijiji hivyo ilitatuliwa kufuatia utekelezaji wa Uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro katika vijiji 975 ambapo vijiji husika vilimepewa ardhi yenye ukubwa wa jumla ya hekta 10,828 kutoka Hifadhi ya Msitu wa Loasi. Aidha, utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri ulihusisha uundaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutatua migogoro yote iliyobaki katika Jimbo la Nkasi Kusini ili kuhakikisha kuwa wananchi wanafanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii kwa amani. Aidha, wananchi wanaombwa kuendelea kusimamia kikamilifu mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji iliyoandaliwa ili kuwa na matumizi endelevu ya ardhi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, ni lini sasa Serikali itaanzisha mpango maalum wa usuluhishi baina ya mtu na mtu katika masuala ya ardhi ili kupunguza migogoro ya kesi za ardhi Mahakamani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea na mikakati mbalimbali

ikiwepo eneo moja ambalo tunalifanyia kazi kwa kasi kubwa sana linaloitwa Kliniki ya Ardhi ambapo wale wanaogombana tunawakutanisha, kuwaweka sawa na nia ya kuwapatanisha inakuwepo pale. Hata hivyo, kuhusu masuala ya kupelekana Mahakamani, nadhani watu wengine ni kwa sababu huko mwanzo tulikuwa hatujawa wazi sana juu ya hizi Kliniki na kwa sasa tumeacha mlango wazi na tunaendelea na zoezi hili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano, Mheshimiwa Juma Hamad, kwa niaba yake Mheshimiwa Festo.

Na. 87

**Changamoto ya Mawasiliano Kijiji cha Kandwi – Chaani**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. JUMA USONGE HAMAD** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatuma wataalamu kwenda Kijiji cha Kandwe kilichopo Wilaya ya Kaskazini Unguja ili kutatua changamoto ya mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kufikisha huduma za mawasiliano katika pande zote mbili za Muungano kwa kushirikiana na watoa huduma. Kwenye mradi wa kufikisha mawasiliano katika Shehia (Kata) 38 Visiwani Zanzibar uliokamilika mwaka 2022, Kijiji cha Kandwi kilijumuishwa katika mradi huu na Kampuni ya Tigo – Zantel ilipewa jukumu la kufikisha mawasiliano katika Kijiji hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeiagiza *UCSAF* kufika katika Kijiji cha Kandwi kufika wiki ya kwanza ya mwezi huu Septemba kwa lengo la kufanya tathmini ya kina ili kubaini kama kuna eneo lolote lenye changamoto ya mawasiliano liweze kutatuliwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mwenye swali yuko kule nyuma ningeomba aulize.

**NAIBU SPIKA:** Amesharudi?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, yupo.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Swali langu ni kwamba, je, ni lini mtaweka *commitment* ya kwenda kwenye Kijiji cha Kandwi ili kujionea hasa mazingira ambayo wananchi wangu wa Kandwi wanakosa huduma ya mawasiliano ukilinganisha na maeneo mengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Juma kwa ufuatiliaji mzuri, lakini naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba tayari timu yetu imefika kwenye Jimbo lake eneo hili la Kandwi na tayari wameweza kuona changamoto ambayo ipo, hasa ni miembe mingi ambayo ipo katika lile eneo. Hata hivyo, kama Wizara, tayari tunafanyia kazi na kuhakikisha kwamba mapema iwezekanavyo tunakuja kuhakikisha maeneo haya ya Kandwi yanapata mawasiliano ya uhakika Mheshimiwa Juma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo swali la upendeleo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu kwa Wizara ya Habari, Mheshimiwa Naibu Waziri anakubaliana nami kwamba vitendo vya utapeli mitandaoni vimezidi? Je, Wizara ya Habari haioni haja ya kusitisha usajili wa laini kiholela mitaani hasa watu waende kujisajili kwenye maduka maalum ya hii mitandao ya simu kama nchi jirani wanavyofanya ili kudhibiti utapeli huu ambao umekuwa ukiumiza na kugharimu Watanzania wengi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga kuhusu utapeli mitandaoni. Nampongeza sana kwa ufuatiliaji, lakini vitendo hivi vya utapeli tayari *TCRA* inaendelea kudhibiti na mojawapo, kwanza tume-*restrict* sana mikoani maeneo ambayo watu wanapata usajili sasa hivi siyo kila mahali. Kwa hiyo, tutaendelea kuona namna njema ya kuweza kuruhusu hawa wanaotoa huduma ya usajili tunaendelea kuwadhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama tutaongeza *scope* ya kuona kwamba wanaweza kufikiwa, lakini vilevile kuhakikisha kwamba hali ya usalama na hali nzuri ya mawasiliano inaendelea kuboreshwa. *TCRA* wanafanya kazi nzuri sana katika hili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita mwenye nyumba Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmeshauliza maswali kwa Serikali na ninyi mmeshapata majibu. Sasa nilete tangazo la wageni

walioko hapa Bungeni. Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Ngoja, natafuta tangazo la Spika hapa ili ndiyo lifuate la wageni wengine. Sijui leo hawa wasaidizi wamepangaje haya majina.

Haya tunaanza na Wageni watano ambao ni wageni wangu kutoka Bunge la Muungano wa Visiwa vya Comoro. Hapo yupo Mheshimiwa Moustadroine Abdou ambaye ni Spika wa Bunge la Muungano wa Visiwa vya Comoro, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia ameongozana na Mheshimiwa Hamada Bacar - Naibu Spika, ameongozana na Mheshimiwa Mistoihi Abdou Rahim, Mbunge; Mheshimiwa Soulaimane Houssene, Mkurugenzi; yupo pia Ndugu Abdoulwahab Ali Aziri, Mshauri wa Mheshimiwa Spika; Ndugu Habib Athmani Zongo, Afisa Dawati wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Ndugu Manfred Mapunda, Afisa Itifaki, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii ni ziara ya kwanza ya Spika wa Bunge la Visiwa vya Comoro kutembelea Bunge letu tangu nchi zetu mbili zilipoanzisha Uhusiano wa Kidiplomasia. Kwa hiyo, tunawakaribisha sana wageni wetu, karibuni sana. Hata hivyo, tunaamini kwamba ziara hii itaendelea kukuza uhusiano kati ya Bunge letu na Bunge la Muungano wa Visiwa vya Comoro na pia uhusiano kati ya nchi hizi mbili. Kwa hiyo, tunawakaribisha sana, karibuni sana.

Pia nitumie fursa hiii kumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, ameongozana na mgeni wetu tangu alipompokea na sasa yuko nao hapa. Tunakushukuru sana Mwenyekiti kwa kazi nzuri, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya Ulinzi na Usalama kutoka Bunge

la Seychelles, wakiambatana na Maafisa wanne kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hawa ni Mheshimiwa Francois Adelaide, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Audrey Vidot, Mjumbe; Mheshimiwa Doyace Porice, Mjumbe; Mheshimiwa Michel Roucou, Mjumbe; Ndugu Gillian Samson, Katibu Kamati; Ndugu Donna Chetty, Katibu Kamati Msaidizi; Ndugu Maria Ndumbaro, Afisa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Ndugu Sasieli Manongi, Afisa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jerry na Mheshimiwa Zainab Katimba.

Tunao Wageni wanne wa Mheshimiwa Spika, kutoka Shirika la *African Evangelistic Enterprise Tanzania;* Yupo Jaji Mstaafu Dkt. Engela Kileo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini; Ndugu Godlisten Moshi, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi; Ndugu Robert Charles, Afisa Mtendaji Mkuu; Mchungaji Elikana Gonda, *Chaplain* wa Bunge (kwa nafasi yake), karibu sana.

Wapo wageni wengine watatu ambao ni wageni wangu kwangu kutoka Soko la Hisa Dar es Salaam *(Dar es Salaam Stock Exchange)* na hawa ni Ndugu Peter Nalitolela, Afisa Mtendaji Mkuu; Ndugu Benjamin Baraka, Mkurugenzi Miradi; Ndugu Leonard Kameta, Meneja Maendeleo ya Biashara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mwimbaji wa Bongo Fleva na Mwanzilishi wa Programu ya Afya ya *The Talk with Abigail Chams* ameambatana na Meneja wake ambaye ni kaka yake. Sasa yeye mwenyewe anajulikana kama Abby Chams, lakini huyu ni Abigail Chamungwana, karibu sana.

Yupo pia Ndugu Gabriel Chamungwana, Meneja wake; yupo Ndugu Abraham Chamungwana ambaye ni kaka yake, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hawa ni viongozi kutoka Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Yupo Ndugu Crispin Chalamila, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU; Ndugu Neema Jamu, Mwakilishi wa Katibu Mkuu Ikulu; Ndugu Sabina Seja, Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa TAKUKURU; Ndugu Joseph Mwaiswelo, Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma TAKUKURU; Ndugu Ismail Selemani, Mkurugenzi Msaidizi Oparesheni za Uchunguzi TAKUKURU; Ndugu Lizzy Kiwia, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Sheria TAKUKURU. Hebu simama tena Ndugu Lizzy Kiwia. Karibu sana Bungeni. Pia yupo Ndugu Martha Mashuki, Afisa Mwandamizi Ofisi ya Rais Ikulu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, ambao ni Ndugu Arjun Mittal halafu na Ndugu Atul Mittal ambaye ni Baba wa Arjun Mittal. Huyu Arjun Mittal ni mwanzilishi wa Kampeni ya Hedhi Salama Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wengine ambao ni wageni wenu; wageni 45 wa Mheshimiwa David Ernest Silinde - Naibu Waziri wa Kilimo, hawa ni Walezi na Wanakwaya wa Mtakatifu Bikira Maria kutoka Jimbo la Tunduma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wenginei ni wageni 80 wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ambao ni vikundi vya mazoezi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah ambaye ni mwanafunzi wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* kutoka Pemba, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Mchungaji kutoka Jimbo la Muhambwe, Kigoma, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Anna Lupembe, Naibu Mkurugenzi na Meneja wa Shirika la *Global Communities* kutoka jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Grace Tendega, Ndugu zake kutoka Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Walimu 25 wa Shule ya Sekondari Isongole kutoka Tukuyu Mkoa wa Mbeya, ahsante sana na karibu sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wapo Ndugu Mayunga Mabisi wa Parokia ya Kanisa Katoliki Mecco kutoka Jijini Mwanza; Mwalimu John Seleman kutoka Ilemela Jijini Mwanza; wanafunzi 19, Walimu na Viongozi 14 wa Shule ya Sekondari Istiqaama kutoka Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wanafunzi 38 na Walimu sita wa Shule ya Sekondari Ibugule kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 80 na Walimu watano wa Shule ya Msingi ya *Rainbow Christian Junior* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao Bungeni siku ya leo, na wengine kadri watakavyopata nafasi ya kuingia hapa Bungeni tutaendelea kuwatangaza.

Lipo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo tarehe 2 Septemba, kutakuwa na semina kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na matumizi ya takwimu zilizoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS)* itakayotolewa na Wizara ya Fedha. Semina hii itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa saa 9.00 alasiri, ama kama muda utabadilishwa nadhani wahusika watawasiliana nanyi Waheshimiwa Wabunge.

Baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, hoja ya dharura.

**SPIKA:** Hoja ya dharura, Mheshimiwa Ng'wasi Kamani.

**HOJA YA DHARURA**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niweze kuweka mbele yako jambo la dharura. Nasimama kwa kanuni ya 54 ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kwa sababu ya muda nitaomba nisiisome.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *TAWA* iliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii tarehe 31 mwezi wa nane siku ya Jumamosi walitoa tangazo la nafasi za ajira, ajira 351; tatu ni za udereva, nafasi 200 za *Conservative Rangers* na nafasi 145 za ma-*technician*. Kati ya vigezo vya waombaji au kigezo muhimu kwa waombaji wote hawa 351 ilikuwa ni wote wanatakiwa kuwa na umri usiozidi miaka 25, yaani wawe na umri wa miaka 25 kushuka chini.

Mheshimiwa Spika, katika vigezo vingine, kwa mfano kwenye udereva, anatakiwa awe na vyeti vyote vya *VETA* na leseni, lakini awe na uzoefu wa mwaka mmoja wa udereva, lakini kwenye hivi vingine wanatakiwa kuwa na vyeti vya maliasili ambavyo vyeti hivi unaweza kuwa na *certificate, diploma* au *degree*.

Mheshimiwa Spika, kwa elimu yetu ya kawaida kabisa, mwanafunzi anamaliza Kidato cha Nne akiwa na miaka 18, lakini akienda mpaka *Form Six* ana miaka 20 na akiingia chuoni maana yake kama ni *certificate* anaweza akamaliza akiwa na miaka 21 au 22; na akienda mpaka *degree* maana yake ni miaka 23 mpaka 24.

Mheshimiwa Spika, waombaji wote wanatakiwa kuwa na umri usiozidi miaka 25. Sasa ukizingatia nafasi hizi huwa zinatangazwa kwa uchache, wahitimu tulionao kule nje ni wengi, lakini nafasi hizi

huwa zinatolewa baada ya muda mrefu sana. Matangazo haya mara ya mwisho yametangazwa ni muda mrefu, mpaka juzi ndipo limetangazwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiruhusu kupitia kanuni hii, naomba nitoe hoja ili Bunge hili liahirishwe na lijadili ili ikiwezekana basi, umri wa waombaji uongezwe ili vijana wetu walioko mtaani wenye sifa hizi wasinyimwe haki ya kuomba na kupata nafasi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawasilisha. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Hebu naomba hilo tangazo. Mheshimiwa Ng'wasi, nisaidie hilo tangazo, sina hapa. Msaidizi kachukue tangazo. Mheshimiwa Waziri kabla sijaitoa hii hoja ili kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Mbunge ili aweze kutoa maelezo ya hoja yake, hiki kigezo cha miaka 25, kina sababu zozote? Mheshimiwa Waziri ulikuwa umesimama. Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba ku-*respond,* niseme kwa swali ambalo limeulizwa au hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Kamani, kwamba *TAWA* ni Jeshi Usu, na vyombo hivi vyenye aina ya mafunzo ya kijeshi umri ni kigezo muhimu sana katika kupima ukakamavu na uwezo wa kupokea mafunzo ya kijeshi. Kwa hiyo, wenzetu wa *TAWA* kwa uzoefu walionao na mahitaji wanayoyahitaji kwa nguvukazi wanayoihitaji wanadhani kwamba umri wa miaka isiyozidi 25 unaweza kumwezesha huyu mwanajeshi wanayemwandaa aweze kwenda kupambana na mazingira ya majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba nafasi zilizotangazwa hizi si nafasi za *graduates* tu. Kama ni *graduates,* watasubiri nyingine zitakapotangazwa kwa sababu Serikali inatoa ajira nyingi sana, lakini

hawa kwa kweli tunawahitaji wanajeshi wanaokwenda kwenye *training;* waruke vihunzi, wapambane huko porini. Kwa hiyo, ni kazi kubwa kidogo, huwezi kumchukua mtu mwenye miaka 35, 40 au kwa sheria ya utumishi ajira tunatoa mwisho umri usiozidi miaka 45. Ukimchukua mtu wa miaka 45 hakika kwenye mafunzo haya hawezi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mafunzo haya ni ya kijeshi na kwamba wanaotakiwa ni Watanzania hao hao na wapo sokoni wengi na nafasi hizi zenyewe hazitoshi kabisa kuweza kuwachukua. Kwa hiyo, tunadhani kwa madhumuni hayo kwa kweli ndiyo dhamira ya *TAWA,* na tangazo hili limetangazwa na Sekretarieti ya Ajira na wamezingatia vigezo hivyo kama nilivyovisema, ahsante.

**SPIKA:** Umesema hili ni Jeshi Usu? Kuna tofauti yoyote kati Jeshi Usu na Jeshi la Watanzania? Viko sawa ama hakuna tofauti ya Jeshi Usu na hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, Jeshi Usu na majeshi mengine yanatofautiana. Mafunzo yanayotolewa kwa Jeshi Usu; na ndiyo maana kwa Kiingereza tunasema *paramilitary.* Ni ya aina ya kijeshi lakini majukumu yake kutokana na nidhamu yake na aina ya kiwango cha ukakamavu unaohitajika ndiyo maana hawa wahusika wanapata *training* zenye ujeshi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa maana ya tangazo lilivyotoka, linawahitaji hawa wa kada za kawaida kama *technician* ambao ndio dhamira yetu, kwamba wakienda kwa mfano madereva, sio kwenda tu kwenye udereva, ni lazima pia kuwe kuna mafunzo ya kijeshi na watafanya kazi zenye aina ya uanajeshi katika *operations* zao. Kwa hiyo, ndiyo maana tumesema hata kama ni dereva, lakini siyo tu kuendesha gari, lazima uwe na sifa nyingine ya umri ili uweze kupata nguvu na uwezo wa kupambana na yale majukumu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama hapa Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani akitaka tutumie Kanuni ya 54 ili tuweze kujadili jambo la dharura, na ameeleza hapa kwamba udharura wa jambo hili unatokana na kwamba kuna vigezo ambavyo vimewekwa kwenye tangazo la ajira ambalo limetoka hivi karibuni, tangazo ambalo litawazuia baadhi ya vijana kupata nafasi kwenye hizi nafasi ambazo zimetangazwa na *TAWA*.

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili leo siyo mara ya kwanza kujitokeza hapa Bungeni kuhusu vigezo vya ajira vinavyotolewa kwenye maeneo mengi. Maeneo haya ya jeshi na Jeshi Usu pia yameshawahi kujitokeza huko nyuma. Nadhani kwa makubaliano ya wakati huo, sinayo hapa, lakini nakumbuka nadhani tulisema kwa upande wa jeshi kwa sababu wana vigezo vya ziada, waachwe hivyo; na hizi taasisi nyingine ziangalie nafasi zile ambazo hazihitaji hicho kigezo cha watu kupitia mafunzo hayo ambayo pengine kwa namna Mheshimiwa Waziri alivyoyaeleza waweze kuchukua hivyo vigezo vya ziada halafu mtu apelekwe yale mafunzo ya kawaida kabisa.

Sasa kwa sababu huwa linajitokeza kwenda na kurudi, nadhani ni muhimu Serikali ipate ushauri wa Bunge leo ili ushauri ule watakaoutoa Wabunge hapa mweze kuuchukua upande wa Serikali. Kwa nini? Kwa sababu nilikuwa napitia hilo tangazo ambalo nimeletewa bahati mbaya simu sasa si huwa zina vile vitu vya kubonyeza, nimemrejeshea mwenyewe, lakini nilianza kwa kusoma kazi za dereva ambaye ameambiwa pale kwa sababu kaambiwa vigezo, pia shughuli atakazokuwa anazifanya huyo dereva.

Zile shughuli zilizoandikwa pale hii miaka 25 sijaelewa, labda Mbunge kwa sababu nataka kuitoa hoja, nitampa nafasi atusomee mfano tu wa huyo dereva halafu tuone ni namna gani huyu dereva tunasema akaruke viunzi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ng'wasi Kamani kwa dakika tatu elezea hoja yako, itoe kwa Bunge kama utaungwa mkono, Bunge litapata nafasi ya kuishauri Serikali.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nikianza kwa kusoma majukumu ya nafasi ya nafasi za udereva:-

(i) *To drive the Authority's vehicles;*
(ii) *To maintain vehicle logbook and movement records;*
(iii) *To maintain smooth running of vehicles;*
(iv) *To make simple repair of the vehicles;* na
(v) *To maintain vehicle cleanliness and service schedule*.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivi ni vya dereva yeyote wa kawaida kabisa mwenye mafunzo, mwenye cheti aliyepitia kwenye mafunzo ya udereva. Sambamba na alichokisema Mheshimiwa Waziri, tumekuwa na hoja hizi za vigezo kwa muda sasa katika Bunge lako Tukufu. Uliwahi pia kutoa mwongozo kwamba pale ambapo panahitaji mafunzo mahsusi, basi watu wawe wanaingizwa kwa vile vigezo vya kawaida na wanakwenda kupewa mafunzo kulingana na kazi watakazofanya.

Mheshimiwa Spika, pia tangazo hili katika vigezo vyake, linataka kwamba hawa watu wawe ni *graduates.* Mheshimiwa Waziri amesema hizi siyo nafasi kwa ajili ya *graduate,* bali ni watu wa kawaida kabisa. Vigezo vinataka mtu anaye-*apply* kazi hizi awe ni *graduate* aidha wa *certificate diploma* au *degree*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna chuo pale *MWEKA* kinachotoa hizi *Wildlife Conservation Certificate,* Moshi. Kinaitwa *MWEKA* ambacho chenyewe kinatoa *degree* ya miaka mitatu. Sasa mtu akimaliza *form six* aje aende akasome *degree,* anamaliza ana miaka kama siyo 23 ni 24, ana mwaka mmoja tu kwa ajili ya kupata nafasi hizi.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri, nafasi hizi ni chache, *graduates* wetu ni wengi, na hawa watu tusiwahukumu kwa uchache wa nafasi ambazo tunaweza kutoa. Tuwahukumu kwa uwezo wa kazi ambazo tunataka kuwapa. Kama sisi wenyewe hatujatangaza nafasi za kutosha, watu

tumewasomesha, wako mtaani na hawana kazi, sasa hivi umri hausimami, mtu ana miaka 26, 27 hata kama hatutafikisha 40 walau tuongeze mpaka 30 ili watu waombe kazi wakapewe mafunzo waweze kuingia katika nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja Wabunge wenzangu waniunge mkono ili tulijadili katika Bunge hili. *(Makofi)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa wengine wote mketi wabaki wale wanaoomba kuchangia. Namba moja, namba mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane. Haya mmetosha. Naandika hapa namba zenu, haya tunaanza na namba moja, si ndiyo nimeanzia huku? Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mimi nitaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kamani kwa ufupi sana, kwamba tumesikiliza hoja ya Mheshimiwa Mbunge na pia hoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Kama wanaweka vigezo vya umri, wanashindwa ku-*consider* vijana umri ambao wanamaliza *Form Six* na kwenda kwenye vyuo mbalimbali na kupata *qualificatio*n kwa vigezo kwamba anaweza akashindwa kuruka vihunzi, kwanza siyo sahihi na siyo kweli kwamba ukiwa na miaka 30, 40 huwezi kuruka vihunzi.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wana miaka 25 hawawezi kuruka. Mazoezi wanayoshindwa watu ambao wana umri mkubwa, tunatofautiana *background*. Wapo watu wengine ni watu wa mazoezi. Kwa hiyo, wao wangetoa *free,* watu wa-*apply,* kama ni kwenda kwenye mazoezi mtu ashindwe *field*. Akishindwa *field* atarudishwa *site* na hawezi ku-*complain,* lakini kwa sasa ilivyokaa ni kwamba unaweka *limit,* mtu anaweza kuomba ile kazi na hana ajira

nyingine, yuko mtaani lakini umeweka umri, lakini anaweza aka-*qualify*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hii habari ya umri tuiangalie, iondolewe. Kama kuna mtu ataenda *site* kule akashindwa *field,* hawezi kulalamika, lakini kwa sasa itaonekana kazi imetengenezwa kwa kundi fulani na kwa umri fulani na wengine hawatakiwi kupata ajira, na kwa kweli wataendelea kulaumu mtaani bila kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kamani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Hanje na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani kuhusiana na umri wa ajira zilizotangazwa na *TAWA*. Kimsingi hoja yake ni hoja ya msingi sana, ndiyo maana kama Wabunge ambao tunawakilisha kundi la vijana humu Bungeni lazima tuzungumze.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwenye jambo alilolisema kwamba tuongeze umri mpaka miaka 30. Nami nasema miaka 30 angalau ili sasa vigezo vile vya jumla, kwa sababu lazima wana utaratibu wao wa ku-*train* watu wao wanaowahitaji, basi waende wakashindwe *field* kama ikitokea kwamba mtu sasa ameshindikana.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili, kwa sababu tunajua watakaoomba ni wengi, nami niseme, kwa sababu ajira za Serikali ni chache sana kutokana na jinsi ambavyo tunalifahamu soko la ajira, yaani kwamba wanaokuja mtaani ambao wanahitaji ajira ni wengi sana. Kwa maana hiyo sasa kuendelea kupunguza wigo (kupunguza goli) maana yake tunaendelea pengine kutengeneza

malalamiko ambayo vijana wanaweza kulalamika kwamba tunategemea mkitangaza ajira ya Serikali, basi msitupunguzie goli ili tukapambane huko huko uwanjani ili tuone atakayefanikiwa aende.

Mheshimiwa Spika, jambo hili pia linahitaji *graduates* na kwamba kuna vijana wengi sana wako mtaani na utaratibu wetu wa mfumo wa elimu unatufanya wanafunzi wakae muda mwingi sana darasani kiasi kwamba anamaliza katika umri huo ambao anasema ndiyo mwisho wa wao kuomba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa nukta hiyo nami naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ili tubadilishe vigezo na tuongeze umri wa vijana kuomba nafasi hizi ambazo tunategemea haki itatendeka.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tuwaombe isiwe kuna nafasi ambazo zimeandaliwa na watu fulani, wawaache vijana wakapambane kwa sababu tayari ilishaleta mkanganyiko kama hivi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburus Saputu atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ninaanza kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ng'wasi kwamba suala la umri ni suala ambalo hata kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri kwamba ni Jeshi Usu, mimi nadhani pia hawa wataalamu wetu wanaoandaa hivi vigezo wakati mwingine watafakari na kuangalia hali ya Watanzania na vijana tulionao huko mtaani na kiwango cha ajira kinachotolewa; na hiki kigezo cha miaka 25 kurudi 18 mimi nadhani bado hakiko sawa na hakitakuwa sawa. Hakitakuwa sawa kwa sababu Jeshi la Wananchi wa Tanzania na hilo Jeshi Usu mafunzo ni tofauti, hayawezi kuwa makali kuzidi Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nadhani suala hili la umri angalau kutoka miaka 18 mpaka 30 kwa majeshi haya Usu siyo sehemu mbaya. Sasa suala la afya lijulikane wakati wa mafunzo hayo na kupimwa kwao na kuangaliwa kwao. Kuweka miaka 25 ni kuwazuia vijana walio wengi kupata ajira na hasa ukizingatia ajira zenyewe ni chache.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba wakati mwingine Serikali ijitambue na tujitambue sisi sote kwamba umri wa kuajiriwa kwa Mtanzania kuingia kwenye mfumo wa Serikali ni miaka mingapi? Sasa lazima Serikali kila mara inapotoa tangazo lake ijiridhishe kwamba ina Watanzania wangapi ambao kwa sasa umri unapita bila kuajiriwa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na kwa kweli naomba tu Bunge hili na kwa busara zako tukahitimishe kwamba na ajira nyingine zote ziangaliwe kuanzia miaka 18 mpaka 30 ni umri sawa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Sekiboko na Mheshimiwa Felista Njau ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kamani, kwa sababu mwisho wa siku muda wa masomo kwanza mtu mpaka asome afanye *certificate, diploma* na *degree* tayari umri unakuwa umeshasogea. Kwa hiyo, tunaposema miaka 18 mpaka 25 tutawaacha watu wengi nje.

Mheshimiwa Spika, pia tusisahau ni muda mrefu sana ajira zilikuwa hazitoki. Tunashukuru angalau kwa miaka hii mitatu au minne tumeanza kupata ajira. Sasa basi kama ni hivyo, tunaomba sana tufahamu kwamba Jeshi Usu linahitaji tu ukakamavu. Kwa hiyo, ukakamavu kwenye udereva unawezakana hata kama anakimbiza labda majangili au vitu kama hivyo, miaka 25, 26 au 30 ana uwezo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Kamani kwamba angalau tusogeze miaka 30 na isiishie tu kwenye mambo ya *TANAPA* na hao wengine, tufanye na kwenye ajira nyingine. Vinginevyo watoto wengi ambao ajira zilisimama miaka sita au saba iliyopita, tutakuwa tumewaacha kwenye mfumo, wataendelea kuwa wakulima wakati wamesoma. Serikali imetumia gharama kubwa kuwasaidia na pia wanahitaji kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naungana na hoja ya kuongeza umri kwenye ajira zote. Namuunga mkono Mheshimiwa Ng'wasi Kamani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko atafuatiwa na Mheshimiwa Felista njau na Mheshimiwa Miraji Mtaturu ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mbunge makini wa kundi la vijana, mdogo wangu Mheshimiwa Ng'wasi Kamani. Kwanza, naiunga mkono hoja hii kwa sababu mbili au tatu. Kwanza, kwa mujibu wa Sheria ya Ajira *(Permanent Employment)* inataka kuanzia miaka isiyozidi 45 na siyo 25. Kwa hiyo, tukiangalia kwa mujibu wa sheria yetu tunajichanganya.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa mujibu wa taratibu za ajira za kijeshi tumeona maeneo mengi walikuwa wanatafuta vijana ambao wana uzoefu wa ziada kwenye maeneo fulani fulani, wengine wawe wamepitia kwenye majeshi ya mgambo na kadhalika. Sasa kwa mwanafunzi ambaye amehitimu katika mfumo wa moja kwa moja, siyo rahisi kupata hivyo vigezo ambavyo mara nyingi wanapotoa ajira za kijeshi huwa wanavitaka, lakini mwisho wa siku ni ukweli usiopingika kwamba tuna vijana wengi sana wako mtaani wanatafuta ajira.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, wanapokuwa wanatangaza tena ajira chache namna hii ni vizuri wakapunguza vigezo ambavyo havina ulazima kwa sababu wanakuwa na

michakato ya ndani ya kuweza kuwapima na kutafuta wale ambao wanawahitaji. Wakitoa matangazo yenye ubaguzi wanaichonganisha Serikali na wananchi wake na wanatuchonganisha sisi ambao tunawawakilisha na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja kwamba kigezo cha miaka 25 kipelekwe angalau miaka 30 au 35 ili tuwape nafasi vijana wengi zaidi kuingia kwenye soko hilo la kupigania ajira ambazo zimetangazwa. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Felista Njau, atafuatiwa na Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naunga mkono hoja kwamba vijana wa Kitanzania, hiki ni kigingi kingine cha kuwakosesha fursa. Nilifikiri katika vigezo vinavyotolewa, hivi vya umri tumekaa muda mrefu vijana wetu wako *bench* hawajapata ajira. Kijana ana-*graduate* anakaa hata miaka mitatu au minne yuko nje anatafuta ajira na ni kijana wa Kitanzania. Tuwape fursa vijana wetu waweze kuajiriwa kama nafasi hizi zikitoka.

Mheshimiwa Spika, nilifikiri kutakuwepo na kigezo cha *NIT* ambacho *at least* kama wale madereva wanajua maadili hata ya kuendesha viongozi na kupunguza ajali barabarani, lakini kigezo hiki cha umri hakiwezi kuja kumfanya kijana wa Kitanzania kukosa nafasi ya ajira, eti kwamba ya udereva Jeshi Usu wana mafunzo yao; watakwenda kuwafundisha, kijana ashindwe akiwa *field,* ndivyo ilivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, hata kigezo kilivyokuja, wale waajiriwa awe tena na kigezo cha JKT ilionekana kabisa kuwa kuna namna ambavyo vijana wa Kitanzania walikuwa wanakosa fursa na hii ni mbinu pia ya kijana wa Kitanzania kumkosesha fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kijana huyo anayeomba hii ajira awe na kigezo cha umri wa miaka 25 mpaka 30 aende akashindwe kule *field* ndiyo tujue kwamba kashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hayo, naomba wakati ajira zimesha-*stack* muda mrefu kwa vijana wetu, hivi vitu vya konakona vitolewe ili vijana wetu wawe na macho waone Serikali inawaona na inawapigania na nafasi zikija ziwe sawa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu na Mheshimiwa Olelekaita, kuna mmoja alikuwa amesimama nimemsahau, naelekea kwa Simbachawene. Sio wewe Mheshimiwa aliyekuwa amesimama wakati huo! Huku nilishahesabu watatu. Pole nilikuwa sijakuona. Kuna Mbunge mwingine alikuwa amesimama? Aah, ulikuwa kule umehamia huko? *(Kicheko)*

Sasa mmesimama wengi, nashindwa kujua nani anayesema ukweli. Wote mlisimama, sawa, lakini nilitaja watu nane, na wa nane alikuwa ni yule pale. Aliyeongezeka ni Mheshimiwa Olelekaita tu, wale niliowahesabu nane mmoja amesahaulika. Haya basi, huyo wa nane wote mkatwe kwa sababu mmesimama wawili kwa wakati mmoja. Mheshimiwa Miraji Mtaturu atafuatiwa na Mheshimiwa Olelekaita, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii atamalizia na mtoa hoja utajiandaa.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani. Kwanza, nampongeza sana kwa kuliwakilisha kundi la vijana vizuri katika hoja hii ambayo ni ya ajira.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua mfumo wetu wa elimu unachukua muda mrefu mpaka vijana wana-*graduate*. Hapa tunaangalia miaka 23 mpaka 25 wanakuwa ndio wanamaliza *degree*. Maana yake ni kwamba vijana wetu wanatumia muda mrefu wakiwa shuleni. Pili, ni kwamba kwa takribani muda wa miaka saba hatukutangaza ajira. Kwa hiyo, kuna vijana wengi wako

mtaani ambao hawana kazi na kwa hakika pamoja na kwamba wanasema sekta binafsi, lakini msingi wa ajira zinatoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba watu wote wanaitegemea Serikali iwape ajira na ndiyo maana hata sasa ikitangazwa watu wengi wanaenda kuomba Serikalini. Kwa hiyo, hoja yangu hapa ni kwamba kwenye suala la muda, hiyo *burden* wabebe pia na Serikali. Kama hawakutangaza ajira muda mrefu zaidi ya miaka saba, sasa tumetangaza vigezo vingine vya umri kama hivi, tuweze ku-*accommodate* vijana wote waweze kuingia katika hiyo hali ili tusaidie kuondoa kundi kubwa la vijana ambao wako mtaani.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ya miaka 25 nami naunga mkono iende angalau miaka 30. Naamini kabisa miaka 30 bado ni kijana anaweza kupewa mafunzo ya aina yoyote *unless* awe *unfit,* lakini kiukweli bado miaka 30 mpaka 34 na 35 bado ni kijana anaweza kupata mafunzo yoyote. Kwa hiyo, tusiwatoe vijana hawa kwa sababu miaka imezidi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali isikie kwenye hili, iongeze umri ili iweze kubeba vijana wengi ambao wako mtaani. Kwa hakika wako tayari kulitumikia Taifa na kusiwe na kigezo ambacho kimeelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja iliyotolewa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Olelekaita atafuatiwa na Mheshimiwa Latifa Juwakali na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Tumpongeze mtoa hoja, nakubaliana tuongeze miaka iwe 30 lakini kwa sababu umetoa nafasi tuwashauri, ushauri mwingine haya matangazo yanayotolewa kwa Kiingereza tunamfaidisha nani? Kwa

nini wasitoe hili tangazo kwa Kiswahili? Kwa hiyo, kama kuna eneo lingine la kurekebisha, wakarekebishe matangazo haya yawe kwa Kiswahili. Sasa unataka dereva, halafu leo unataka aongee Kiingereza, halafu ni dereva wa wanyamapori, anaenda kuzungumza hicho Kiingereza na nani? Hilo ni moja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia kitu kingine hapa. Hili tangazo la wiki mbili pekee, ni vizuri kwa sababu wamesema ni *online,* kwamba wana-*propose online* tuweke kwenye *portal,* lakini mara kadhaa imekuja shughuli, mitandao yetu inakuwa na shida na tume-*extend* matangazo mengi hapa kwa sababu ya muda mfupi unaotolewa. Kwa hiyo, ushauri mwingine waongeze iwe mwezi mzima.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naangalia kwenye tangazo hapa anaambiwa, *"A signed application letter should be either in Swahili or English."* Sasa kama kuna hizi *option,* tangazo liwe kwa Kiswahili. Kilichonishtua zaidi pale kwa dereva, sifa za dereva anaambiwa awe na *one year experience without causing accident.* Sasa hiyo imekaaje? Yaani kweli sisi sote ni madereva na tuko barabarani, *not every accident* inakuwa *caused* kwa sababu ya *maintenance* ya gari *and after all* utapataje hiyo data?

Mheshimiwa Spika, yaani leo dereva ni mwananchi kutoka Kiteto halafu eti unamwambia *one year experience* halafu *without causing accident.* Hii imekaaje? Ingekuwa kila mtu anaye-*cause accident* anakuwa nje ya barabara, matangazo kama haya ambayo ni *unreasonable* kati ya maeneo ambayo yanatakiwa yaondolewe, ni sehemu hiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Latifa Juwakali atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja au ajenda hii inayowahusu vijana moja kwa moja. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Ng'wasi Kamani kwa kuona namna gani ajenda hii inavyotugusa tukiwa kama Wabunge wa kundi la vijana.

Mheshimiwa Spika, wenzangu waliotangulia hapa wameongelea zaidi kwenye hili Jeshi Usu. Binafsi nimeshaona matangazo mengi ambayo yanasema kigezo namba mbili au tatu cha mwombaji wa ajira ni umri. Umri wanatangaza kuanzia *degree* wanasema kwamba isizidi miaka 24 mpaka 25, lakini tukishuka ngazi nyingine, kuanzia *diploma* wanasema isizidi miaka 20 labda mpaka 23.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba tatizo la ajira ni kubwa kwa nchi yetu na kwa sababu asilimia isiyozidi 60 vijana wa nchi hii wanasumbuliwa na tatizo hili la ajira. Kwa nini tusiangalie vigezo vingine ikawa hiki kigezo cha umri siyo kigezo cha msingi zaidi au ikiwezekana basi tuishauri Serikali tuongeze umri sasa kutoka miaka 25 kwenye *degree* tupeleke mpaka miaka 30; kwenye ngazi ya *diploma* tutoke hapa ambapo tuliweka miaka 20 mpaka miaka 22, iwe miaka 25; na kwenye *degree* tutoke kwenye miaka 25 mpaka ngazi ya miaka 30?

Mheshimiwa Spika, kwenye ngazi hii ya elimu watu wanatofautiana. Tukiangalia kuna wanafunzi ambao wanatoka moja kwa moja kuanzia darasa la kwanza mpaka kwenda kwenye ngazi ya *degree,* hao tunaweza tuka-*assume* kwamba wanaweza waka-*cover* katika miaka 25. Kuna wanafunzi wengine bahati mbaya sana wanafika *Form Six,* lakini wakifika *Form Six* hawafanikiwi. Je, wakiwa hawajafanikiwa, hawa wanafunzi wanakuwa wamemaliza kusoma? Hawajamaliza. Wengine wanarudi kuanza kwenye ngazi ya *diploma*. Kwa hiyo, wakianza kwenye ngazi ya *diploma* kule ikafika miaka 25 na hii miaka mitatu ya *diploma* je, mwanafunzi huyu tutamwona katika namna gani?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja miaka iongezwe ifike miaka 30. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene na mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Tunasikia kauli za Waheshimiwa Wabunge kwenye eneo hili, lakini ninachotaka kusema tu ni kwamba vigezo hivi vimewekwa baada ya kazi kubwa sana kufanywa na vyombo vyetu vya ulinzi. Lilikuwa ni zoezi shirikishi ambalo lilihusika katika kuandaa mitaala yetu ya kuwaandaa askari wetu wa Jeshi hili la Uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, matokeo ya ushirikishwaji ule wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ndiyo yalituletea vigezo hivi. Nimesikia mfano umetolewa kwa dereva, ndani ya majeshi yetu ya uhifadhi dereva kiuhalisia siyo dereva wa kawaida. Madereva wetu kwenye eneo la uhifadhi wanafanya kazi katika mazingira ya kiupekee sana. Unaweza kumkuta dereva wetu huko kwenye mapori akalazimika kuendesha gari kwenye sehemu hata haina barabara. Kwa hiyo, yale mafunzo ya utimamu anayopata ndiyo yanayotupeleka huko kwenye vigezo vya umri. Vilevile katika kukabiliana labda na majangili huko, inatupeleka kwenye vigezo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wataalamu wetu kwenye vyombo vya ulinzi waliona umuhimu wa kuwa na kada ya askari ambao watakuwa na muda mrefu wa kuendelea kupata mafunzo wakiwa ndani ya jeshi, umri ambao utawawezesha wao kuweza kushiriki mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa tumeyasikia mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na sisi tunayachukua, tutarudi kwenye vyombo vyetu vya usalama tuyajadili tuone jinsi ambavyo tunaweza kuya-

*accommodate*. Vilevile, tutakaa na wenzetu wenye *instrument* hii inayohusiana na mambo ya ajira, na Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana wakati anatoa maelezo haya, lakini kwa sababu ni ushauri, tunaupokea tunaenda kuufanyia kazi na Mheshimiwa Waziri atahitimisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Chuo cha Mweka kiko chini yenu au kiko chini ya Wizara gani?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kiko chini yetu.

**SPIKA:** Chini yenu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Wastani wa mtu anayehitimu hapo Mweka, asome kitu chochote tu, wastani wa umri wa anayehitimu Mweka ni umri gani?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kati ya miaka 21 au 22.

**SPIKA:** Haya, watu ambao wanaenda kusoma hapo Mweka ni wale waliomaliza *form four* au wanafika *form six?* Yaani Mweka huwa mnachukua watu wa *form six* au mnachukua tu wa *form four?*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, wapo wa *form six* na wapo pia wa *form four.*

**SPIKA:** *Form six* kumbe siku hizi wanamaliza mapema sana. Yaani kuhitimu na miaka 21. Haya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora na mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Natambua na kuheshimu sana michango ya Waheshimiwa Wabunge, lakini nataka tu niweke vizuri kwamba imeonekana kama vile tumeweka sharti ambalo linawaondoa vijana. Hatujawaondoa vijana kwa sababu hata hao wanaopewa hii fursa ni vijana. Maana tumesema *limit* isizidi miaka 25, siyo maana yake kwamba hii *limit* ambao hawajazidi 25 ni wazee, hapana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kamani ana hoja yake ya miaka mingi, hataki ile *experience* ya miaka mingi kwa sababu ilikuwa inawa-*exclude* vijana kwenye haki ya kupata ajira. Sasa hiki ni kitu tofauti. Hii ni kwamba hawa wanaopewa hizi ajira ni *below 25.* Kwa hiyo, hawa ni vijana, ni kundi la vijana hao hao, tena hapa sana sana hii hoja inawatetea wazee kwa sababu ukisema *above 30* kwenda juu ni wazee.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hawa ambao Serikali tunasema *position* yake ni vijana, tena hawa tunawachukua vijana kwa sababu vyombo hivi vina asili yake. Ninukuu maneno ya *General* Mwamunyange aliwahi kusema kwamba, "Ni ngumu sana raia kujua nini kinatokea kwenye jeshi." *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa unajua mwanzo nilikuuliza tofauti. Hebu tuondoe kwenye hiyo dhana, kwa sababu ukitaka kuifanya *TAWA,* kwamba na yenyewe ni Jeshi la Wananchi, duh! Sasa jamani hawa watu mbona itakuwa shughuli hapa nchini sasa, kwa sababu kila mtu ni mwanajeshi.

Yaani hili neno 'jeshi' nalo itabidi tuje tulitazame vizuri kisheria maana kuna mambo tulifanya marekebisho hapa Bungeni wenyewe. Maana kila mtu kama ni wa jeshi la ulinzi labda kama *TAWA* na wenyewe wanaitwa jeshi la akiba, lakini kama ni la wanyamapori na wenyewe tukawapa hadhi kama ya Jeshi la Wananchi, mbona itakuwa kazi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninachotamani kieleweke ni kwamba, hawa wanaopewa hizi ajira ni vijana. Nataka tu hicho kieleweke. Siyo kwamba, ni wazee, ni vijana na ndiyo kusema *limit* ya umri isizidi miaka 25. Sharti hili limekuwepo katika Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji kumekuwa na sharti hili hili la umri. Kwa nini umri?

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu, vyombo hivi na majeshi haya wakati mwingine hata kustaafu hawatumii Sheria yetu ya Utumishi ya miaka 60. Kwa mfano Polisi...

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene, lugha ya mazungumzo yako mimi nakuelewa kabisa, lakini nakuomba sana tafadhali, watenganishe *TAWA* na haya majeshi unayoyataja. Mbona ni kama vile *TAWA* na wenyewe wako kwenye orodha ya vyombo vya ulinzi na usalama? Mbona naanza kupata wasiwasi kama ndiyo picha tuliyoijenga?

Yaani wewe hoja yako ya msingi mimi nimeielewa kabisa, kwamba hata hawa ni vijana, lakini ukisema tena kwenye majeshi yetu, na hawa nao wamo kwenye ile orodha? Yaani *TAWA* wanalingana na Jeshi la Zimamoto, Jeshi la Magereza na Jeshi la Wananchi? Wanalingana? Mimi sijui, nielimishe. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, wanapolingana ni pale kwenye eneo la uhitaji wa ukakamavu kwa sababu ndiyo tunaingiza *training* ya jeshi hata kama hatusemi ni jeshi na ndiyo maana kwa Kiingereza labda inaeleweka, ni *paramilitary*. Kwa hiyo, ni ujeshi ndani ya mtu ambaye siyo mwanajeshi ili a-*behave* na afanye majukumu yanayofanana na ya kijeshi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hawa kwenye Kiingereza wanaitwa *Conservation Ranger*. *Conservation Ranger* ni kazi ya *field* kwa hiyo, aina ya unayemhitaji pia inaweza ikatakiwa. Hata kuna

ajira nyingine ambazo zimeshatangazwa tukahitaji wenye umri mkubwa kwa sababu ya *speciality* au fani walizonazo. Kwa mfano, huwezi kumhitaji mtu ambaye ni mbobezi katika fani, hata hii ya uhifadhi ambaye atakuwa na umri mdogo wa miaka 25, hapana.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa wengi hapa, tunao watoto. Watoto wetu wanaomaliza *degree,* kama ameenda moja kwa moja kwa mfumo wa elimu ya Tanzania, akifika miaka 24 tayari ni *graduate* ana *degree*. Kwa hiyo, siyo kwamba, imewa-*exclude* sana kwamba, hapa ni jambo kubwa la kiasi hicho. Hata hivyo, mimi nimebeba tu kutetea hoja ya Serikali, lakini mambo haya yana michakato yake ambayo inatoka mbali sana. Kwa haraka haraka hapa tutasema sasa tunaridhia au vipi. Nipo tayari kusikiliza Bunge linasema nini na baadaye Serikali tutasema kwamba *position* hii ikoje au tufanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, isije ikaonekana kwamba, Simbachawene ni mbishi, anabisha tu, aah ah. Hii ni hoja ya Serikali, kwa hiyo, wazee wangu nawaheshimu sana Waheshimiwa Wabunge, lakini nataka niseme kabisa kwamba, hatukufika hapa hivi hivi, ni kwa sababu ya vigezo na Serikali ina utaratibu wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, hitimisha hoja yako.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwanza nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuniunga mkono katika hoja hii ambayo ina maslahi mapana sana na makubwa kwa vijana na Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wastani wa vyuo vyetu nchi nzima vinatema vijana au wahitimu kuanzia 100,000 mpaka 300,000 kwa mwaka. Wote tunajua kwamba, vijana hawa hawawezi kumezwa wote kuingia katika ajira Serikalini. Wote tunajua kwamba ni ukweli

usiopingika tumekuwa na muda mrefu kidogo ajira za Serikalini zimekuwa hazitangazwi na kutolewa. Tumshukuru tu Mheshimiwa Rais kwamba tangu ameingia madarakani amejitahidi kutoa ajira nyingi kuwameza vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *principle* moja inaitwa *Legitimate Expectations* au Matarajio Halali. Vijana hawa wanaotoka katika vyuo vyetu, ambao Serikali yetu imetumia fedha nyingi sana kuwasomesha wanatoka wakiwa na matarajio halali kwamba Serikali itawapokea, kuwa-*groom* na kuwaingiza katika *system* zake ili nao waendelee kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu hatuna hifadhi za watu binafsi, hifadhi zote ni za Serikali. Maana yake ni kwamba, kila aliyeenda kusoma kozi hii ajira yake pekee ni Serikalini. Leo hii tunatoa mwanya wa mwaka mmoja, maana yake tunawaambia wahitimu wote waliohitimu katika kozi hizi kwamba, asipopata kazi ndani ya mwaka mmoja wa kuhitimu kwake asahau, aende akatafute kazi nyingine. Hiyo siyo haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri. Mtu akisoma vizuri, *straight*, ameanza mwanzo mpaka mwisho bila kuweka *gap,* ndiyo atamaliza na umri wa miaka 24, lakini wote tunayafahamu mazingira yetu, uhalisia wetu tunaufahamu. Mtu kwa sababu zozote anaweza akapata *gap* ya mwaka mmoja au miwili hajaenda chuo *whether* anatafuta ada au mazingira yoyote yale. Maana yake huyu mtu atamaliza kusoma akiwa haajiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini hii siyo haki kwa vijana wetu bado. Kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tunao mwanya wa kuongeza umri ili kuweka muda ambao mtu kwa umri wake na *fitness* yake anaweza kufundishika kwa mafunzo haya na akafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, tumesoma pia *description* ya kazi anazokwenda kufanya mtu. Tumeona kwenye udereva, sawa

udereva kinachohitajika mtu haendi kubeba magogo, udereva ni kuendesha gari tu. Hata kama anakwenda kuendesha katika sehemu isiyo na barabara, kuendesha ni kuendesha na haya mafunzo ambayo wamesema wakishawachukua hawa watu wanakwenda kuwapa, yanatosha kabisa kum-*equip* huyu mtu kwenda kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwanza namshukuru Mbunge kwamba yeye mwenyewe hajaja na maazimio. Kwa hiyo, ametusaidia, lakini nia ilikuwa ni kwamba, Serikali isikie Waheshimiwa Wabunge mnasemaje kuhusu jambo hili ili waone kama kuna mahali ambapo wanaweza kufanya maboresho zaidi. *(Makofi)*

Sote nadhani tunakubaliana, huko nyuma hoja hii ilipokuja hapa Bungeni kwa mara ya kwanza, tulipoizungumza Serikali iliichukua na ndiyo maana kwenye vigezo hivyo, sasa hivi kile kigezo cha kupita Jeshi la Kujenga Taifa hakipo. Maana yake ni nini? Ni kwamba, tangazo hili linawachukua watu ambao siyo tu wataenda kwenye ajira huko *TAWA*, lakini watatakiwa sasa waende kwenye mafunzo ambayo huko nyuma wangekuwa wameshapitia JKT.

Kwa hiyo, hili la umri kama alivyolileta Mheshimiwa Mbunge na kwa ufafanuzi alioutoa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ni kwamba, kwa kuwa, tulishaondoa kile kigezo cha JKT maana yake ni wale watu wanaoenda huko kujifunza ni lazima wawe katika ule umri ambao wanaweza kumudu yale mafunzo watakayokuwa wanapewa, ambayo huko awali wangekuwa wamepewa JKT, hilo ni la kwanza.

La pili ni kwamba, kwa sababu waajiriwa wengi, siyo wote, watakuwa wanatoka kwenye kile Chuo cha Maliasili cha Mweka, sasa kule wanapewa mafunzo ya aina gani? Haya mengine yangeweza kutangulia kule ili hata kama mtu atakuwa na umri

uliosogea mafunzo haya awe alishayapata kule Mweka ili anapoomba kazi *TAWA* hata kama ana miaka 26 au 27 awe ameshayapitia kule mafunzo haya mengine anayohitaji akiwa mdogo. Kwa nini?

Kwa sababu, mzazi anapoenda kumlipia huyu mtoto ada kule ana imani kwamba atapata ajira kwenye hii sekta. Sasa hii sekta ikishamuondoa na miaka 26 ndiyo basi tena. Sasa kwa hiyo, hayo yote ndiyo maana nilisema tutoe hoja hii Serikali isikie Waheshimiwa Wabunge wanasema nini na mchukue yale ambayo yanaweza kurekebishwa yarekebishwe. *(Makofi)*

Kwa mfano, haya ya dereva, kwa kweli, Dereva wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania hawezi kulingana na Dereva wa *TAWA*. Tukitaka kuwaweka wote hawa wawe na vigezo sawa, basi tuwapeleke wote wakafundishwe na Jeshi la Wananchi wa Tanzania halafu watawanywe kwenye haya majeshi, maana vigezo vinafanana. Maadam wanajifunza huo utofauti, basi na sisi katika kuwachukua hao vijana tuwachukue kwa utofauti kwa sababu, wale wengine wana vipimo vingine ambavyo pengine haya majeshi mengine, hata kama yanatumia neno 'jeshi,' hayavihitaji hivyo, lakini kwa upande wa Jeshi la Wananchi pengine wanavihitaji. Kwa hiyo, na sisi tujaribu kuona hizo tofauti ili tusiwaondoe kwenye huu mfumo wa ajira vijana wengi. *(Makofi)*

Pia hoja nyingine ambayo ni ya msingi kabisa ni kwamba, hata hawa wa chini ya miaka 25 nao ni vijana, lakini hoja ni kwamba, uhitaji wa ajira wote wanahitaji. Hawa wa chini ya miaka 25 ni vijana na wa juu ya miaka 25 pia ni vijana. Uhitaji wa ajira wa huyu aliyemaliza masomo yake baada ya miaka 25 ni mkubwa zaidi kuliko wa huyu ambaye bado ni kijana, anaweza kuwa ndiyo anatafuta elimu, anajitafuta na yeye. Huyu mwingine umri unazidi kusogea kwa haraka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, haya yote Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, kama ulivyosema, ni mambo ambayo

baadhi yanazungumzika. Wale wa *ranger* wanaoshika bunduki ni habari nyingine, lakini hawa wengine jitahidini kuweka mazingira, maana umri wa kijana hata huko Umoja wa Mataifa ni miaka 29, ndiyo kijana. Ukija huku kwingine kwenye siasa kila watu wanaangalia namna, miaka 40. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tujaribu kuona aina za mafunzo ambazo mtu wa zaidi ya miaka 25 anaziweza, basi tuweke hayo mazingira. Yale ambayo hayawezekani, tuweke hivyo kwamba hayawezekani, lakini kigezo kikiwa kinafanana kwa dereva, yule wa *conservation* sijui kitu gani ameitwa, nadhani kunaweza kuwa na mambo tofauti hapo na tukawa tumefikia lengo lile ambalo alikuwa analizunguza Mheshimiwa Mbunge hapa na hoja za Waheshimiwa Wabunge zimezungumzwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunashukuru kwamba, kile kigezo cha JKT kiliondoka, lakini pamoja na kwamba kwa sasa wataenda wapate huko mafunzo moja kwa moja, kwa hiyo, hoja ya umri ni ya muhimu. Ila mtazame yale ambayo umri hautakuwa na ulazima sana kwa aina ya mafunzo au aina ya kazi ambayo mtu atakuwa anahitaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, hoja yako imesikika na uzuri ni kuwa, hukuwa umeleta azimio. Kwa hiyo, hakuna cha kukitoa kwa Bunge. Hoja yako imesikika na Serikali wataifanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024** ***(The Prevention and Combating of Corruption (Amendments) Bill, 2024)***

**na**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024** ***(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kutujalia afya na uhai na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge la Kumi na Mbili. Kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa 2024, yaani *The Prevention and Combating of Corruption Amendment Act 2024*.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu na kwa kuona ni vyema nimsaidie yeye na Serikali yetu katika nafasi hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Napenda kumwahidi Mheshimiwa Rais ya kwamba, nitaendelea na majukumu aliyonipatia kwa nguvu zangu zote, moyo wangu wote na kwa akili zangu zote kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia, natumia nafasi hii kuwashukuru sana viongozi wetu wakuu. Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa na Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwa kutusimamia na kwa maelekezo kwa ofisi yetu ambayo ndiyo yamekuwa dira na mwelekeo wetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nachukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wenzangu mbalimbali walioteuliwa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni bila kuwataja majina, wanajulikana. Nawapongeza sana kwa imani ambayo Rais anayo kwao, waje tushirikiane tuweze kuchapa kazi. Kwa namna ya pekee nampongeza sana Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Deus Sangu ambaye kwa kweli, tangu ameingia ofisini *replacement* niliyopata baada ya kuondoka Mheshimiwa Ridhiwani, ambaye naye nampongeza kwa kupata Uwaziri, lakini *replacement* hii nadhani ni kama kaondoka Mayele kaingia yule mwenzie anayefunga magoli sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nimpongeze Mheshimiwa Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa imani aliyoipata kutoka kwa Rais. Tuna imani kwamba, ofisi yetu inapata msaada mkubwa kwake na tunamshukuru sana hata kwa hatua ya kazi hii ambayo ninaisoma hapa mbele yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukushukuru wewe pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote kutokana na majukumu mnayotekeleza katika Bunge hili, hakika nchi yetu inapata

mwelekeo mzuri kwa sababu ya mchango wa Bunge lako. Tunakushukuru sana na kukupongeza ikiwa ni pamoja na kuaminiwa kuwa, Rais wa Mabunge yote ya Dunia, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi katika Kamati yetu, tuna Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Mhagama akisaidiwa na Mheshimiwa Kyombo. Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati wanatulea vizuri, wanatuelekeza vizuri, hakika tunaishi katika maisha ya raha kwa sababu tunafanya kazi kama marafiki bila ku-*compromise* ufanisi, kwa ajili ya kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichukue nafasi hii kabla ya kuwasilisha maelezo ya kina kuhusiana na Muswada huu, niwasilishe maelezo ya utangulizi kwamba rushwa ni tatizo lenye madhara mabaya sana kwa jamii. Rushwa inaua demokrasia, inadumaza utawala wa sheria na kusababisha ukiukwaji wa haki za binadamu. Rushwa ni chanzo kimojawapo cha uharibifu wa rasilimali za umma, inaathiri utoaji huduma kwa umma na kuchangia kukua kwa vitendo vya uhalifu na vitendo vingine vinavyoathiri usalama.

Mheshimiwa Spika, tangu nchi yetu ipate uhuru Mwaka 1961, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuzuia na kupambana na rushwa. Hatua hizo ni pamoja na kusimamia maadili na kuweka sharti la uwajibikaji katika utumishi wa umma, kuweka mazingira wezeshi ya uwazi katika utendaji wa kampuni na mawakala wa sekta binafsi, sanjari na kuweka mazingira sawa ya kiushindani, kibiashara na kudhibiti rushwa katika ununuzi wa umma na kuimarisha ukusanyaji mapato.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa habari, kushirikisha wadau katika kuzuia na kupambana na rushwa, kutunga sheria madhubuti ya kuzuia rushwa na kuanzishwa taasisi ya usimamizi na utekelezaji wa sheria hiyo pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Serikali ilitunga Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329. Lengo la kutungwa kwa sheria hii ni kuimarisha utawala bora na kutokomeza rushwa Tanzania Bara. Sheria hii, pamoja na masuala mengine, ilianzisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, yaani TAKUKURU, taasisi ambayo ilipewa wajibu wa kuchukua hatua za kuzuia na kupambana na rushwa katika taasisi za umma na sekta binafsi Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, miaka 17 imepita tangu kutungwa kwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329. Kutungwa kwa Sheria hii kumewezesha utekelezaji wa majukumu mbalimbali yenye kuelekea kutimiza malengo ya sheria hiyo, yaani kuimarisha utawala bora na kutokomeza rushwa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kuendana na mahitaji na mabadiliko mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya kiteknolojia, sheria hii imefanyiwa marekebisho madogo mara mbili, mwaka 2018 kupitia Sheria Na. 7 ya 2018 na Mwaka 2019 kupitia Sheria Na. 11 ya Mwaka 2019 na kufanyiwa urekebu mara moja Mwaka 2022. Pamoja na marekebisho mbalimbali na urekebu uliofanyika katika sheria hii, bado sheria hii inakabiliwa na upungufu ambao unapunguza ufanisi katika kufikia lengo la kutungwa kwake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kufanyiwa urekebu Mwaka 2022, bado yamebainika upungufu katika utekelezaji wa sheria hiyo ambapo baadhi ya upungufu huo ni pamoja na sheria kutoainisha makosa ya rushwa katika uchaguzi, michezo na burudani; kukosekana tafsiri kwa baadhi ya misamiati muhimu iliyotumika kwenye sheria; kutokuwepo kwa uwiano wa makosa na adhabu; ukinzano kati ya sheria hii na Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256; muda mfupi wa kushikilia mali za mtuhumiwa zinazodhaniwa kuwa ni mazalia ya uhalifu wakati wa uchaguzi hivyo, kukwamisha utaratibu wa utaifishaji; ufinyu wa tafsiri, *(narrow definition)* ya maana ya umiliki wa mali inayosababisha kuwe na changamoto wakati wa

kufanya uchunguzi wa tuhuma za limbikizo la mali zinazopatikana kwa njia isiyo halali.

Mheshimiwa Spika, sheria kutokuwatambua wadau wengine katika sekta binafsi kwenye mapambano dhidi ya rushwa, mbali na taasisi za kifedha pekee. Kifungu kinachoelekeza namna ya kufanya uthaminishaji wa mali zinazochunguzwa chini ya sheria, kina changamoto kwenye utekelezaji na sheria ya kutoa masharti yanayompa mamlaka Mkurugenzi Mkuu kuchunguza akaunti, lakini kutompa mamlaka ya kuweka zuio la muda la akaunti ya benki pale inapobainika fedha zilizo kwenye akaunti za mtuhumiwa zinazochunguzwa, kudhaniwa kwamba zimehusika na makosa ya rushwa au mtuhumiwa anajihusisha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 na vilevile inakusudia kuimarisha lengo kuu la sheria ambalo ni kuimarisha Utawala Bora na kutokomeza rushwa nchini. Ufafanuzi wa upungufu na mapendekezo ya marekebisho ya vifungu, unatolewa hapa chini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu cha tatu kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha baadhi ya tafsiri ya misamiati iliyotumika katika sheria na kuongeza fasili ya misamiati mipya inayotokana na masharti mapya yanayopendekezwa kuongezwa katika sheria.

Mheshimiwa Spika, kfungu cha sita kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha majukumu ya Naibu Mkurugenzi Mkuu. Lengo la marekebisho haya ni kufafanua majukumu ya Naibu Mkurugenzi Mkuu ili kurahisisha utendaji na uendeshaji wa Taasisi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha saba kinaipa TAKUKURU mamlaka ya kuzuia na kupambana na rushwa kwa kubainisha mianya ya rushwa katika taasisi za umma, mashirika ya umma na sekta binafsi, kuhamasisha umma kushiriki katika mapambano dhidi

ya rushwa, kushirikiana na wadau katika mapambano dhidi ya rushwa, kufanya uchunguzi wa tuhuma za rushwa na kwa kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka, kuendesha mashauri ya rushwa Mahakamani. Kifungu hiki kipo kimya kuhusu Mamlaka ya TAKUKURU kuchukua hatua kwa makosa ya rushwa yaliyotajwa kwenye sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha saba kinarekebishwa ili kuiwezesha TAKUKURU kutekeleza jukumu la kuzuia na kupambana na rushwa hata chini ya sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha na kuharakisha mchakato wa uchunguzi. Lengo la marekebisho haya ni kusaidia kugundua na kuzuia rushwa na makosa yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kudhibiti matumizi mabaya ya mamlaka ya upekuzi ya Afisa Uchunguzi wa TAKUKURU. Kwa sheria ilivyo sasa haijabainisha masharti kuwa ni kosa kwa mchunguzi kutumia vibaya mamlaka ya kupekua.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 15, 16, 17, 18 na 20 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa adhabu kwa makosa yanayohusiana na vitendo vya rushwa. Lengo la marekebisho hayo ni kuipa mamlaka Mahakama ama kutoa amri ya kulipisha fedha pale mshtakiwa anapokutwa na hatia na kubainika alipata manufaa kutokana na kutenda vitendo vya rushwa au kuamuru kutaifishwa kwa mazalia/mali yatokanayo au yaliyowezesha kutendwa vitendo vya rushwa. Kwa wahalifu kuwanyang'anya mapato yaliyotokana na uhalifu itahakikisha hawafaidiki kutokana na vitendo vyao vya kihalifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuongeza wigo huo nchi itakuwa inatekeleza wajibu wake kwenye makubaliano iliyoingia ya kimataifa ikiwemo makubaliano ya kupambana na rushwa ambayo

yanataka mbali ya kumwadhibu mshtakiwa aliyekutwa na hatia lakini pia mali alizozipata kutokana na vitendo vya rushwa zitaifishwe.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 25 kilivyo sasa kinatoa adhabu kwa mtu aliye kwenye nafasi ya madaraka anayedai rushwa ya ngono bila kumwajibisha anayemshawishi aliye kwenye nafasi ya madaraka kutenda kosa la rushwa ya ngono. Kifungu cha 25 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti zaidi ya kupambana na rushwa ya ngono. Marekebisho haya yanamlenga mtu anayeomba rushwa ya ngono kwa kutumia ushawishi wa mamlaka aliyonayo na mtu anayeshawishi au anayetoa ahadi au kutoa rushwa kwa mtu aliye na madaraka.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 27(1)(b) kinatumia neno "*owns*" ambalo kimsingi tafsiri yake haimbani mmiliki aliyeandikisha mali kwa jina la mtu mwingine kwa lengo la kuficha umiliki. Kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupanua wigo kwa kujumuisha mali ambazo zipo chini ya mtuhumiwa, lakini zinamilikiwa kwa jina la mtu mwingine. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia ukwepeshaji wa umiliki kwa kutumia umiliki mbadala na kuhakikisha uwajibikaji na utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 31 kimekuwa na utata katika kutoa tafsiri miongoni mwa watumiaji wa sheria. Utata umekuwa ni viini kama vilivyopaswa kuthibitishwa ili kosa liweze kuthibitika limetendwa. Baadhi ya wanamawazo, wamekuwa wakiamini ili kuthibitisha kosa hili la matumizi mabaya ya madaraka ni budi kuthibitisha viini hivi kwa pamoja, yaani kuvunja sheria na kutumia mamlaka yake vibaya wakati kuna wengine ambao wanaamini inatosha kuthibitisha moja ya viini hivyo viwili kulingana na mazingira ya kosa.

Mheshimiwa Spika, utata huu mara kadhaa umekuwa unachelewesha kufanya uamuzi wa kufungua mashtaka na pia umekuwa ukiipa Mahakama changamoto katika kufikia maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 35 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupanua wigo wa matumizi yake. Kilivyo sasa kimejifunga kwenye mikataba peke yake, kwa kufanyiwa marekebisho itahusu zaidi ya kupata mikataba Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 38A ni kipya kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuweka masharti yanayompa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kuzuia akaunti ya mtuhumiwa yenye fedha zinazochunguzwa baada ya kuifanyia upekuzi akaunti husika. Lengo la marekebisho haya zaidi ya kumpa mamlaka Mkurugenzi Mkuu kuzuia akaunti yenye fedha zinazohusishwa na vitendo vya rushwa ni kutekeleza wajibu wa nchi, kutekeleza makubaliano ya kimataifa iliyoingia na kuahidi kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, mfano nchi inawajibika chini ya Ibara ya 31(2) ya Makubaliano wa Umoja wa Mataifa dhidi ya rushwa na chini ya Ibara ya 16 ya Makubaliano ya Umoja wa Afrika ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ambayo yanazitaka nchi washirika kuweka utaratibu wa kisheria wa namna ya kuweka zuio la matumizi ya mapato yatokanayo na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 43(3) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, kinakinzana na kifungu cha 15(3) cha Sheria ya Mapato yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 kwenye eneo la nani atakuwa mmiliki wa mazalia ya uhalifu na vifaa vilivyowezesha uhalifu baada ya kutaifishwa kwa amri ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Mapato yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 kuhusu umiliki wa mali itokanayo na amri ya Mahakama ya kutaifisha mali iliyopatikana au iliyowezesha kutekeleza au vilivyowezesha kutekeleza kosa jinai ambapo ilibadilisha mmiliki kutoka Msajili wa Hazina na kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwenye marekebisho hayo Kifungu cha 43(3) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 hakikuguswa, hivyo Msajili wa Hazina akaendelea kutajwa kama ndiye atakayekuwa mmiliki wa mali zilizotaifishwa, kutoka hapo ikawa inakinzana na Sheria ya Mapato yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 ambayo inamtaja Katibu Mkuu Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kifungu cha 43(3) kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuweka ulinganifu wa masharti ya kifungu hicho na masharti ya Kifungu cha 15(3) cha Sheria ya Mapato yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256. Kwa kufanyika marekebisho hayo, kutaoanisha masharti ya vifungu hivyo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa katika maeneo ya uchaguzi, michezo na burudani. Kwa kutumia Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 ambacho kinahusu hongo. Kifungu hicho kina sharti mahususi linalopaswa kuthibishwa ili kuthibitisha kosa la hongo, sharti hilo ni kiini cha "*principal-agent relationship*" kati ya mtoaji na mpokeaji wa rushwa.

Mheshimiwa Spika, kiini hiki kimekuwa hakiwezi kuthibitika kwenye kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa katika maeneo ya uchaguzi, michezo na burudani kwa kuwa kwenye maeneo hayo ya uchaguzi, michezo na burudani hakuna uhusiano wa "*principal-agent*" unaokuwepo kati ya mtoa rushwa na mpokeaji. Kutokana na changamoto hiyo, Serikali imekuwa ikishindwa kesi za aina hiyo pale zinapofunguliwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa changamoto hiyo, sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza "Sehemu ya Tano A" mpya ambayo inaweka masharti ya makosa yanayohusiana na masuala ya rushwa katika uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani bila kuweka takwa la kiini cha *principal agent relationship*.

Mheshimiwa Spika, kwa maelekezo haya, itaiwezesha TAKUKURU kupambana na rushwa katika maeneo hayo ya uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani kwa ufanisi. Kwa kuweza kupambana na rushwa katika nyanja hizi kutahakikisha uadilifu na hivyo vinadumishwa katika mchakato wa uchaguzi, matukio ya michezo, shughuli za michezo ya kubahatisha na tasnia ya burudani.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 46 kinatoa masharti kwa TAKUKURU kushirikiana na sekta binafsi hususan taasisi za kifedha katika mapambano ya rushwa. Wigo huu wa wadau unatambuliwa na kifungu hiki ni mdogo ukilinganishwa na wadau waliopo. Kifungu cha 46 kinarekebishwa kwa lengo la kupanua wigo huo wa taasisi kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake kwa baadhi. Lengo la marekebisho haya ni kupanua wigo wa ushirikiano ili kujumuisha wadau wote muhimu kwa pamoja na sekta binafsi ili rushwa iweze kukomeshwa katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 49 na cha mwisho, kinahusiana na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329, kinatamka kuwa uthamini wa mali utatumia bei halisi ya vifaa vilivyotumika wakati wa ujenzi. Kifungu hiki kimekuwa na changamoto kwenye utekelezaji wake kwa sababu imekuwa ni vigumu kupata kumbukumbu za gharama hizo wakati wa uchunguzi, kwani kwa kawaida uchunguzi unapofanywa inakuwa ni miaka mingi imepita tangu majengo yalipojengwa. Kifungu cha 49 kinarekebishwa ili kuzingatia viwango vya kitaalamu vya namna ya kufanya tathmini kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, kurekebishwa kwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 kutaharakisha na kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wadau kwa kuongeza kasi ya kupambana na kuzuia vitendo vya rushwa, kuimarisha mchakato wa urejeshaji wa mali zinazopatikana kwa njia za rushwa, kuendeleza utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa na Kikanda ya mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption (Amendments) Act, 2024)* na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja.

**MAELEZO YA MHESHIMIWA GEORGE B. SIMBACHAWENE, WAZIRI OFISI YA RAIS-MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA, 2024 (THE PREVENTION AND COMBATING OF CORRUPTION (AMENDMENTS) ACT, 2024) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema; na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge la Kumi na Mbili, na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, 2024 (The Prevention and Combating of Corruption (Amendments) Act, 2024).

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu, na kwa kuona ni vyema nimsaidie yeye na Serikali yetu katika nafasi hii ya Waziri Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nipende kumwahidi Mheshimiwa Rais ya kwamba naendelea na majukumu

aliyonipatia kwa nguvu zangu zote, moyo wangu wote na kwa akili zangu zote kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Aidha, nipende kuwashukuru na kuwapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa shukrani kama nisipokushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako wa kipekee katika Bunge hili Tukufu. Aidha kwa namna ya pekee, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, (ndc.) na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Aidha, niwapongeze, Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na uratibu), Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jenista Joackim Mhagama (Mb) kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Afya, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb) kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Jerry William Silaa (Mb), kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Balozi Mahmoud Thabit Kombo (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Deogratius J. Ndejembi (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Waheshmiwa Manaibu Waziri wote walioaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Rais katika Wizara mbalimbali. Vilevile, kipekee naomba kumpongeza Mhe. Hamza Said Johari kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nipende kukuahidi kwamba mimi binafsi na Ofisi ya RaisMenejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tutaendelea kutoa ushirikiano wa hali juu kwa Bunge lako Tukufu katika eneo hili tunalolisimamia.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu Ikulu, Mheshimiwa Muruli Majura Mahendeka kwa ushirikiano wake katika kufanikisha maandakizi ya Muswada huu pia nawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya RaisMenejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiongozwa na Katibu Mkuu, Mheshimiwa Juma Selemani Mkomi kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mbunge wa Madaba) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mbunge wa Nkenge) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa umakini na kusikiliza, na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioalikwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta

Jedwali la Marekebisho linalojumuisha mapendekezo na ushauri wa Kamati uliowasilishwa kwa lengo la kuuboresha Muswada ulio mbele ya Bunge lako kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Kabla ya kuwasilisha maelezo ya kina kuhusiana na Muswada huu, naomba kuwasilisha maelezo ya utanguliza kuwa; Rushwa ni tatizo lenye madhara mabaya kwa jamii. Rushwa inaua demokrasia, inadumaza utawala wa sheria na kusababisha ukiukwaji wa haki za binadamu. Rushwa ni chanzo kimojawapo cha uharibifu wa rasilimali za umma, inaathiri utoaji huduma kwa umma na kuchangia kukua kwa vitendo vya uhalifu na vitendo vingine vinavyoathiri usalama.

Mheshimiwa Spika, Tangu Nchi yetu ipate uhuru mwaka 1961, Serikali imeendelea kuchukuwa hatua mbalimbali katika kuzuia na kupambana na rushwa. Hatua hizo ni pamoja na kusimamia maadili na kuweka sharti la uwajibikaji katika utumishi wa umma, kuweka mazingira wezeshi ya uwazi katika utendaji wa makampuni na mawakala wa sekta binafsi sanjari na kuweka mazingira sawa ya kiushindani na kibiashara na kudhibiti rushwa katika ununuzi wa umma na kuimarisha ukusanyaji mapato.

Mheshimiwa Spika; Hatua nyingine zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji habari, kushirikisha wadau katika kuzuia na kupambana na rushwa, kutunga sheria madhubuti ya kuzuia rushwa na kuanzishwa taasisi ya kusimamia utekelezaji wa Sheria hiyo pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika; Mwaka 2007 Serikali ilitunga Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329. Lengo la kutungwa kwa Sheria hii ni kuimarisha utawala bora na kutokomeza rushwa Tanzania Bara. Sheria hii, pamoja na masuala mengine, ilianzisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Taasisi ambayo ilipewa wajibu wa kuchukua hatua za kuzuia na kupambana na rushwa katika taasisi za umma na sekta binafsi Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika; Miaka 17 imepita tangu kutungwa kwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329. Kutungwa kwa Sheria hii kumewezesha utekelezaji wa majukumu mbalimbali yenye kuelekea kutimiza malengo ya Sheria hiyo, yaani kuimarisha utawala bora na kutokomeza rushwa nchini. Aidha, ili kuendana na mahitaji na mabadiliko mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya teknolojia, Sheria hii imefanyiwa marekebisho madogo mara mbili, mwaka 2018 kupitia Sheria Namba 7 ya 2018 na mwaka 2019 kupitia Sheria Namba II ya mwaka 2019 na kufanyiwa urekebu mara moja mwaka 2022. Pamoja na marekebisho mbalimbali na urekebu uliofanyika katika Sheria hii, bado Sheria hii inakabiliwa na upungufu ambao unapunguza ufanisi katika kufikia lengo la kutungwa kwake.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na Sheria ya Kuzuia na Kupambana Rushwa kufanyiwa urekebu Mwaka 2022, bado yamebainika mapungufu katika utekelezaji wa sheria hiyo ambapo baadhi ya mapungufu hayo ni pamoja na Sheria kutoainisha makosa ya rushwa katika uchaguzi, michezo na burudani; kukosekana tafsiri kwa baadhi ya misamiati muhimu iliyotumika kwenye sheria; kutokuwepo kwa uwiano wa makosa na adhabu; mkinzano kati ya Sheria hii na Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256; muda mfupi wa kushikilia mali za mtuhumiwa zinazodhaniwa kuwa ni mazalia ya uhalifu wakati wa uchunguzi, hivyo kukwamisha utaratibu wa utaifishaji; ufinyu wa tafsiri (narrow definition) ya maana ya umiliki wa mali inayosababisha kuwe na changamoto wakati wa kufanya uchunguzi wa tuhuma za limbikizo la mali zilizopatikana kwa njia isiyo halali; Sheria kutowatambua wadau wengine katika sekta binafsi kwenye mapambano dhidi ya rushwa mbali ya taasisi za kifedha pekee; kifungu kinachoelekeza namna ya kufanya uthaminishaji wa mali zinazochunguzwa chini ya Sheria kina changamoto kwenye utekelezaji wake; na sheria kutoa masharti yanayompa mamlaka Mkurugenzi Mkuu kuchunguza akaunti lakini kutompa mamlaka ya kuweka zuio la muda la akaunti za benki pale anapobaini fedha zilizo kwenye akaunti za watuhumiwa anazozichunguza zinadhaniwa kuhusika na makosa ya rushwa au mtuhumiwa anajihusisha na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika; Muswada huu unakusudia kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329. Vile vile, unakusudia kuimarisha lengo kuu la sheria ambalo ni kuimarisha utawala bora na kutokomeza rushwa nchini. Ufafanuzi wa upungufu na mapendekezo ya marekebisho ya vifungu unatolewa hapa chini:

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika vifungu mbalimbali vifuatavyo:
Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha baadhi ya tafsiri za misamiati iliyotumika katika Sheria na kuongeza fasili za misamiati mipya inayotokana na masharti mapya yanayopendekezwa kuongezwa katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha majukumu ya Naibu Mkurugenzi Mkuu. Lengo la marekebisho haya ni kufafanua majukumu ya Naibu Mkurugenzi Mkuu ili kurahisisha utendaji na uendeshaji wa Taasisi.

Mheshimiwa Spika; Kifungu cha 7 kinaipa TAKUKURU mamlaka ya kuzuia na kupambana na rushwa kwa kubainisha mianya ya rushwa katika taasisi za umma, mashirika ya umma na sekta binafsi, kuhamasisha umma kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa, kushirikiana na wadau katika mapambano dhidi ya rushwa, kufanya uchunguzi wa tuhuma za rushwa na kwa kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka kuendesha mashauri ya rushwa mahakamani. Kifungu hiki kipo kimya kuhusu mamlaka ya TAKUKURU kuchukua hatua kwa makosa ya rushwa yaliyotajwa kwenye sheria nyingine. Kifungu cha 7 kinarekebishwa ili kuiwezesha TAKUKURU kutekeleza jukumu la kuzuia na kupambana na rushwa hata chini ya sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuboresha na kuharakisha mchakato wa uchunguzi. Lengo la marekebisho haya ni kusaidia kugundua na kuzuia rushwa na makosa yanayohusiana nayo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kurekebishwa ili kudhibiti matumizi mabaya ya mamlaka ya upekuzi ya afisa uchunguzi wa TAKUKURU; Kwa sheria ilivyo sasa haijabainisha masharti kuwa ni kosa kwa mchunguzi kutumia vibaya mamlaka ya kupekua.

Mheshimiwa Spika, Vifungu vya 15, 16, 17, 18 na 20 vinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza wigo wa adhabu kwa makosa yanayohusiana na vitendo vya rushwa. Lengo la marekebisho hayo ni kuipa mamlaka mahakama ama kutoa amri ya kulipisha fedha (pecuniary penalty) pale mshtakiwa anapokutwa na hatia na kubainika alipata manufaa kutokana na kutenda vitendo vya rushwa au kuamuru kutaifishwa kwa mazalia/mali yatokanayo au yaliyowezesha kutendwa vitendo vya rushwa. Kwa wahalifu kuwanyang'anya mapato yaliyotokana na uhalifu itahakikisha hawafaidiki kutokana na vitendo vyao vya kihalifu.

Aidha kwa kuongeza wigo huo nchi itakuwa inatekeleza wajibu wake kwenye makubaliano iliyoingia ya kimataifa ikiwemo makubaliano ya kupambana na rushwa (United Nations Conventions Against Corruption -Article 31) ambayo yanataka mbali ya kumuadhibu mshtakiwa aliyekutwa na hatia lakini pia mali alizozipata kutokana na vitendo vya rushwa zitaifishwe.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 25 kilivyo sasa kinatoa adhabu kwa mtu aliye kwenye nafasi ya madaraka anayedai rushwa ya ngono bila kumuwajibisha anayemshawishi aliye kwenye nafasi ya madaraka kutenda kosa la rushwa ya ngono. Kifungu cha 25 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti zaidi ya kupambana na rushwa ya ngono. Marekebisho haya yanamlenga mtu anayeomba rushwa ya ngono kwa kutumia ushawishi wa mamlaka aliyonayo na mtu anayeshawishi au anayetoa ahadi au kutoa rushwa kwa mtu aliye na madaraka.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 27(1)(b) kinatumia neno "owns" ambalo kimsingi tafsiri yake haimbani mmiliki aliyeandikisha mali kwa

jina la mtu mwingine kwa lengo la kuficha umiliki. Kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupanua wigo kwa kujumuisha mali ambazo zipo chini ya mtuhumiwa lakini zinamilikiwa kwa jina la mtu mwingine. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia ukwepeshaji wa umiliki kwa kutumia uwakilishi mbadala na kuhakikisha uwajibikaji na utekelezaji wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 31 kimekuwa na utata katika kutoa tafsiri yake miongoni mwa watumiaji wa sheria. Utata umekuwa ni viini gani vinavyopaswa kuthibitishwa ili kosa liweze kuthibitika limetendwa, Kuna baadhi (one school of thought) wamekuwa wakiamini ili kuthibitisha kosa hilo la matumizi mabaya ya madaraka ni budi kuthibitisha viini hivi kwa pamoja yaani 'kuvunja sheria' na 'kutumia mamlaka yake vibaya' wakati kuna wengine (another school of thought) wamekuwa wakiamini inatosha kuthibitisha moja ya viini hivyo viwili kulingana na mazingira ya kosa. Utata huu mara kadhaa umekuwa unachelewesha kufanya uamuzi wa kufungua mashtaka na pia umekuwa ukiipa Mahakama changamoto katika kufikia maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 35 kinapendekezwa kurekebishwa ili kupanua wigo wa matumizi yake, Kilivyo sasa kimejifunga kwenye mikataba peke yake, kwa kufanyiwa marekebisho itahusu zaidi ya kupata mikataba serikalini.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 38A ni kipya kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuweka masharti yanayompa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kuzuia akaunti ya mtuhumiwa yenye fedha zinazochunguzwa baada ya kuifanyia upekuzi akaunti husika. Lengo la marekebisho haya zaidi ya kumpa mamlaka Mkurugenzi Mkuu kuzuia akaunti yenye fedha zinazohusishwa na vitendo vya rushwa ni kutekeleza wajibu wa nchini kutekeleza makubaliano ya kimataifa iliyoingia na kuahidi kutekeleza. Mfano Nchi inawajibika chini ya Ibara ya 31 (2) ya Makubaliano wa Umoja wa Mataifa Dhidi ya Rushwa (United Nations Convention Against Corruption), na chini ya Ibara ya 16 ya Makubaliano ya Umoja wa Afrika ya Kuzuia na

Kupamabana na Rushwa (Afrika Union Convention on Prevention and Combating of Corruption) ambayo yanazitaka Nchi Washirika kuweka utaratibu wa kisheria wa namna ya kuweka zuio la matumizi ya mapato yatokanayo na vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 43 (3) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kina mkinzano na kifungu cha 15(3) cha Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 (the Proceeds of Crime Act Cap 256) kwenye eneo la nani atakuwa mmiliki wa mazalia ya uhalifu na vifaa vilivyowezesha uhalifu baada ya kutaifishwa kwa amri ya Mahakama.

Mwaka 2018 Serikali ilifanya marekebisho katika Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 kuhusu mmiliki wa mali iliyotokana na amri ya mahakama ya kutaifisha mali iliyopatikana au iliyowezesha kutendeka kosa jinai ambapo ilimbadilisha mmiliki kutoka Msajili wa Hazina na kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha hata hivyo kwenye marekebisho hayo kifungu cha 43(3) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 hakikuguswa hivyo Msajili wa Hazina akaendelea kutajwa kama ndiye atakayekuwa Mmiliki wa mali zilizotaifishwa kutoka hapo ikawa inakinzana na Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256 ambayo inamtaja Katibu Mkuu Wizara ya Fedha.

Hivyo Kifungu cha 43(3) kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuweka ulinganifu wa masharti ya kifungu hicho na masharti ya kifungu cha 15(3) cha Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256. Kwa kufanyika marekebisho haya kutaoanisha masharti ya vifungu hivyo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na changamoto ya kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa katika maeneo ya uchaguzi, michezo na burudani kwa kutumia kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 ambacho kinahusu hongo, kifungo hicho kina sharti mahususi linalopaswa kuthibishwa ili kuthibitisha kosa la hongo, sharti hilo ni kiini cha "principal-agent

relationship" kati ya mtoaji na mpokeaji wa rushwa, Kiini hiki imekuwa hakiwezi kuthibitika kwenye kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa katika maeneo ya uchaguzi, michezo na burudani kwa kuwa kwenye maeneo hayo ya uchaguzi, michezo na burudani hakuna uhusiano wa "principal—agent" unaokuwepo kati ya mtoa rushwa na mpokeaji. Kutokana na changamoto hiyo, Serikali imekuwa ikishindwa kesi za aina hiyo pale zinzpofunguliwa mahakamani.

Ili kuondoa changamoto hiyo, Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza "SEHEMU YA TANO A" mpya ambayo inaweka masharti ya makosa yanayohusiana na masuala ya rushwa katika uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani bila kuweka takwa la kiini cha principal agent relationship. Kwa marekebisho haya itaiwezesha TAKUKURU kupambana na rushwa katika maeneo hayo ya uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani kwa ufanisi. Kwa kuweza kupambana na rushwa katika nyanja hizi kutahakikisha uadilifu na haki vinadumishwa katika michakato ya uchaguzi, matukio ya michezo, shughuli za michezo ya kubahatisha na tasnia ya burudani.

Mheshimiwa Spika; Kifungu cha 46 kinatoa masharti kwa TAKUKURU kushirikiana na sekta binafsi hususani Taasisi za kifedha katika kupambana na rushwa. Wigo huu wa wadau unaotambuliwa na kifungu hiki ni mdogo ukilinganishwa na wadau waliopo. Katika utekelezaji wa majukumu ya kiuchunguzi na uendeshaji mashtaka, Taasisi inapaswa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta binafsi zaidi ya waliobainishwa kwenye kifungu tajwa, wadau hao ni pamoja na makampuni binafsi, kama makampuni ya mawasiliano, asasi za kiraia, washirika wa maendeleo, taasisi za kidini, bodi za kitaaluma na taasisi za elimu na nyinginezo.

Hivyo kifungu cha 46 kinarekebishwa kwa lengo la kupanua wigo wa Taasisi kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ambao baadhi nimewabainisha. Lengo la marekebisho haya ni kupanua wigo wa ushirikiano ili kujumuisha

wadau wote muhimu ikiwa ni pamoja na sekta binafsi na sekta za umma.

Mheshimiwa Spika; Kifungu oha 49(a)(i) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 kinatamka kuwa uthamini wa mali (majengo) utatumia bei halisi ya vifaa vilivyotumika wakati wa ujenzi. Kifungu hiki kimekuwa na changamoto kwenye utekelezaji wake kwa sababu imekuwa ni vigumu kupata kumbukumbu za gharama hizo wakati wa uchunguzi kwani kwa kawaida uchunguzi unapofanywa inakuwa miaka mingi imeishapita na watu wengi wanapojenga huwa hawatunzi kumbukumbu za gharama za ununuzi wa vifaa walizofanya. Kifungu cha 49 kinarekebishwa ili kuzingatia viwango vya kitaaluma vya namna ya kufanya uthamini kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, Kurekebishwa kwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 kutaharakisha na kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wadau kwa:

(a) kuongeza kasi ya kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa;

(b) kuimarisha mchakato wa urejeshaji mali zilizopatikana kwa njia za rushwa; na

(c) kuendeleza utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa na Kikanda ya mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, 2024 (The Prevention and Combating of Corruption (Amendments) Act, 2024) na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, NAOMBA KUTOA HOJA.

GEORGE B. SIMBACHAWENE (Mb)
WAZIRI OFISI YA RAIS-MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA
2024

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Waziri ahsante sana. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, aje awasilishe Hoja ya Kamati. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria, kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 *[The Prevention and Combating of Corruption (Amendment) Bill, 2024]*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Tano, Kikao cha Hamsini na Sita kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 28 Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria

ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mikutano ya Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearings)* kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 16 Agosti, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa wadau mbalimbali ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 21 Agosti, 2024, Kamati ilikutana tena na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 *[The Prevention and Combating of Corruption (Amendment) Bill, 2024]*. Muswada huu unakusudia kurekebisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 ili kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada huu unalenga kuimarisha malengo makuu ya Sheria hiyo ambayo ni kuzuia, kuchunguza na kupambana na rushwa na makosa yanayohusiana na hayo na kuhakikisha taasisi inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya marekebisho ya sheria hii. Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu pamoja na maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati ilibaini changamoto au upungufu katika Ibara mbalimbali zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ibara ya pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha tatu cha sheria kinachohusu tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika sheria. Kamati ilielezwa kuwa marekebisho kwenye ibara hii kwa ujumla wake yanalenga kuboresha baadhi ya tafsiri za misamiati iliyotumika katika sheria, na kuongeza fasili za misamiati mipya inayotokana na masharti mapya yanayopendekezwa kuongezwa katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo yanaboresha tafsiri ya msamiati '*advantage*' kwa kuongeza maneno *'or sexual favor'* katika sheria. Maneno hayo yalitumika katika sheria lakini hayakuwa yamejumuishwa kwenye tafsiri. Vilevile Ibara inaongeza tafsiri za misamiati mipya inayotokana na masharti mapya yanayopendekezwa kuongezwa katika sheria. Baadhi ya misamiati hiyo ni *'election,' 'entertainment,' 'entity,' 'sport'* na *'sport manipulation.'*

Mheshimiwa Spika, ibara ya nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha saba cha sheria kinachohusu majukumu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Ibara hii inapendekeza kurekebisha kifungu cha saba katika aya ya (e) na (f) na kuongeza aya mpya (g) ili kutoa mamlaka kwa taasisi kutekeleza hatua za kuzuia na kupambana na rushwa kwa makosa yanayohusu rushwa na yanayohusiana na rushwa chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, au sheria nyingine yoyote pamoja na kuipatia taasisi mamlaka ya kuchukua hatua nyingine muhimu zenye lengo la kuharakisha uzuiaji na upambanaji dhidi ya rushwa zaidi ya hatua za kawaida zilizoorodheshwa katika kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuboresha maneno yaliyotumika katika sheria na kuiwezesha taasisi kutekeleza hatua muhimu za ziada katika kuzuia na kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, ibara ya tano ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 10 cha sheria kinachohusu mamlaka maalum ya uchunguzi. Ibara hii inapendekeza kurekebisha kifungu cha 10 (3) kwa kuweka masharti kuwa ni kosa kwa mtu ambaye atakaidi amri ya kufika mbele ya Afisa Uchunguzi wa Taasisi au kuwasilisha nyaraka pale zinapohitajika. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha na kuharakisha mchakato wa uchunguzi ili kusaidia kugundua na kuzuia rushwa na makosa yatokanayo na rushwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 inapendekeza kufuta Kifungu cha 25 kilichopo na kukiandika upya. Kifungu kinachopendekezwa kinaweka masharti kuwa ni kosa kwa mtu mwenye mamlaka kuomba rushwa ya ngono au kuomba upendeleo wa aina nyingine kama sharti la kutoa au kupata ajira, cheo, haki au upendeleo mwingine.

Mheshimiwa Spika, kifungu hicho pia kinaeleza kuwa ni kosa kwa mtu anayeahidi au kutoa rushwa ya ngono au upendeleo mwingine kwa mtu mwenye mamlaka au aliye katika nafasi ya mamlaka ili kumshawishi mtu huyo kutoa upendeleo wa ajira, cheo,

haki au upendeleo mwingine wowote. Kifungu kinaeleza kuwa, mtu atakayetiwa hatiani kwa makosa haya ataadhibiwa kwa kulipa faini isiyopungua shilingi millioni mbili na isiyozidi milioni kumi au kifungo kisichopungua miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12 na 17 za Muswada zinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 31 na kuongeza sehemu ya 5 (a) mtawalia kwenye sheria. Kamati ilielezwa kuwa, marekebisho kwenye ibara hii yanakusudia kufuta kifungu cha 31 na kukiandika upya ili kufafanua na kuondoa utata wa tafsiri katika vifungu hivyo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha tafsiri sahihi na isiyo na utata kwa matumizi ya sheria yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, sehemu ya 5(a) inayopendekezwa inaongeza kosa na adhabu ya rushwa katika uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani ili kuiwezesha taasisi kupambana na rushwa katika uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha taasisi kupambana na rushwa kwa ufanisi katika nyanja hizi na hivyo kuhakikisha uadilifu na haki vinadumishwa katika michakato ya uchaguzi, matukio ya michezo, shughuli za michezo ya kubahatisha na tasnia ya burudani.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 38 cha sheria kinachohusu kukamata au kushikilia mali za mtuhumiwa. Kamati ilielezwa kuwa marekebisho kwenye ibara hii yanakusudia kuongeza Kifungu cha 38A kinachoweka sharti la kumzuia mtuhumiwa kuhamisha fedha zinazochunguzwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara hiyo inampa mamlaka Mkurugenzi Mkuu baada ya kupata idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini *(DPP)*, kumwelekeza Afisa Uchunguzi Mwandamizi au Mkuu wa Taasisi kuzuia fedha za mtuhumiwa zinazohusika na uchunguzi zilizopo katika akaunti ya benki au katika miamala ya kifedha na kuchukua nyaraka yoyote kutoka benki au taasisi ya fedha kwa

muda wa siku 21 wakati idhini ya Mahakama kuendelea kuzuia fedha hizo ikifuatiliwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara pia inahusu mamlaka ya Mahakama kuongeza muda wa kuzuia fedha hizo ikiwa kuna sababu za msingi za kuhusisha fedha hizo na utendekaji wa kosa la rushwa, Mahakama pia wakati wowote inaweza kubadili amri ya zuio hilo. Lengo la marekebisho haya ni kuoanisha masharti ya sheria na mahitaji ya Ibara ya 51 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa, Ibara za nne na sita za Mkataba wa Umoja wa Afrika na kuifanya Serikali kuweza kurejesha mapato haramu yatokanayo na rushwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 43(3) ili kuweka masharti ya mali zilizotaifishwa kuwekwa chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anayehusika na Hazina badala ya Msajili wa Hazina. Lengo ni kuoanisha masharti ya kifungu hicho na masharti ya Kifungu cha 15(3) cha Sheria ya Mapato yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya ibara ya tatu ya Muswada, Kamati ilishauri tafsiri mpya ya neno "*sport*"' iandikwe upya bila kuwepo kwa maneno "*any football match*" kwa lengo la kujumuisha michezo yote bila kuonesha kipaumbele kwa mchezo mmoja wa mpira wa miguu tu, maneno "*any football match,*" yaani mechi ya mpira wa miguu kwenye tafsiri ya neno "*sport*" yameonesha kutoa kipaumbele kwa mchezo mmoja ikilinganishwa na aina mbalimbali

ya michezo iliyopo nchini. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya ibara ya nne ya Muswada, Kamati ilishauri marekebisho kwenye Kifungu cha 7(g) kinachofafanua kuwa, katika mapambano dhidi ya rushwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inaweza kuchukua hatua mbalimbali ili kudhibiti masuala ya rushwa zaidi ya zile zilizoorodheshwa kwenye sheria kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali kuondoa ombwe la tafsiri ya maneno hatua mbalimbali yaliyotumika kwenye sheria yaani *"such other measures"* na kutumia maneno *"appropriate measure"* yaliopo katika ibara ya pili ya Muswada yenye maana ya hatua za kisheria na kiutawala, yaani *"includes legal and administrative measures"* ili kuleta maana iliyokusudiwa kwa kuzuia ombwe la tafsiri linaloweza kumpa Afisa wa TAKUKURU mamlaka ya matumizi mabaya ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya ibara ya tano ya Muswada. Marekebisho ya Kifungu cha 10(3) kuhusu Mamlaka Maalum ya Uchunguzi kimeainisha kosa kwa mtu ambaye atakaidi wito kufika mbele ya Afisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa au kushindwa kuwasilisha nyaraka anazotakiwa kuziwasilisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikuwa na maoni kuwa zipo sababu za msingi zinazoweza kusababisha mtu kushindwa kufika mbele ya Afisa wa Taasisi kama vile ugonjwa, kuwa kizuizini chini ya mamlaka nyingine, kutokupokea ujumbe wa wito, kushindwa kutoa nyaraka kutokana na sababu za kisheria kama vile kutopata ruhusa kwa mtu mwenye mamlaka ya nyaraka hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, endapo itabainika kuwa mtu huyo amesema uwongo atakuwa ametenda kosa la kumdanganya Afisa Taasisi, kosa ambalo tayari lipo kwenye sheria. Hivyo basi, Kamati ilishauri Kifungu hicho kufanyiwa maboresho kwa kuzingatia sababu za msingi zinazoweza kutolewa na mtuhumiwa. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Ibara ya 10 ya Muswada. Mapendekezo ya mabadiliko ya sheria katika Kifungu cha 25, hasa ongezeko la Kifungu Kipya cha 25(1)(b), kimeleta hisia hasi kwa wadau waliofika mbele ya Kamati, asasi za kiraia na wanaharakati mbalimbali kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Wadau wengi wamelalamikia kifungu hicho kwa mtazamo kuwa kinawanyima wahanga wa rushwa ya ngono haki zao, stahiki na kinawapa kinga wahusika wa vitendo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa chimbuko la mapendekezo haya ni pamoja na mikataba ya kimataifa na kikanda. Ibara ya 15(a) ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa *(The United Nations Convention Against Corruption)* inaelekeza nchi wanachama kutunga sheria yenye kosa la kushawishi kutoa rushwa ya ngono. Ibara ya 4(1)(b) ya Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa *(The African Union Convention on Preventing and Combating Corruption)* inaelekeza nchi wanachama kutunga sheria yenye kosa la kushawishi kutoa rushwa ya ngono. Ibara ya 3(b) ya Mkataba wa *SADC* dhidi ya rushwa *(The SADC Protocol against Corruption)* inaelekeza nchi wanachama kutunga sheria yenye kosa la kushawishi kutoa rushwa ya ngono.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini, Tanzania Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi kwenye Sheria ya Kupambana na Rushwa na Makosa ya Uhujumu Uchumi ya mwaka 2023, Kifungu cha 52 kimeainisha kuwa ni kosa kushawishi kutoa rushwa ya ngono.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 kimeainisha kuwa ni kosa kwa mtu yeyote ambaye atatoa au ataahidi kutoa rushwa kwa namna yoyote ile ili kupata upendeleo wowote, mtu huyo atakuwa ametenda kosa la rushwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka mkazo kwa mtu mwenye mamlaka kutoshawishika kutoa upendeleo wa aina yoyote kwa ahadi ama kupewa rushwa ya ngono, Kamati inapendekeza kuongeza adhabu kwenye Kifungu cha 25 cha sheria hiyo, kwa adhabu ya faini ukomo wa juu kutoka kuwa shilingi milioni tano na kuwa milioni kumi na kwa adhabu ya kifungo ukomo wa juu kutoka kuwa miaka mitatu na kuwa miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeandaa jedwali la marekebisho ya sheria linalopendekeza maboresho hayo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Ibara za 12 na 17 za Muswada; Marekebisho ya vifungu vya 31, 46B, 46C na 46D yanapendekeza adhabu kwa makosa mbalimbali ya rushwa, kutokana na marekebisho ya tafsiri ya neno "*advantage*" lililopo kwenye ibara ya pili ya Muswada linalojumuisha maneno "*sexual favor.*" Kamati iliishauri Serikali kufanya marekebisho ya adhabu zilizopo, kwani itakuwa ngumu kujua thamani ya bei ya soko ya upendeleo wa kingono kama inavyoonekana kwenye Muswada "*or an amount equivalent to three times the market value of the advantage.*" Kwenye Muswada inaonekana hivyo. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri wa Kamati kwa kuondoa maneno "*sexual favor*" kwenye tafsiri ya neno "*advantage*" marekebisho ambayo yanaleta maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Ibara ya 14 ya Muswada. Marekebisho ya kwenye kifungu cha 38A (1) yanakusudia kumpa mamlaka Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi baada ya kupata idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini *(DPP),* kumwelekeza Afisa Uchunguzi Mwandamizi au Mkuu wa Taasisi kuzuia fedha za

mtuhumiwa zinazohusika na uchunguzi zilizopo katika akaunti ya benki au katika miamala ya kifedha na kuchukua nyaraka yoyote kutoka benki au taasisi ya fedha, kwa muda wa siku 21 wakati idhini ya Mahakama kuendelea kuzuia fedha hizo ikifuatiliwa.

Mheshimiwa Spika, awali, Kamati iliishauri Serikali kutafuta kwanza idhini ya Mahakama kabla ya kuzuia fedha au nyaraka yoyote kutoka benki au kwenye taasisi ya fedha. Kamati iliridhika na maelezo na ufafanuzi uliotolewa na Serikali juu ya ugumu wa kiuchunguzi na uwezekano wa fedha hizo kuhamishwa kutoka kwenye akaunti ya benki au nyaraka hizo kuharibiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati ilishauri Serikali kupunguza idadi ya siku kutoka siku 21 hadi siku 14 ambapo idhini ya Mahakama itafuatiliwa ili kuendelea kuzuia ama kuachilia akaunti ya mtuhumiwa. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Ibara ya 17 ya Muswada. Marekebisho ya Kifungu cha 46B (4) na 46D (5) yanapendekeza kuweka adhabu kwa mtu ambaye hatatoa taarifa pale ambapo atafahamu kosa la rushwa limefanyika kwa mujibu wa vifungu hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali kuweka adhabu katika Kifungu cha 46C(3) kinachotoa wajibu kwa mtu anayefahamu kuhusu uvunjaji wa kifungu hicho cha rushwa katika michezo ya bahati nasibu. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla. Ibara ya 15 inafanya marekebisho ya Kifungu cha 43(3) kuweka masharti ya mali zilizotaifishwa kwa makosa ya rushwa kuwekwa chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anayehusika na Hazina badala ya Msajili wa Hazina ili kuendana na masharti ya Kifungu cha 15(3) cha Sheria ya Mapato yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo hayo. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mazalia ya Uhalifu, Sura ya 256 *(The Proceeds of Crime Act, CAP 256)* kwa kuweka kifungu cha kuhamisha mali zilizokamatwa na Msajili wa Hazina kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha anayehusika na Hazina *(a transition provision)*.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba majina ya Wajumbe wa Kamati yasomeke kama yalivyo kwenye taarifa hii kwenye kumbukumbu za Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, kwa upekee, Kamati inampongeza na kumshukuru aliyekuwa Naibu Waziri wa Ofisi hii na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kwa ushirikiano mkubwa aliotupatia Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inampongeza Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kamati inamwahidi ushirikiano uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kumshukuru Ndugu Juma Selemani Mkomi, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee, Kamati inamshukuru kwa ushirikiano wake aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; Kamishna wa Polisi *CP* Salum Hamduni, na inampongeza kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inampongeza na kumwahidi ushirikiano Ndugu Crispin Chalamila, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc,* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya Kamati naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja kwa niaba ya Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama. Ahsante. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA WA MWAKA 2024 [*THE PREVENTION AND COMBATING OF CORRUPTION (AMENDMENT) BILL, 2024*] – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 [*The Prevention and Combating of Corruption (Amendment) Bill, 2024*].

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na tano, kikao cha hamsini na sita kwenye Bunge la 12, tarehe 28 Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina.

Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

## 1.2 Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mikutano ya Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearings*) kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 16 Agosti, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa wadau mbalimbali ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Nawashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kwa kuzingatia maoni ya Wadau. Mnamo tarehe 21 Agosti, 2024 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaye alijibu hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 [*The Prevention and Combating of Corruption (Amendment) Bill, 2024*]. Muswada huu unakusudia kurekebisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 ili kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake. Aidha, Muswada huu unalenga kuimarisha malengo makuu ya Sheria hiyo ambayo ni kuzuia, kuchunguza na kupambana na rushwa na makosa yanayohusiana na hayo na kuhakikisha Taasisi inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 2.2 Maudhui ya Marekebisho ya Sheria hii

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika Ibara mbalimbali zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

**2.2.1 Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 2 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 3 cha Sheria kinachohusu tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria. Kamati ilielezwa kuwa, Marekebisho kwenye Ibara hii kwa ujumla wake, yanalenga kuboresha baadhi ya tafsiri za misamiati iliyotumika katika Sheria, na kuongeza fasili za misamiati mipya inayotokana na masharti mapya yanayopendekezwa kuongezwa katika Sheria hii.

Mapendekezo hayo yanaboresha tafsiri ya msamiati "*advantage*" kwa kuongeza maneno "or *sexual favor*" katika Sheria, maneno hayo yalitumika katika sheria lakini hayakuwa yamejumuishwa kwenye tafsiri. Vilevile Ibara inaongeza tafsiri za misamiati mipya inayotokana na masharti mapya yanayopendekezwa kuongezwa

katika Sheria. Baadhi ya misamiati hiyo ni "*election, entertainment, entity, sport,* na *sport manipulation*".

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 4 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 cha Sheria kinachohusu majukumu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Ibara hii inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 katika aya (e) na (f) na kuongeza aya mpya (g) ili kutoa mamlaka kwa Taasisi kutekeleza hatua za kuzuia na kupambana na rushwa kwa makosa yanayohusu rushwa na yanayohusiana na rushwa chini ya sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa au sheria nyingine yoyote pamoja na kuipatia Taasisi mamlaka ya kuchukua hatua nyingine muhimu zenye lengo la kuharakisha uzuiaji na upambanaji dhidi ya rushwa zaidi ya hatua za kawaida zilizoorodheshwa katika kifungu hicho.

Lengo la marekebisho haya ni kuboresha maneno yaliyotumika katika sheria na kuiwezesha Taasisi kutekeleza hatua muhimu za ziada katika kuzuia na kupambana na rushwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 10 cha Sheria kinachohusu mamlaka maalum ya uchunguzi. Ibara hii inapendekeza kurekebisha kifungu cha 10 (3) kwa kuweka masharti kuwa ni kosa kwa mtu ambaye atakaidi amri ya kufika mbele ya Afisa uchunguzi wa Taasisi au kuwasilisha nyaraka pale zinapohitajika. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha na kuharakisha mchakato wa uchunguzi ili kusaidia kugundua na kuzuia rushwa na makosa yatokanayo na rushwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 10 inapendekeza kufuta kifungu cha 25 kilichopo na kukiandika upya. Kifungu kinachopendekezwa kinaweka masharti kuwa ni kosa kwa mtu mwenye mamlaka kuomba rushwa ya ngono au kuomba upendeleo wa aina nyingine kama sharti la kutoa au kupata ajira, cheo, haki au upendeleo mwingine wowote.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu hicho pia, kinaeleza kuwa ni kosa kwa mtu anayeahidi au kutoa rushwa ya ngono au upendeleo mwingine kwa mtu mwenye mamlaka au aliye katika nafasi ya mamlaka ili kumshawishi mtu huyo kutoa upendeleo wa ajira, cheo, haki au upendeleo mwingine wowote. Kifungu kinaeleza kuwa, mtu atakayetiwa hatiani kwa makosa haya, ataadhibiwa kwa kulipa faini isiyopungua shilingi millioni mbili na isiyozidi milioni kumi au kifungo kisichopungua miaka mitano

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 12 na 17 ya Muswada zinapendekeza kurekebisha kifungu cha 31 na kuongeza sehemu ya tano A mtawalia kwenye Sheria. Kamati ilielezwa kuwa, marekebisho kwenye Ibara hii yanakusudia kufuta kifungu 31 na kukiandika upya ili kufafanua na kuondoa utata wa tafsiri katika vifungu hivyo. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha tafsiri sahihi na isiyo na utata kwa matumizi ya sheria yaliyokusudiwa. Aidha, sehemu ya tano A inayopendekezwa inaongeza kosa na adhabu ya rushwa katika uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani ili kuiwezesha Taasisi kupambana na rushwa katika uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani.

Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Taasisi kupambana na rushwa kwa ufanisi katika nyanja hizi na hivyo kuhakikisha uadilifu na haki vinadumishwa katika michakato ya uchaguzi, matukio ya michezo, shughuli za michezo ya kubahatisha, na tasnia ya burudani.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 38 cha Sheria kinachohusu kukamata au kushikilia mali za mtuhumiwa. Kamati ilielezwa kuwa, marekebisho kwenye Ibara hii yanakusudia kuongeza kifungu cha 38A kinachoweka sharti la kumzuia mtuhumiwa kuhamisha fedha zinazochunguzwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara hiyo inampa mamlaka Mkurugenzi Mkuu baada ya kupata idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP),

kumuelekeza Afisa uchunguzi mwandamizi au Mkuu wa Taasisi kuzuia fedha za mtuhumiwa zinazohusika na uchunguzi zilizopo katika akaunti ya benki au katika miamala ya kifedha na kuchukua nyaraka yoyote kutoka benki au taasisi ya fedha, kwa muda wa siku ishirini na moja wakati idhini ya mahakama kuendelea kuzuia fedha hizo ikifuatiliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara pia inahusu mamlaka ya mahakama kuongeza muda wa kuzuia fedha hizo ikiwa kuna sababu za msingi za kuhusisha fedha hizo na utendekaji wa kosa la rushwa, Mahakama pia wakati wowote inaweza kubadili amri ya zuio hilo.

Lengo la marekebisho haya ni kuoanisha masharti ya Sheria na mahitaji ya Ibara ya 51 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa Dhidi ya Rushwa, Ibara ya 4 na 6 za Mkataba wa Umoja wa Afrika na kuifanya Serikali kuweza kurejesha mapato haramu yatokanayo na rushwa.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 15 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 43(3) ili kuweka masharti ya mali zilizotaifishwa kuwekwa chini ya Katibu Mkuu wa wizara ya Fedha anayehusika na Hazina badala ya Msajili wa Hazina. Lengo ni kuoanisha masharti ya kifungu hicho na masharti ya kifungu cha 15(3) cha Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

### 3.1.1 Marekebisho ya Ibara ya 3 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishauri tafsiri mpya ya neno "*sport*" iandikwe upya bila kuwepo kwa maneno "*any football match*" kwa lengo la kujumuisha michezo yote bila kuonesha kipaumbele kwa mchezo moja wa mpira wa miguu, maneno "*any football match*" yani mechi ya mpira wa miguu kwenye tafsiri ya neno "*sport*" yameonesha kutoa kipaumbele kwa mchezo mmoja ikilinganishwa na aina mbalimbali ya michezo iliyopo nchini. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.1.2 Marekebisho ya Ibara ya 4 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishauri marekebisho kwenye kifungu cha 7(g) kinachofafanua kuwa, katika mapambano dhidi ya rushwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inaweza kuchukua hatua mbalimbali ili kudhibiti masuala ya Rushwa zaidi ya zile zilizoorodheshwa kwenye Sheria kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliishauri Serikali kuondoa ombwe la tafsiri ya maneno hatua mbalimbali yaliotumika kwenye sheria yaani "*such other measures*" na kutumia maneno "*appropriate measure*" yaliopo katika Ibara ya 2 ya Muswada yenye maana ya hatua za Kisheria na Kiutawala yaani "*includes legal and administrative measures*" ili kuleta maana iliokusudiwa kwa kuzuia ombwe la tafsiri linaloweza kumpa Afisa wa Takukuru mamlaka ya matumizi mabaya ya kifungu hicho.

**Mheshimiwa Spika,** Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.1.3 Marekebisho ya Ibara ya 5 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Marekebisho ya kifungu cha 10(3) kuhusu Mamlaka Maalum ya Uchunguzi kimeanisha kosa kwa mtu ambaye

atakaidi wito kufika mbele ya Afisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa au kushidwa kuwasilisha nyaraka anazotakiwa kuziwasilisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikuwa na maoni kuwa zipo sababu za msingi zinazoweza kusababisha mtu kushindwa kufika mbele ya Afisa wa Taasisi kama vile ugonjwa, kuwa kizuizini chini ya mamlaka nyingine, kutokupokea ujumbe wa wito, kushindwa kutoa nyaraka kutokana na sababu za kisheria kama vile kutopata ruhusa kwa mtu mwenye mamlaka ya nyaraka hizo.

Aidha, endapo itabainika kuwa mtu huyo amesema uwongo atakuwa ametenda kosa la kumdanganya Afisa Taasisi, kosa ambalo tayari lipo kwenye sheria. Hivyo basi, Kamati ilishauri Kifungu hicho kufanyiwa maboresho kwa kuzingatia sababu za msingi zinazoweza kutolewa na mtuhumiwa. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.1.4 Marekebisho ya Ibara ya 10 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria katika kifungu cha 25 hasa ongezeko la kifungu kipya cha 25(1)(b) kimeleta hisia hasi kwa Wadu waliofika mbele ya Kamati, Asasi za Kiraia na Wanaharakati mbalimbali kwenye vyombo vya Habari na Mitando ya Kijamii. Wadau wengi wamelalamikia kifungu hicho kwa mtazamo kuwa kinawanyima wahanga wa rushwa ya ngono haki zao stahiki na kinawapa kinga wahusika wa vitendo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa Chimbuko la mapendekezo haya ni pamoja na Mikataba ya Kimataifa na Kikanda, Ibara ya 15(a) ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa Dhidi ya Rushwa (*United Nations Convention Against Corruption*) inaelekeza nchi wanachama kutunga Sheria yenye kosa la kushawishi kutoa rushwa ya ngono, Ibara ya 4 (1) (b) ya Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (*African Union Convention on*

*Preventing and Combating Corruption*) inaelekeza nchi wanachama kutunga Sheria yenye kosa la kushawishi kutoa rushwa ya ngono, Ibara ya 3 (b) ya Mkataba wa SADC dhidi ya Rushwa (*SADC Protocal against Corruption*) inaelekeza nchi wanachama kutunga Sheria yenye kosa la kushawishi kutoa rushwa ya ngono.

**Mheshimiwa Spika,** Hapa Nchini, Tanzania Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi kwenye Sheria ya Kupambana na Rushwa na Makosa ya Uhujumu Uchumi ya mwaka 2023 kifungu cha 52 kimeainisha kuwa ni kosa kushawishi kutoa rushwa ya ngono.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuwa kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, sura ya 329 imeainisha kuwa ni kosa kwa mtu yoyote ambae atatoa au ataahidi kutoa rushwa kwa namna yoyote ile ili kupata upendeleo wowote mtu huyo atakuwa ametenda kosa la rushwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuweka mkazo kwa mtu mwenye mamlaka kutoshawishika kutoa upendeleo wa aina yoyote kwa ahadi ama kupewa rushwa ya ngono. Kamati inapendekeza kuongeza adhabu kwenye kifungu cha 25 cha Sheria hiyo, kwa adhabu ya faini ukomo wa juu kutoka kuwa shilingi milioni tano na kuwa milioni kumi, na kwa adhabu ya kifungu ukomo wa juu kutoka kuwa miaka mitatu na kuwa miaka kumi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeandaa jedwali la Marekebisho ya Sheria yanayopendekeza maboresho hayo.

### 3.1.5 Marekebisho ya Ibara ya 12 na 17 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Marekebisho ya vifungu vya 31, 46B, 46C na 46D yanapendekeza adhabu kwa makosa mbalimbali ya rushwa, kutokana na marekebisho ya tafsiri ya neno "*advantage*" lililopo kwenye Ibara ya 2 ya Muswada linalo jumuisha neno "*sexual favour*" Kamati iliishauri Serikali kufanya marekebisho ya adhabu zilizopo kwani itakuwa ngumu kujua thamani ya bei ya soko ya upendeleo

wa kingono kama inavyoonekana kwenye muswada "*or an amount equivalent to three times the market value of the advantage***".** Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri wa Kamati kwa kuondoa maneno "*sexual favour*" kwenye tafsiri ya neno "*advantage*" marekebisho ambayo yanaleta maana iliyokusudiwa.

### 3.1.6 Marekebisho ya Ibara ya 14 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Marekebisho ya kwenye kifungu cha 38A (1) yanakusudia kumpa mamlaka Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi baada ya kupata idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), kumuelekeza Afisa uchunguzi mwandamizi au Mkuu wa Taasisi kuzuia fedha za mtuhumiwa zinazohusika na uchunguzi zilizopo katika akaunti ya benki au katika miamala ya kifedha na kuchukua nyaraka yoyote kutoka benki au taasisi ya fedha, kwa muda wa siku ishirini na moja wakati idhini ya mahakama kuendelea kuzuia fedha hizo ikifuatiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Awali Kamati iliishauri Serikali kutafuta kwanza idhini ya Mahakama kabla ya kuzuia fedha au nyaraka yoyote kutoka benki au kwenye taasisi ya fedha. Kamati iliridhika na maelezo na ufafanuzi uliotolewa na Serikali juu ya ugumu wa kiuchunguzi na uwezekano wa fedha hizo kuhamishwa kutoka kwenye akaunti ya benki au nyaraka hizo kuharibiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa msingi huo, Kamati ilishauri Serikali kupunguza idadi ya siku kutoka siku ishirini na moja hadi siku kumi na nne ambapo idhini ya Mahakama itafuatiliwa ili kuendelea kuzuia ama kuachilia akaunti ya Mtuhumiwa. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.1.7 Marekebisho ya Ibara ya 17 ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Marekebisho ya Kifungu cha 46B (4) na 46D (5) yanapendekeza kuweka adhabu kwa mtu ambaye hatatoa taarifa

pale ambapo atafahamu kosa la Rushwa limefanyika kwa mujibu wa vifungu hivyo. Kamati iliishauri Serikali kuweka adhabu katika kifungu cha 46C (3) kinachotoa wajibu kwa mtu anayefahamu kuhusu uvunjaji wa kifungu hicho cha Rushwa katika michezo ya bahati nasibu. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.2 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 15 inafanya marekebisho ya Kifungu cha 43 (3) yanaweka masharti ya mali zilizotaifishwa kwa makosa ya Rushwa kuwekwa chini ya Katibu Mkuu wa wizara ya Fedha anayehusika na Hazina badala ya Msajili wa Hazina, ili kuendana na masharti ya kifungu cha 15(3) cha Sheria ya Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Sura ya 256.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na Mapendekezo hayo. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kufanya marekebisho kwenye sheria ya Mazaliia ya Uhalifu, Sura ya 256 (*The Proceeds of Crime Act, CAP 256*) kwa kuweka kifungu cha kuhamisha mali zilizokamatwa na Msajili wa Hazina kwenda kwa Katibu Mkuu wa wizara ya Fedha anayehusika na Hazina yaani "*a transition provision*".

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb - **M/Mwenyekiti**
2) Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb - Mjumbe

3) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
4) Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb - Mjumbe
5) Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb - Mjumbe
6) Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb - Mjumbe
7) Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb - Mjumbe
8) Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe
9) Mhe. Omar Issa Kombo, Mb - Mjumbe
10) Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb - Mjumbe
11) Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - Mjumbe
12) Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb - Mjumbe
13) Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe
14) Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb - Mjumbe
15) Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb - Mjumbe
16) Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb - Mjumbe
17) Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
18) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb - Mjumbe
19) Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe
20) Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb -Mjumbe
21) Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb - Mjumbe
22) Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, aidha kwa upekee Kamati inampongeza na kumshukuru aliyekuwa Naibu Waziri wa Ofisi hii na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb) kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kwa ushirikiano mkubwa alioupatia Kamati,

Kamati pia inampongeza Mhe. Deus Clement Sangu (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati inamuahidi ushirikiano uliotukuka. Kamati inaendelea kumshukuru Ndg. Juma Selemani Mkomi Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala

Bora na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Kiupekee Kamati inamshukuru kwa ushirikiano wake aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Kamishna wa Polisi Cp. Salum R. Hamduni na inampongeza kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga. Aidha, Kamati inampongeza na kumuahidi ushirikiano Ndugu Crispin F. Chalamila, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya Kamati naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

2 Septemba, 2024

**SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, ahsante sana kwa kuwasilisha taarifa hii ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Hamza Saidi Johari, aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuwasilisha hoja ya Serikali mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama leo mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara yangu ya kwanza tangu nilipoteuliwa kushika nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tarehe 14 Agosti, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu na kuona ni vyema nimsaidie yeye na Serikali yetu katika nafasi hii ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Napenda kumwahidi kwamba nitatekeleza majukumu yangu haya aliyonipa kwa nguvu zangu zote, kwa moyo wangu wote na kwa akili zangu zote kwa maslahi mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi Mbunge, kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge

na Uratibu, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge, kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa Balozi Mahmoud Thabit Kombo, Mbunge, kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, niruhusu pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa na kubadilishwa kutoka Wizara moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika. Namtakia heri katika kutekeleza majukumu hayo makubwa na kuiwakilisha nchi yetu Tanzania kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua umepokea pongezi nyingi kufuatia kuchaguliwa kwako kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani. Hata hivyo, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu kama Mbunge niruhusu nami nikupongeze kwa kushika nafasi hiyo. Ninaamini kuwa umahiri na weledi wako katika kuongoza Bunge hili ndivyo vimewezesha wewe kuchaguliwa katika nafasi hiyo adhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia

vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa Kutunga Sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Naishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuahidi kwamba mimi na Ofisi yangu tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge lako Tukufu katika kutekeleza majukumu yake. Nawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bwana Samwel Marco Maneno kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile nampongeza Bwana Onorious John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kufanikisha maandalizi ya Muswada huu kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukurani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, na Mbunge wa Madaba na Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa umakini sambamba na maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]* unaopendekeza kufanya marekebisho katika sheria tatu zifuatazo: -

(i) Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Mkuu, Sura ya 388 *[The Deep -Sea Fisheries Management and Development Act, Cap. 388;*

(ii) Sheria ya Madini, Sura ya 123 *[The Mining Act, Cap. 123* na;

(iii) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura ya 280 *[The Tanzania Fisheries Research Institutes Act, Cap. 280.*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza inayohusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo sheria mbalimbali zimerekebishwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388. Sheria hii ilitungwa mwaka 2020 baada ya kufutwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Bahari Kuu ya Mwaka 1998. Sheria hii haijawahi kufanyiwa marekebisho. Hivyo, marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hii ni ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Nne ya Muswada ikisomwa pamoja na aya ya B ya Jedwali la Marekebisho inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 11 kwa madhumuni ya kuainisha Mamlaka ya Uteuzi wa Wajumbe wa Kamati ya Watalamu ya Ushauri walioainishwa katika aya za (c), (d), (e) na (f) na kubainisha muda wao wa kuhudumu kama Wajumbe wa Kamati. Hivyo

inapendekezwa kuwa Wajumbe tajwa wateuliwe na Waziri mwenye dhamana ya uvuvi na kuhudumu kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, lengo la mapendekezo ya marekebisho ya Kifungu cha 11 ni kuondoa ombwe lililopo sasa kuhusiana na mamlaka ya uteuzi na muda wa Wajumbe kushika wadhifa huo kwenye Kamati ya Watalamu ya Ushauri.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Tano ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 16 (1) kwa kufuta na kuandika upya aya (n) ili kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kuteua Maafisa wa Utoaji leseni, Wakaguzi wa Uvuvi na Maafisa walioidhinishwa kutoka miongoni mwa watumishi wa Mamlaka na kuteua waangalizi wa uvuvi kutoka kwenye Mamlaka au nje ya Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii ilivyo sasa aya ya (n) inamtaka Mkurugenzi Mkuu kuteua maafisa hao kutoka miongoni mwa Maafisa wa Mamlaka pekee. Hivyo, madhumuni ya marekebisho haya ni kupanua wigo wa uteuzi ili kuwezesha watu ambao sio Maafisa wa Mamlaka kuteuliwa kuwa waangalizi wa uvuvi kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Sita ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 35 ili kuweka masharti yanayoanzisha kosa la kujihusisha na shughuli zozote za uvuvi wa Bahari Kuu bila kibali halali. Kwa sasa sheria inakataza kufanya shughuli za uvuvi bila kibali halali, lakini haijaweka sharti linaloanzisha kosa kutokana na kukiuka masharti hayo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na marekebisho ya kifungu cha 35, Jedwali la Pili linarekebishwa ili kujumuisha katika orodha ya makosa na adhabu. Kosa jipya lililoundwa chini ya mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 35, ambapo kiwango cha juu cha faini kinachopendekezwa kutokana na kosa hili ni dola za Kimarekani milioni moja. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuimarisha utekelezaji *(enforcement)* kutokana na makosa hayo kufanywa

mara kwa mara na hivyo kupelekea Serikali kupoteza mapato kutokana na kufanyika kwa shughuli za uvuvi wa Bahari Kuu bila vibali halali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura ya 123. Sheria hii ilitungwa mwaka 2010 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara 13. Marekebisho yanapendekeza kurekebisha jumla ya vifungu 12 na vifungu vipya viwili vinapendekezwa kuongezwa. Vifungu vinavyopendekezwa kurekebishwa ni vifungu vya 4, 8, 27F, 66, 73, 86A, 87, 88, 90A, 100C, 100D na 106. Aidha, vifungu vipya vinavyopenda kuongezwa ni kifungu cha 5B na 27I.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha Nne cha Sheria ya Madini, Sura ya 123 kama ifuatavyo; katika tafsiri ya msamiati "madini ya ujenzi" *(industrial minerals),* kwa kufuta neno "*lime*" na badala yake kuweka neno "*limestone*". Lengo la marekebisho haya ni kuondoa ukakasi uliojitokeza kwa kuwa "*lime*" ni zao la madini ya "*limestone*" yanayochimbwa na hivyo neno hilo haliakisi maana iliyokusudiwa katika muktadha wa madini ya ujenzi yanayochimbwa.

Mheshimiwa Spika, katika tafsiri ya msamiati "kiapo cha uadilifu" *(integrity pledge),* kwa kufuta maneno "*mineral right holder*" na badala yake kuweka maneno "*mineral rights holders, licenced dealers and licenced brokers.*" Marekebisho haya yana lengo la kuwajumuisha wafanyabiashara wa madini yaani "*licenced dealers and licenced brokers*" katika mawanda ya watu na taasisi zinazopaswa kuapa kiapo cha uadilifu. Kwa hali ilivyo sasa, wafanyabiashara wa madini hawana wajibu wowote wa kuapa kiapo hicho cha uadilifu katika tasnia ya madini.

Mheshimiwa Spika, katika tafsiri ya msamiati "madini ya nishati" *(energy minerals),* kwa kuongeza rasilimali za jotoardhi *(geothermal)* katika orodha ya madini ambayo yanatambuliwa chini ya sheria. Lengo la marekebisho haya ni kufanya madini ambata kama vile

*sulphur*, zebaki, *lithium, helium* na madini mengine ambayo ni rasilimali za jotoardhi ambayo hubeba nishati ya joto yasimamiwe na sheria kama madini ya nishati kwa kuongeza tafsiri mpya ya msamiati "rasilimali za jotoardhi" *(geothermal resources)*. Lengo la kuongezwa kwa tafsiri hii ni kutoa ufafanuzi wa kina wa msamiati huo, hasa ikizingatiwa kwamba maneno "*geothermal resources*" yametumika pia katika tafsiri ya msamiati "madini ya nishati".

Mheshimiwa Spika, pia kwa kuongeza tafsiri mpya ya msamiati "mnada wa madini" *(mineral auction)*. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa msamiati huo ambao umetumika katika vifungu vya 87 na 100C vinavyopendekezwa kurekebishwa na Muswada huu kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "*gross value*".

Mheshimiwa Spika, katika tafsiri mpya inayopendekeza, maneno "*refining ore*" yaliyokuwepo katika tafsiri ya zamani yameondolewa. Kuondolewa kwa maneno hayo ni kutokana na kuwa utozaji wa mrabaha wakati wa usafishaji *(refinery)* unaathiri maduhuli ya Serikali ikilinganishwa na utoaji wa mrabaha kwa kuzingatia bei ya soko. Aidha, tafsiri hiyo inapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuiwianisha na tafsiri iliyopo kwenye kifungu cha 87(6) cha sheria ambacho pia kimetoa tafsiri ya msamiati *gross value*.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "uchenjuaji wa madini" *(mineral processing),* msingi wa mapendekezo hayo ya marekebisho ni kutokana na kwamba tafsiri hiyo kama ilivyo sasa haijitoshelezi kwa kuwa haijumuishi shughuli nyingine muhimu *(unit operations)* katika uchenjuaji au usafishaji wa madini. Katika tafsiri ya msamiati "leseni ya kati ya uchimbaji madini" *(mining licence),* kwa kufuta tarakimu dola 100,000 na badala yake kuweka tarakimu dola 5,000,000.

Mheshimiwa Spika, msingi wa mapendekezo haya ni kutokana na mwingiliano wa kiwango cha mtaji wa uwekezaji kati ya leseni

ndogo ya uchimbaji wa madini *(primary mining license)* na leseni ya kati ya uchimbaji wa madini kwa maana ya *mining license*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Madini, Sura ya 123 leseni za uchimbaji wa madini zipo za aina tatu na zinazotofautishwa kwa kuzingatia viwango vya mtaji wa uwekezaji, ambapo leseni ndogo ya uchumbaji wa madini mtaji wake ni kiasi chochote chini ya dola 5,000,000 na leseni ya kati ya uchimbaji wa madini mtaji wake ni kuanzia dola 100,000 hadi dola 100,000,000 na leseni kubwa ya uchimbaji wa madini mtaji wake unapaswa kuwa zaidi ya dola 100,000,000.

Mheshimiwa Spika, hivyo, inapendekezwa kwamba leseni ya kati ya uchimbaji wa madini mtaji wake uanzie dola 5,000,000 ambayo ni ukomo wa mtaji wa leseni ndogo ya uchimbaji wa madini, badala yake mtaji huo kuanzia dola 100,000 kiwango ambacho kinaingiliana na kipo ndani ya wigo wa mtaji wa leseni ndogo ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, katika tafsiri ya msamiati "*processing area*" kwa kufuta neno "*milling*" na badala yake kuweka neno "*comminution.*" Msingi wa mapendekezo haya ni kwamba neno "*milling*" lililopo sasa halina utoshelevu kwa kuwa kitaalamu linaacha hatua nyingine za usagaji zikiwemo "*crushing*" na "*grinding*". Aidha, neno "*comminution*" kitaalamu linajumuisha "*crushing*", "*milling*" na "*grinding*".

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 ya Muswada ikisomwa pamoja na aya ya C ya Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 5B ili kumpa Waziri mamlaka ya kutangaza baadhi ya madini kuwa ya muhimu na ya kimkakati kwa Jamhuri ya Muungano, baada ya kupokea mapendekezo kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kutambua madini muhimu na ya kimkakati ili kukuza maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi na kudumisha usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 11 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 8(1) kwa kuongeza aya mpya ya (c) ili kuweka ukomo wa muda kwa maombi ya kupewa haki ya madini pale mwombaji anaposhindwa kulipa ada ya maombi kuhusiana na eneo husika. Kwa hali ilivyo sasa, kwa kuwa maombi ya haki ya madini yanafanyika kwa njia ya mtandao, kumekuwepo na maombi mengi ya leseni za madini ambayo yapo kwenye masjala ya Tume ya Madini na kwamba Sheria ya Madini haijaweka masharti ya ukomo wa muda wa malipo na mamlaka ya kuondoa maombi hayo pale ambapo mwombaji anashindwa kulipa ada ya maombi kuhusiana na eneo husika.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mlundikano wa maombi ambayo waombaji wake wameshindwa kulipa ada za maombi kwa muda mrefu pia kunazuia waombaji wengine kuomba eneo husika kutokana na kuwepo kwa maombi ambayo hayajalipiwa ada kwa muda mrefu. Lengo la marekebisho ni kuhakikisha malipo ya ada ya maombi ya haki ya madini *(mineral right)* yanafanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 27F ili kuweka adhabu kwa wamiliki wa haki za madini ambao wanatoa taarifa za uongo au zenye kupotosha au kushindwa kuwasilisha taarifa sahihi za madini. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha utii wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya cha 27I ili kuanzisha Maabara ya Madini ya Tume ya Madini. Lengo la marekebisho hayo ni kuirasimisha taasisi hiyo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa msingi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 66 ili kuweka adhabu kwa mtu atakayeshindwa kulipa ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha utii wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 73 ili kutofautisha leseni za wafanyabiashara wa madini ya *Tanzanite* na wafanyabiashara wa madini ya vito vingine vya rangi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka udhibiti wa madini ya *Tanzanite* kwa namna maalum ya kutangaza kwa kuzingatia uwepo wa madini hayo wa kipekee nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 16 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 86A ili kuweka masharti kwamba mwingizaji wa madini nchini hatatakiwa kulipa mirabaha kwa madini yanayoingizwa nchini endapo atathibitisha kuwa amelipa mirabaha katika nchi yalikotoka madini. Lengo la marekebisho haya ni kuepusha ulipaji wa mirabaha zaidi ya mara moja.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 87 kwa kuongeza viwango vya mirabaha inayopaswa kulipwa Serikalini na wafanyabiashara wa madini ya vito yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi ambayo yamenunuliwa katika minada ya madini na Maonyesho ya Kimataifa ya Madini ya Vito. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka katika shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18 ya Muswada ikisomwa pamoja na aya ya D ya Jedwali la Marekebisho, inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 88 kwa kufuta maneno: *"has the meaning attributed to those words in subsection (6) of section 87 and that provision*." Kwa kuwa kifungu cha 87(6) kinachorejewa kimependekezwa kufutwa chini ya Ibara ya 17(b) ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 90A ili kuondoa masharti kuhusu ukaguzi kwa madini yanayouzwa wakati wa mnada wa madini unaosimamiwa na Serikali au unaotokana na Maonesho ya Kimataifa ya Vito. Lengo la marekebisho haya ni kuepusha gharama

za minada kwa wafanyabiashara na kuongeza ushiriki wao katika muda unaosimamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 20 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 100A ili kupunguza vikwazo kwa usafirishaji nje ya nchi vito vya thamani vilivyouzwa na Serikali au katika Maonesho ya Kimataifa ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 100D ili kuruhusu biashara ya makinikia ndani ya nchi. Kwa sasa sheria inazuia biashara ya makinikia ndani na nje ya nchi. Lengo la marekebisho haya ni kuvutia uwekezaji katika viwanda vya madini ghafi nchini.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 106 ili kuwataka wafanyabiashara wa madini, mawakala au madalali walio na leseni kuapa kiapo cha uadilifu. Lengo la marekebisho haya ni kudumisha viwango vya maadili, uaminifu na uadilifu katika shughuli za madini pamoja na kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne na ya mwisho ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura ya 280. Sheria hii iliyotungwa mwaka 2016 haijawahi kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 24 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 21 ili kuongeza maneno ya nyongeza mwishoni mwa kifungu hicho yanayoweka bayana kwamba, ukiukaji wowote wa masharti yaliyoainishwa katika aya (a) na (b) unaweza kufanya kibali cha utafiti kusitishwa. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa watafiti wote wa masuala ya uvuvi wanazingatia masharti ya sheria kuhusiana na tafiti wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 25 na ya mwisho ya Muswada inapendekeza kufuta kifungu cha 24 cha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura ya 280 kwa kuwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Uvuvi yanakinzana na mamlaka yaliyotolewa kwa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuepusha mgongano wa mamlaka na kuiwezesha sheria itekelezeke kwa urahisi na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, niruhusu nitumie fursa hii kuishukuru familia yangu, mke wangu Neema Johari, binti zangu Tamika Johari, Saritha Johari na kijana wangu Reefat Johari kwa kuwa nami katika kila hatua ya utumishi wangu hadi hatua hii niliyofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru mama yangu Bi. Mwatunza Said na Marehemu Baba yangu Mzee Said Mohamed Johari, kwa malezi yao mazuri kwangu. Hakika uwepo wao una mchango mkubwa katika mafanikio yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]* kama ulivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho, ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

## HOTUBA YA MHESHIMIWA HAMZA SAIDI JOHARI (MB), MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI WA MWAKA 2024 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) BILL, 2024) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuwasilisha hoja ya Serikali mbele ya Bunge lako tukufu, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama leo mbele ya Bunge lako tukufu kwa mara yangu ya kwanza tangu nilipoteuliwa kushika nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tarehe 14 Agosti, 2024.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kubwa kwangu, na kwa kuona ni vyema nimsaidie yeye na Serikali yetu katika nafasi hii ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Napenda kumuahidi kwamba nitatekeleza majukumu haya aliyonipa kwa nguvu zangu zote, kwa moyo wangu wote na kwa akili zangu zote kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nitumie fursa hii kuwapongeza Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Balozi Mahmoud T habit Kombo (Mb.) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, niruhusu pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa na kubadilishwa kutoka Wizara moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuungana na watanzania wenzangu kumpongeza Mhe. Dkt. Faustine Engelbert

Ndugulile kwa kuchanguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika. Ninamtakia kheri katika kutekeleza majukumu hayo makubwa na kuiwakilisha Nchi yetu Tanzania kimataifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nisharti pamoja na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninatambua umepokea pongezi nyingi kufuatia kuchaguliwa kwako kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Lakini kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako tukufu kama Mbunge, niruhusu nami nikupongeze kwa kushika nafasi hiyo. Ninaamini kuwa umahiri na weledi wako katika kuongoza Bunge hili ndivyo vimewezesha wewe kuchaguliwa katika nafasi hiyo adhimu. Nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, (ndc.) na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuahidi kwamba mimi na Ofisi yangu tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge lako Tukufu katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bw. Samwel Marco Maneno kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, ninampongeza Bw. Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kufanikisha maandalizi ya Muswada huu kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mbunge wa Madaba) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Florent Laurent Kyombo (Mbunge wa Nkenge) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa umakini sambamba na maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024) unaopendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tatu (3) zifuatazo:

1. Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 (The Deep Sea Fisheries Management and Development Act, cap. 388);

2. Sheria ya Madini, Sura ya 123 (The Mining Act, Cap. 123); na

3. Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura ya 280 (The Tanzania Fisheries Research Institute Act, Cap. 280).

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nne.

Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo Sheria mbalimbali zimerekebishwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388. Sheria hii ilitungwa mwaka 2020 baada ya kufutwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Bahari Kuu ya Mwaka 1998. Sheria hii haijawahi kufanyiwa marekebisho, hivyo marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hii ni ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 ya Muswada ikisomwa pamoja na aya ya B ya Jedwali la Marekebisho inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 1 1 kwa madhumuni ya kuainisha mamlaka ya uteuzi wa wajumbe wa Kamati ya Wataalam ya Ushauri walioainishwa katika aya za (c), (d), (e) na (f) na kubainisha muda wao wa kuhudumu kama wajumbe wa Kamati. Hivyo, inapendekezwa kuwa, wajumbe tajwa wateuliwe na Waziri mwenye dhamana ya uvuvi na kuhudumu kwa kipindi cha miaka mitatu. Lengo la mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 1 1 ni kuondoa ombwe lililopo sasa kuhusiana na mamlaka ya uteuzi na muda wa wajumbe kushika wadhifa huo kwenye Kamati ya Wataalam ya Ushauri.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 16(1) kwa kufuta na kuandika upya aya (n) ili kumpa Mkurugenzi Mkuu mamlaka ya kuteua maafisa wa utoaji leseni, wakaguzi wa uvuvi na maafisa walioidhinishwa kutoka miongoni mwa watumishi wa Mamlaka na kuteua waangalizi wa uvuvi kutoka kwenye Mamlaka au nje ya Mamlaka. Kwa hali ilivyo sasa, aya (n) inamtaka Mkurugenzi Mkuu kuteua maafisa hao kutoka miongoni mwa maafisa wa Mamlaka pekee. Hivyo, madhumuni ya marekebisho haya ni kupanua wigo wa uteuzi ili

kuwezesha watu ambao sio maafisa wa Mamlaka kuteuliwa kuwa waangalizi wa uvuvi kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 35 ili kuweka masharti yanayoanzisha kosa la kujihusisha na shughuli zozote za uvuvi wa bahari kuu bila kibali halali. Kwa sasa, Sheria inakataza kufanya shughuli za uvuvi bila kibali halali lakini haijaweka sharti linaloanzisha kosa kutokana na kukiuka masharti hayo. Sambamba na marekebisho ya kifungu cha 35, Jedwali la Pili linarekebishwa ili kujumuisha katika orodha ya makosa na adhabu, kosa jipya lililoundwa chini ya mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 35, ambapo kiwango cha juu cha faini kinachopendekezwa kutokana na kosa hilo ni dola za kimarekani milioni moja. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuimarisha utekelezaji (enforcement) kutokana na makosa hayo kufanywa mara kwa mara na hivyo kupelekea Serikali kupoteza mapato kutokana na kufanyika kwa shughuli za uvuvi wa bahari kuu bila vibali halali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura ya 123. Sheria hii ilitungwa mwaka 2010 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara kumi na tatu (13). Marekebisho yanapendekeza kurekebisha jumla ya vifungu kumi na mbili na vifungu vipya viwili vinapendekezwa kuongezwa. Vifungu vinavyopendekezwa kurekebishwa ni vifungu vya 4, 8, 27 F, 66, 73, 86A, 87, 88, 90A, 100C, 100D na 106. Aidha, vifungu vipya vinavyopendekezwa kuongezwa ni kifungu cha 5B na 271.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 4 cha Sheria ya Madini, Sura ya 123 kama ifuatavyo:

(a)Katika tafsiri ya msamiati "madini ya ujenzi" (industrial minerals), kwa kufuta neno "lime" na badala yake kuweka neno "limestone". Lengo la marekebisho haya ni kuondoa ukakasi uliojitokeza kwa

kuwa "lime" ni zao la madini ya "limestone" yanayochimbwa na hivyo neno hilo haliakisi maana iliyokusudiwa katika muktadha wa madini ya ujenzi yanayochimbwa;

(b)Katika tafsiri ya msamiati "kiapo cha uadilifu" (integrity pledge), kwa kufuta maneno "mineral right holder" na badala yake kuweka maneno "mineral rights holders, licenced dealers and licenced brokers" Marekebisho haya yana lengo la kuwajumuisha wafanyabiashara wa madini yaani "licenced dealers and licenced brokers" katika mawanda ya watu na taasisi zinazopaswa kuapa kiapo cha uadilifu. Kwa hali ilivyo sasa, wafanyabiashara wa madini hawana wajibu wowote wa kuapa kiapo hicho cha uadilifu katika tasnia ya madini;

(c) Katika tafsiri ya msamiati "madini ya nishati" (energy minerals), kwa kuongeza rasilimali za jotoardhi (geothermal) katika orodha ya madini ambayo yanatambuliwa chini ya Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kufanya madini ambata kama vile salfa, zebaki, lithium, helium na madini mengine ambayo ni rasilimali za jotoardhi ambayo hubeba nishati ya joto yaSimamiwe na Sheria kama madini ya nishati;

(d)Kwa kuongeza tafsiri mpya ya msamiati "rasilimali za jotoardhi" (geothermal resources). Lengo la kuongezwa kwa tafsiri hii ni kutoa ufafanuzi wa kina wa msamiati huo, hasa ikizingatiwa kwamba maneno "geothermal resources" yametumika pia katika tafsiri ya msamiati "madini ya nishati";

(e)Kwa kuongeza tafsiri mpya ya msamiati "mnada wa madini" (mineral auction). Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa msamiati huo ambao umetumika katika vifungu vya 87 na IOOC vinavyopendekezwa kurekebishwa na Muswada huu;

(f) Kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "gross value". Katika tafsiri mpya inayopendekezwa, maneno "refining or" yaliyokuwepo katika tafsiri ya zamani yameondolewa. Kuondolewa

kwa maneno hayo ni kutokana na kuwa utozaji wa mrabaha wakati wa usafishaji (refinery) unaathiri maduhuli ya Serikali ikilinganishwa na utozaji wa mrabaha kwa kuzingatia bei ya soko. Aidha, tafsiri hiyo inapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuiwianisha na tafsiri iliyopo kwenye kifungu cha 87(6) cha Sheria ambacho pia kimetoa tafsiri ya msamiati "gross value";

(g)Kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "uchenjuaji wa madini" ("mineral processing"). Msingi wa mapendekezo hayo ya marekebisho ni kutokana na kwamba tafsiri hiyo kama ilivyo sasa haijitoshelezi kwa kuwa haijumuishi shughuli nyingine muhimu (unit operations) katika uchenjuaji au usafishaji wa madini;

(h)Katika tafsiri ya msamiati "leseni ya kati ya uchimbaji madini" ("mining licence"), kwa kufuta tarakimu "US$ 100,000" na badala yake kuweka kuhakikisha utii wa Sheria. Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya cha 271 ili kuanzisha Maabara ya Madini ya Tume ya Madini. Lengo la marekebisho hayo ni kuirasimisha taasisi hiyo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa msingi wa sheria. Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 66 ili kuweka adhabu kwa mtu atakayeshindwa kulipa ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha utii wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 15 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 73 ili kutofautisha leseni za wafanyabiashara wa madini ya Tanzanite na wafanyabiashara wa madini ya Vito vingine vya rangi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka udhibiti wa madini ya Tanzanite kwa namna maalumu na kuyatangaza kwa kuzingatia uwepo wa madini hayo wa kipekee nchini Tanzania. Ibara ya 16 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 86A ili kuweka masharti kwamba muingizaji wa madini nchini hatatakiwa kulipa mirabaha kwa madini yanayoingizwa nchini endapo atathibitisha kuwa amelipa mirabaha katika nchi yalikotoka madini. Lengo la marekebisho haya ni kuepusha ulipaji wa mirabaha zaidi ya mara moja.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 87 kwa kuongeza viwango vya mirabaha inayopaswa kulipwa Serikalini na wafanyabiashara wa madini ya Vito yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi ambayo yamenunuliwa katika minada ya madini na maonyesho ya kimataifa ya madini ya Vito. Lengo la marekebisho haya kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka katika shughuli za madini. Ibara ya 18 ya Muswada ikisomwa pamoja na aya ya D ya Jedwali la Marekebisho inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 88 kwa kufuta maneno "has the meaning attributed to those words in subsection (6) of section 87 and that provision" kwa kuwa kifungu cha 87(6) kinachorejewa kimependekezwa kufutwa chini ya Ibara ya 17(b) ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 90A ili kuondoa masharti kuhusu ukaguzi kwa madini yanayouzwa wakati wa mnada wa madini unaosimamiwa na Serikali au unaotokana na maonesho ya kimataifa ya Vito. Lengo la marekebisho haya ni kuepusha gharama za minada kwa wafanyabiashara na kuongeza ushiriki wao katika mnada unaosimamiwa na Serikali. Ibara ya 20 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha IOOC ili kupunguza vikwazo kwa usafirishaji nje ya nchi Vito vya thamani vilivyouzwa na Serikali au katika maonesho ya kimataifa ya madini.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha IOOD ili kuruhusu biashara ya makinikia ndani ya nchi. Kwa sasa Sheria inazuia biashara ya makinikia ndani na nje ya nchi. Lengo la marekebisho haya ni kuvutia uwekezaji katika viwanda vya madini ghafi nchini. Ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 106 ili kuwataka wafanyabiashara wa madini walio na leseni na mawakala au madalali walio na leseni kuapa kiapo cha uadilifu. Lengo la kuhakikisha utii wa Sheria. Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya cha 271 ili kuanzisha Maabara ya Madini ya Tume ya Madini. Lengo la marekebisho hayo

ni kuirasimisha taasisi hiyo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa msingi wa sheria. Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 66 ili kuweka adhabu kwa mtu atakayeshindwa kulipa ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha utii wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 15 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 73 ili kutofautisha leseni za wafanyabiashara wa madini ya Tanzanite na wafanyabiashara wa madini ya Vito vingine vya rangi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka udhibiti wa madini ya Tanzanite kwa namna maalumu na kuyatangaza kwa kuzingatia uwepo wa madini hayo wa kipekee nchini Tanzania. Ibara ya 16 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 86A ili kuweka masharti kwamba muingizaji wa madini nchini hatatakiwa kulipa mirabaha kwa madini yanayoingizwa nchini endapo atathibitisha kuwa amelipa mirabaha katika nchi yalikotoka madini. Lengo la marekebisho haya ni kuepusha ulipaji wa mirabaha zaidi ya mara moja.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 87 kwa kuongeza viwango vya mirabaha inayopaswa kulipwa Serikalini na wafanyabiashara wa madini ya Vito yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi ambayo yamenunuliwa katika minada ya madini na maonyesho ya kimataifa ya madini ya Vito. Lengo la marekebisho haya tarakimu "US$ 5,000,000" Msingi wa mapendekezo haya ni kutokana na mwingiliano wa kiwango cha mtaji wa uwekezaji kati ya leseni ndogo ya uchimbaji wa madini (primary mining licence) na leseni ya kati ya uchimbaji wa madini (mining licence). Kwa mujibu wa Sheria ya Madini, Sura ya 123, leseni za uchimbaji wa madini zipo za aina tatu na zinazotofautishwa kwa kuzingatia viwango vya mtaji wa uwekezaji ambapo leseni ndogo ya uchimbaji wa madini mtaji wake ni kiasi chochote chini ya US$ 5,000,000; leseni ya kati ya uchimbaji wa madini mtaji wake ni kuanzia US$ 100,000 hadi US$ 100,000,000; na leseni kubwa ya uchimbaji wa madini mtaji wake unapaswa kuwa zaidi ya US$ 100,000,000. Hivyo, inapendekezwa kwamba

leseni ya kati ya uchimbaji wa madini mtaji wake uanzie US$ 5,000,000 ambao ni ukomo wa mtaji wa leseni ndogo ya uchimbaji wa madini, badala ya mtaji huo kuanzia US$ 100,000 kiwango ambacho kinaingiliana na kipo ndani ya wigo wa mtaji wa leseni ndogo ya uchimbaji wa madini;

(i) Katika tafsiri ya msamiati "processing area", kwa kufuta neno "milling" na badala yake kuweka neno "comminution". Msingi wa mapendekezo haya ni kwamba neno "milling" lililopo sasa halina utoshelevu kwa kuwa kitaalamu linaacha hatua nyingine za usagaji zikiwemo "crushing" na "grinding". Aidha, neno "comminution" kitaalamu linajumuisha "crushing", "milling" na "grinding".

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 ya Muswada ikisomwa pamoja na aya ya C ya Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 5B ili kumpa Waziri mamlaka ya kutangaza baadhi ya madini kuwa ya muhimu na ya kimkakati kwa Jamhuri ya Muungano, baada ya kupokea mapendekezo kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kutambua madini muhimu na ya kimkakati ili kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kudumisha usalama wa taifa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 1 1 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 8(1) kwa kuongeza aya mpya ya (c) ili kuweka ukomo wa muda kwa maombi ya kupewa haki ya madini pale mwombaji anaposhindwa kulipa ada ya maombi kuhusiana na eneo husika. Kwa hali ilivyo sasa, kwa kuwa maombi ya haki ya madini yanafanyika kwa njia ya mtandao, kumekuwepo na maombi mengi ya leseni za madini ambayo yapo kwenye masjala ya Tume ya Madini na kwamba Sheria ya Madini haijaweka masharti ya ukomo wa muda wa malipo na mamlaka ya kuondoa maombi hayo pale ambapo mwombaji anashindwa kulipa ada ya maombi kuhusiana na eneo husika. Vilevile, mrundikano wa maombi ambayo waombaji wake wameshindwa kulipa ada za maombi kwa muda mrefu pia kunazuia waombaji wengine kuomba eneo husika kutokana na kuwepo kwa maombi ambayo hayajalipiwa ada kwa

muda mrefu. Lengo la marekebisho ni kuhakikisha malipo ya ada ya maombi ya haki ya madini (mineral right) yanafanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 27 F ili kuweka adhabu kwa wamiliki wa haki za madini ambao wanatoa taarifa za uongo au zenye kupotosha au kushindwa kuwasilisha taarifa sahihi za madini. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha utii wa Sheria. Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya cha 27I ili kuanzisha Maabara ya Madini ya Tume ya Madini. Lengo la marekebisho hayo ni kuirasimisha taasisi hiyo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa msingi wa sheria. Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 66 ili kuweka adhabu kwa mtu atakayeshindwa kulipa ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika Sheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha utii wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 15 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 73 ili kutofautisha leseni za wafanyabiashara wa madini ya Tanzanite na wafanyabiashara wa madini ya Vito vingine vya rangi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka udhibiti wa madini ya Tanzanite kwa namna maalumu na kuyatangaza kwa kuzingatia uwepo wa madini hayo wa kipekee nchini Tanzania. Ibara ya 16 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 86A ili kuweka masharti kwamba muingizaji wa madini nchini hatatakiwa kulipa mirabaha kwa madini yanayoingizwa nchini endapo atathibitisha kuwa amelipa mirabaha katika nchi yalikotoka madini. Lengo la marekebisho haya ni kuepusha ulipaji wa mirabaha zaidi ya mara moja.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 87 kwa kuongeza viwango vya mirabaha inayopaswa kulipwa Serikalini na wafanyabiashara wa madini ya Vito yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi ambayo yamenunuliwa katika minada ya madini na maonyesho ya kimataifa ya madini ya Vito. Lengo la marekebisho haya kuongeza wigo wa

ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutoka katika shughuli za madini. Ibara ya 18 ya Muswada ikisomwa pamoja na aya ya D ya Jedwali la Marekebisho inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 88 kwa kufuta maneno "has the meaning attributed to those words in subsection (6) of section 87 and that provision" kwa kuwa kifungu cha 87(6) kinachorejewa kimependekezwa kufutwa chini ya Ibara ya 17(b) ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 90A ili kuondoa masharti kuhusu ukaguzi kwa madini yanayouzwa wakati wa mnada wa madini unaosimamiwa na Serikali au unaotokana na maonesho ya kimataifa ya Vito. Lengo la marekebisho haya ni kuepusha gharama za minada kwa wafanyabiashara na kuongeza ushiriki wao katika mnada unaosimamiwa na Serikali. Ibara ya 20 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha IOOC ili kupunguza vikwazo kwa usafirishaji nje ya nchi Vito vya thamani vilivyouzwa na Serikali au katika maonesho ya kimataifa ya madini.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha IOOD ili kuruhusu biashara ya makinikia ndani ya nchi. Kwa sasa Sheria inazuia biashara ya makinikia ndani na nje ya nchi. Lengo la marekebisho haya kuvutia uwekezaji katika viwanda vya madini ghafi nchini. Ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 106 ili kuwataka wafanyabiashara wa madini walio na leseni na mawakala au madalali walio na leseni kuapa kiapo cha uadilifu. Lengo la marekebisho haya ni kudumisha viwango vya maadili, uaminifu na uadilifu katika shughuli za madini pamoja na kuzingatia Sheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne na ya mwisho ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura ya 280. Sheria hii iliyotungwa mwaka 2016 haijawahi kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 24 ya Muswada ikisomwa pamoja na aya ya E ya Jedwali la Marekebisho inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 21 ili kuongeza maneno ya nyongeza mwishoni mwa kifungu hicho yanayoweka bayana kwamba ukiukaji wowote wa masharti yaliyoainishwa katika aya (a) na (b) unaweza kufanya kibali cha utafiti kusitishwa. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuhakikisha watafiti wote wa masuala ya uvuvi wanazingatia masharti ya Sheria kuhusiana na tafiti wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 25 na ya mwisho ya Muswada inapendekeza kufuta kifungu cha 24 cha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura ya 280 kwa kuwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Uvuvi yanakinzana na mamlaka yaliyotolewa kwa Bodi. Lengo la marekebisho haya ni kuepusha mgongano wa mamlaka na kuiwezesha Sheria itekelezeke kwa urahisi na ufanisi.
Mheshimiwa Spika, Kabla ya kuhitimisha hoja yangu, niruhusu nitumie fursa hii kuishukuru familia yangu, mke wangu Neema Grace, binti zangu Tamika na Saritha pamoja na kijana wangu Reefat kwa kuwa nami katika kila hatua ya utumishi wangu hadi hatua hii niliyofika. Hakika, uwepo wao una mchango mkubwa katika mafanikio yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024) kama ulivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa spika, NAOMBA KUTOA HOJA.

Hamza S. Johari (Mb.),
MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI
02 Septemba, 2024

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. Kwa niaba yake Mheshimiwa Zedi. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI J. ZEDI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Nne, Kikao cha Kumi na Tatu kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 15 Februari, 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia Katiba, sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya

aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Eliezer Mbuki Feleshi, kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya wadau. Mnamo tarehe 22 Agosti, 2024 Kamati ilikutana na Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbnge na Waziri wa Katiba na Sheria ambaye alijibu na kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba, Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Muswada, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]* ukiwa umegawanyika katika sehemu nne na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tatu kwa madhumuni ya kuondoa upungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni kama ifuatavyo: -

(a) Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Maeneo ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 *(The Deep-Sea Fisheries Management and Development Act (CAP 388);*

(b) Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 *(The Mining Act (CAP. 123);* na

(c) Marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura 280 *(The Tanzania Fisheries Research Institute Act [CAP280])*.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi, inayojumuisha Ibara ya Kwanza inayohusu jina fupi na Ibara ya Pili inayoelezea marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu, pamoja na maelezo ya Serikali, Kamati ilibaini changamoto au upungufu katika sheria mbili kati ya sheria tatu zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Maeneo ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 *(The Deep-Sea Fisheries Management and Development Act (CAP 388)*. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya Nne hadi Ibara ya Saba ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Marekebisho kwenye sheria hii kwa ujumla wake yanalenga kuondoa ombwe lililopo sasa kuhusiana na mamlaka ya uteuzi na muda wa Wajumbe kushikilia wadhifa huo kwenye Kamati ya wataalamu ya ushauri, kutanua wigo wa uteuzi kwa kujumuisha watu ambao sio maafisa wa uangalizi na kuteuliwa kufanya kazi hizo kama wana sifa na vigezo vinavyomwezesha mtu kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, marekebisho haya yanapendekeza kuanzisha kosa la kujihusisha na shughuli za uvuvi bila leseni. Lengo la pendekezo hili ni kusaidia kuzuia vitedo vya uvuvi haramu kwenye Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Nne inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 11 cha sheria kwa kuongeza vifungu vidogo vya (3) na (4) ili kuanzisha Mamlaka ya Uteuzi wa Wajumbe wa Kamati ya

Ushauri ya Wataalamu walioainishwa katika aya (c), (d), (e), na (f) ya sheria. Waziri anayehusika na masuala ya uvuvi anapewa mamlaka ya kuwateua wajumbe hao baada ya kushauriana na waziri anayehusika na masuala ya uvuvi wa Tanzania -Zanzibar. Ibara pia inaweka ukomo wa Wajumbe wa Kamati kukaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja. Wajumbe wa Kamati hiyo wanaopedekezwa kuteuliwa na Waziri wametajwa katika Muswada kuwa ni hawa wafuatao: -

(a) Mawakili wa Serikali Waandamizi wawili kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mmoja kutoka kila upande wa Muungano;

(b) Wachumi wawili wenye ujuzi wa masula ya uvuvi, mmoja kutoka kila upande wa Muungano;

(c) Watafiti wawili katika sayansi ya bahari kutoka katika taasisi za utafiti, mmoja kutoka kila upande wa Muungano; na

(d) Wanachama wawili wenye ujuzi na uzoefu katika sekta ya uvuvi, mmoja kutoka kila upande wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho ni kuondoa ombwe lililopo sasa kuhusu mamlaka ya uteuzi na muda wa wajumbe kukaa madarakani.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 *(The Mining Act (CAP. 123)*. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya Nane hadi Ibara ya 21 ya Muswada.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, marekebisho haya kwa ujumla yanalenga kuboresha tafsiri za misamiati iliyotumika kwenye sheria hii, kutoa mamlaka ya Waziri mwenye dhamana

kutangaza baadhi ya madini kuwa ni ya kimkakati kwa lengo la kulinda rasilimali hizo na kudumisha usalama wa Taifa, kutoa ukomo wa muda wa kuomba leseni kwenye mfumo na kutoa adhabu kwa wamiliki wa haki za madini wanaotoa taarifa za uongo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 5B katika sheria ili kumpa Waziri mamlaka kwa amri atakayoitangaza katika Gazeti la Serikali na baada ya idhini ya Baraza la Mawaziri kutangaza baadhi ya madini kuwa ni ya muhimu na ni ya kimkakati. Hatua hiyo inatekelezwa baada ya Waziri kupokea mapendekezo kutoka Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kutambua madini muhimu na ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwenye maeneo yafuatayo: -

(i) Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya *388 [The Deep-Sea Fisheries Management and Development Act (CAP 388)];* na

(ii) Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 *[The Mining Act (CAP. 123)]* ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ibara ya Nne ya Muswada, Kamati iliishauri Serikali kufanya rejea sahihi katika kifungu kidogo cha (4) kwani kifungu kidogo cha (2) kilichorejewa katika ibara hiyo kimekosewa na ilipaswa kurejewa kifungu kidogo cha (1) kwa kuwa Wajumbe wa Kamati ya Wataalam wametamkwa katika kifungu kidogo cha (1) na siyo cha (2). Tunaipongeza Serikali kwa kukubali

ushauri wa Kamati na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri ambao Kamati imeutoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 *(The Mining Act (CAP. 123)*. Ibara ya 10 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 5B kinachohusu Waziri kutangaza madini muhimu na ya kimkakati. Kamati iliishauri Serikali kuboresha kwa tafsiri ya maneno *strategic minerals* yenye maana ya *mineral resources with diplomatic or defense importance* na badala yake isomeke *"Strategic minerals refer to minerals that are of critical importance to a Nation's economy."* Lengo ni kuboresha mawanda ya pendekezo la tafsiri kwenye Muswada. Hapa pia tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba nitambue majina ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hii na naomba yaingizwe katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Hamza Johari, Mbunge, na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi hiyo. Kamati inamwahidi ushirikiano uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiupekee Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Jaji Eliezer Mbuki Feleshi kwa kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania. Kamati pia inamshukuru kwa ushirikiano alioutoa kwa Kamati kwa Kipindi chote alichohudumu katika nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J.

Mwihambi, *ndc,* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msimamo wa Kamati kuhusu hoja, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya Kamati, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI WA MWAKA 2024 *[THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) BILL, 2024]* – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

### Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na nne, kikao cha kumi na tatu kwenye Bunge la 12, tarehe 15 Februari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha

Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina.

Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya aliyekua Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Eliezer Mbuki Feleshi (Mb) kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mikutano wa Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearings*) kwa siku mbili kuanzia tarehe 15 hadi 16 Agosti 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka wadau mbalimbali ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Kipekee Niwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya Wadau. Mnamo tarehe 22 Agosti, 2024 Kamati ilikutana na Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria ambae alijibu na kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]* ukiwa umegawanyika katika sehemu nne (4) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tatu (3) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

a) Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 (The Deep Sea Fisheries Management and Development Act (CAP 388);

b) Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 (The Mining Act (CAP. 123); na

c) Marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura 280 (The Tanzania Fisheries Research Institute Act [CAP280]).

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi, inayojumuisha **Ibara ya 1** inayohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoelezea marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika sheria mbalimbali.

## 2.2 Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Serikali, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria mbili kati ya sheria tatu zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

**2.2.1Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 The Deep-Sea Fisheries Management and Development Act (CAP 388).** Marekebisho hayo yanayofafanuliwa katika Ibara ya 4 hadi Ibara ya 7 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Marekebisho kwenye Sheria hii kwa ujumla wake yanalenga kuondoa ombwe lililopo sasa kuhusiana na mamlaka ya uteuzi na muda wa wajumbe kushikilia wadhifa huo kwenye kamati ya wataalamu ya ushauri, kutanua wigo wa uteuzi, kwa kujumuisha watu ambao sio maafisa wa Uangalizi kuteuliwa kufanya kazi hizo kama wana sifa na vigezo vinavyomuwezesha mtu kufanya kazi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile marekebisho haya yanapendekeza kuanzisha kosa la kujihusisha na shughuli za uvuvi bila leseni, lengo la pendekezo hili ni kusaidia kuzuia vitedo vya uvuvi haramu kwenye bahari kuu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 4 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 11 cha sheria kwa kuongeza vifungu vidogo vya (3) na (4) ili kuanisha mamlaka ya uteuzi wa Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Wataalamu walioainishwa katika aya (c), (d), (e), na (f) ya Sheria. Waziri anayehusika na Masuala ya Uvuvi anapewa mamlaka ya kuwateua wajumbe hao baada ya kushauriana na Waziri anayehusika na masuala ya Uvuvi Tanzania Zanzibar.

Ibara pia inaweka ukomo wa Wajumbe wa Kamati kukaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu, na wanaweza kuteuliwa

tena kwa kipindi kingine kimoja. Wajumbe wa kamati hiyo wanaopedekezwa kuteuliwa na Waziri wametajwa katika Muswada kuwa ni : -

(a) Mawakili wa Serikali Waandamizi wawili kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mmoja kutoka kila upande wa Muungano;

(b) Wachumi wawili wenye ujuzi wa masula ya Uvuvi, mmoja kutoka kila upande wa Muungano;

(c) Watafiti wawili katika Sayansi ya Bahari kutoka katika taasisi za utafiti, mmoja kutoka kila upande wa Muungano; na

(d) Wanachama wawili wenye ujuzi na uzoefu katika sekta ya uvuvi, mmoja kutoka kila upande wa Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la marekebisho ni kuondoa ombwe lililopo sasa kuhusu mamlaka ya uteuzi na muda wa wajumbe kukaa madarakani.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 (The Mining Act (CAP. 123)**. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 8 hadi Ibara ya 21 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Marekebisho kwa ujumla yanalenga Kuboresha tafsiri za misamiati iliyotumika kwenye sheria hii, kutoa mamlaka ya Waziri mwenye dhamna kutangaza baadhi ya madini kuwa ni ya kimkakati kwa lengo la kulinda rasilimali hizo na kudumisha usalama wa Taifa, kutoa ukomo wa muda wa kuomba leseni kwenye mfumo na kutoa adhabu kwa wamiliki wa haki za madini watakaotoa taarifa za uongo.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 10 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 5B katika Sheria ili kumpa Waziri mamlaka kwa amri

atakayoitangaza katika *Gazeti la Serikali*, na baada ya idhini ya Baraza la Mawaziri kutangaza baadhi ya madini kuwa ya muhimu na ya kimkakati. Hatua hiyo itatekelezwa baada ya Waziri kupokea mapendekezo kutoka taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kutambua madini muhimu na ya kimkakati.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwenye maeneo yafuatayo: -

**3.2 Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 The Deep-Sea Fisheries Management and Development Act (CAP 388)** na **Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 (The Mining Act (CAP. 123)** ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 4 ya Muswada Kamati iliishauri Serikali kufanya rejea sahihi katika kifungu kidogo cha (4) kwani kifungu kidogo cha (2) kilichorejewa katika ibara hiyo kimekosewa na ilipaswa kurejewa kifungu kidogo cha (1) kwakuwa Wajumbe wa kamati ya wataalam wametamkwa katika kifungu kidogo cha (1) na sio cha (2). Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.3 Marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura 123 (The Mining Act (CAP. 123).

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 10 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 5B kinachohusu Waziri kutangaza madini muhimu na ya kimkakati. Kamati iliishauri Serikali kuboresha kwa tafsiri ya maneno "*strategic minerals*" yenye maana ya "*mineral resources with diplomatic or defence importance*" na badala yake isomeke "*Strategic minerals" refer to minerals that are of critical importance to a nation's economy*, Lengo ni kuboresha mawanda ya pendekezo la tafsiri kwenye Muswada. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

## 4.0 HITIMISHO

### 3.4 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb | - | **M/ Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Boniphace NyanginduButondo,Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Omar Issa Kombo, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb | - | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. | Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, | - | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb | - | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Hamza Johari (Mb) Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kushika nafasi hiyo, Kamati inamuahidi ushirikiano uliotukuka.

**Mheshimiwa Spika**, kiupekee Kamati inampongeza Mhe. Dkt. Jaji Eliezer Mbuki Feleshi kwa kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Kamati pia inamshukuru kwa ushirikiano alioutoa kwa Kamati kwa Kipindi chote alichohudumu katika nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 3.5 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya Kamati naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
2 Septemba, 2024

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi, ahsante sana kwa wasilisho hilo kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wetu, baada ya kusikiliza hoja upande wa Serikali na kusikiliza maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge juu ya hoja zote mbili, tutaanza uchangiaji tutakaporejea jioni.

Waheshimiwa Wabunge, ambao tutaanza nao kuchangia tutakaporejea ni Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mheshimiwa Edward Olelekaita na Wabunge wengine tutaendelea kuwataja kadiri muda utakavyokwenda.

Baada ya kusema hayo, wageni wetu mliopo kwenye majukwaa huko karibuni sana Bungeni. Tangazo lenu sijaletewa hapa mbele, lakini ninaamini mmetembelea Bunge na tumefurahi kuwaona. Karibuni sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni leo. *(Makofi)*

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption Amendment Bill, 2024)***

**na**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya Mwaka 2024 *(The Written Laws [Miscellaneous Amendment] Bill, 2024)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, jiandae Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Neema Kichiki.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii nami nichangie Miswada miwili ambayo iko mbele yetu; Muswada ulioletwa na Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ambao umeletwa na Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria asubuhi ya leo katika Bunge lako Tukufu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ni miongoni mwa vitu ambavyo Mheshimiwa Rais wetu wa kwanza Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alivikemea kwa nguvu sana. Akafika hatua ya kusema kwamba miongoni mwa maadui ambao wangeongezwa katika Maadui watatu wa Taifa amba oni ujinga, maradhi na

umaskini, alikuwa anatarajia kuiongeza rushwa miongoni mwa maadui wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, alizungumzia rushwa mwaka 1958 katika Baraza la Kutunga Sheria la Mkoloni, wakati huo yeye akiwa Kiongozi wa Upinzani katika Bunge lile. Aliizungumzia rushwa kwa hisia kali na leo hii tunaonyesha namna ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita inachukua hatua kubwa katika suala zima la udhibiti wa rushwa katika kutenda haki na katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Serikali kwa viongozi ambao wamepewa dhamana na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utunzi wa sheria unatakiwa usiache ombwe kubwa katika kutoa nafasi ya rushwa, lakini tuimarishe utunzi wa sheria mbalimbali zikiwemo hizi ambazo tumeletewa hapa. Katika Sheria hii ya Rushwa Ibara ya Tano ambayo inarekebisha Kifungu cha 10 cha Sheria, inataja namna ambapo Afisa wa Taasisi hii ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa atamwita mtu yeyote, akikaidi atakumbana na adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliona jambo hili ni zuri, lakini pia kuwe na mwanya wa kuonyesha kwamba kuna Maafisa wengine wanaweza kuitwa, kuna mtu anaweza kuitwa na Afisa au kuwasilisha nyaraka kwa sababu pengine nafasi yake ni ndogo. Kuna Afisa Masuuli ambaye anawajibika na hiyo nyaraka au Afisa mwenye dhamana. Mfano, ikiitwa hapa katika taasisi ya hii Bunge, mwenye mamlaka ya nyaraka zote ni Katibu wa Bunge. Kwa hiyo, anaweza akaitwa Afisa ambaye yuko chini hapa, kwa hiyo, kuwe na sababu ambazo zinasababisha mtu asipeleke nyaraka hii kwa sababu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumeishawishi Serikali na imekubali kwamba kuwe na sababu ambazo zinaweza kuwa na *exemption* kwamba akiitwa mtu kupeleka nyaraka kuwe na sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 ambayo inarekebisha Kifungu cha 25 cha Sheria ya Rushwa, ambacho kimekuja na hisia mbalimbali na wadau wengi tuliwapokea katika Kamati waliona kwamba Kifungu (b) ambacho kilikuwa kinaongezwa katika marekebisho ya sheria hii, kimekubaliwa kiondolewe kwa sababu hizo, kwamba kilikuwa na ombwe ya wale wanaoshawishi ambao tunajua kumekuwa na changamoto nyingi hasa katika vyuo vyetu vikuu, na watu wanaoomba ajira. Wengi wamekuwa na ushawishi mbaya, lakini tumeona wale wenye mamlaka walinde viapo vyao, walinde thamani ya kazi waliyopewa na pia waheshimu nafasi zao, wasiingie katika mitego hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumekubaliana na Serikali kuwa kifungu hiki cha (b) kitolewe kwa sababu ya kuhakikisha jamii inakuwa salama kwa upande mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na ni wazi kwamba mtoaji rushwa na mpokea rushwa wote mbele ya sheria ni watu ambao wanapaswa kuwajibika. Tumeona wale wenye mamlaka walinde nafasi zao ili ombwe hili la huko mtaani liweze kutuepuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 15 inarekebisha Sheria Mama Ibara ya 43(3), mali ambazo zinapatikana kwa njia ya rushwa zilikuwa zipelekwe kwa Msajili wa Hazina, lakini sasa kutokana na mabadiliko haya ya sheria ambayo yamekuja hapa katikati katika Bunge hili, Msajili wa Hazina sasa hayuko katika Wizara ya Fedha, yuko katika Wizara ya Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, moja kwa moja mwenye dhamana ya mali ambazo zinakamatwa abaki kuwa Katibu Mkuu ambaye ni Afisa Masuuli. Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha abaki kuzihodhi zile mali ambazo zitapatikana na rushwa, kwa maana ya Serikali. Zamani ilikuwa Msajili wa Hazina ndiyo alikuwa anazitunza, sasa kwa sababu Msajili wa Hazina kaondolewa katika Wizara ya Fedha, kapelekwa katika Wizara ya Mipango na Uwekezaji, basi

sasa Katibu Mkuu na Kamati tumekubaliana hili kwamba Katibu Mkuu ndiyo awe na dhamana hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, kuna mambo mengi yameguswa. Mimi nitachangia jambo dogo tu. Ibara ya Tisa inaenda kurekebisha Sheria Mama ya Madini Na. 123 inarekebisha Kifungu cha 126 ambapo inaeleza kwamba, zamani ilikuwa mtu mwenye leseni ya kati alikuwa anaweza angalau kuanzia dola 100,000/=. Kwa hiyo, sasa wamekuja vizuri, leseni ya kati maana yake ni watu ambao wana nguvu kubwa ya uchumi, kwa maana ya *Mining License*, waweze kuanza na angalu dola milioni tano. Kwa hiyo, hii tunakubaliana ni wazo zuri na ninaomba Bunge lako hili Tukufu likubali, na ninalishawishi likubali kupitisha marekebisho haya mawili ya Sheria ya TAKUKURU na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi, ninaunga mkono hoja ya Kamati, na pia naunga mkono hoja ya Serikali na marekebisho yake na Bunge lako likubali kupitisha na kuwa sheria ambazo zitapitishwa na Bunge hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Kimei, jiandae Mheshimiwa Neema.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa. Naomba nianze kwa kumpongeza Rais wetu kwa kuleta sheria hii ambayo ni Sheria ya Kimataifa. Kusema ukweli ni mambo ya kupambana na ugaidi au kupambana na rushwa, ni mambo ya Kimataifa na yanatakiwa yazingatie viwango vya Kimataifa ambavyo vimekubalika kwenye mashirika yetu ya Kimataifa, *United Nations* na mahali pengine. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa kuleta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri wa Utawala Bora na Utumishi kwa kuleta na kuiwasilisha vizuri Sheria hii ya Kupambana

na Kuzuia Rushwa. Kabla sijaendelea zaidi, pengine ingekuwa ni sahihi kuwapongeza Mawaziri wote wapya waliochaguliwa na Mheshimiwa Rais, ni Mawaziri Wazuri, tunawaombea Mungu na wale waliobadilishwa Wizara zao, nao pia tunajua kwamba Mheshimiwa Rais ameona kwamba wanaweza wakatumika vizuri zaidi kwenye maeneo ambayo amewapeleka. Kwa hiyo, nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mwanasheria Mkuu kwa kuwasilisha vizuri hili wasilisho la Marekebisho kwenye sheria nyingine ndogo ndogo. Nakushukuru na wewe kwa jinsi ambavyo unatuendesha, unatuongozea Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema hivi kwamba, dhana ya Sheria ya Kupambana na Kuzuia Rushwa nchini ni kuwafanya wananchi waogope, wajue kwamba wakijiingiza kwenye masuala yoyote ya rushwa, kwenye mnyororo wowote unaowapelekea rushwa, watachukuliwa hatua nzito ambazo zitawafanya wajute, pia zinawaingiza kwenye uwoga kwamba nisifanye. Ndiyo maana inasema ni kupambana na kuzuia.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi sheria hii siyo kwamba ni kuadhibu, ni kuhakikisha kwamba hivyo vitu havitokei. Kwa sababu, *by the time* vinakuja kutokea, nchi inakuwa imejiingiza kwenye hasara kubwa, kupoteza thamani ya fedha inayoenda kwenye miradi na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasikitika kwamba kusema kweli ili watu waogope lazima waone kwamba sheria ile na vile vigezo vilivyoko kisheria vinatumika kuwaadhibu na kwamba kuna ukweli watu wanashikwa na wanafungwa, wanatozwa na hata kama ikilazimika sheria iwe imeweka viwango vikubwa vya adhabu, kwa sababu kigezo cha kuogopa sheria pia ni kiwango cha adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisema hapa unaenda kumfunga mtu miaka miwili, siyo adhabu ambayo inatisha sana. Miaka mitatu

haitishi, miaka mitano haitishi, miaka inayotisha ni miaka 30 lakini inayotisha zaidi ni kifo. Tukisema kwamba mtu ukishikwa umejiingiza kwenye rushwa unaenda kuuawa, kuna nchi zimefanya hivyo, nafikiri kama *China*, ukishikwa mtuhumiwa ni kifo. Kwa hiyo, watu waliogopa kabisa, sasa hii kupambana kwetu unaona kunaishia chini huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba ile taasisi yetu TAKUKURU katika miaka yote hii kuna mambo mengi yametokea, lakini sijasikia mtu amepelekwa Mahakamani au sijasikia mtu amechunguzwa kwa sababu ameonekana anajilimbikizia mali kwa wingi na haijulikani kwamba anapata wapi hizo fedha kwa sababu tunajua kiwango chake cha mshahara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu vinatokea, lakini hatuoni kinachotokea. Kwa hiyo, mwananchi ataogopa nini? Hata ukibadilisha hii sheria leo, kama hakuna kitakachotokea, mtu atajua aah, hata nikifanya, pengine ile ile hela ambayo nimepata rushwa ndiyo nitaitumia hiyo hiyo hela kuniokoa. Kwa hiyo, inakuwa haitishi.

Mhehsimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba, kitu cha kwanza ambacho sheria inatakiwa ije i-*address* na iangalie ni viwango na watu kuona kwamba kweli ile taasisi inayoshughulika inafanya kazi yake na adhabu zinatolewa na hizo adhabu zinatisha. Kwa hiyo, naomba wenzetu wa TAKUKURU waanze sasa kuwa wakali, waanze kushughulika wakijua kwamba wanalinda maslahi ya nchi hii na ndiyo njia pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba, kwa mfano miaka yote hii ambayo hatujasikia toka waanzishe ile Mahakama inayoitwa ya Mafisadi, ile Mahakama sijui imeishia wapi sasa. Hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *issue* inayotokea ni kwamba, kama watu hawajasikia wanasema, hakuna kitu bwana. Wanaendelea tu kama *business as usual.* Aidha, watuambie kwamba hakuna rushwa,

rushwa imepungua sana, lakini mimi nitasita kukubali kwani rushwa ipo, inaendelea na tunawajua watu wetu. *CAG* anaonyesha mifano mingi au matukio mengi ambayo unaweza ukayahusisha na rushwa, lakini pia wale wa nje wanaotutathmini sisi watasema hii nchi iko juu sana kwa kiwango cha rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tuchukue hilo na tujaribu kulifanyia kazi na kwamba hata kwenye huu Muswada ambao marekebisho yanakuja, tunaona adhabu ime-*range* kati ya shilingi milioni tatu mpaka 20 *maximum*, ndiyo ninaona huko, hamna mtu anayetozwa shilingi milioni 100, hamna. Halafu isipokuwa ile *advantage* wanasema ni *value advantage* lakini ukweli ni kwamba, vifungo navyo ndiyo hivyo miaka miwili mpaka miaka 10 sana sana. Kwa hiyo, hiyo bado haijawa na makali ambayo yanastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri watu waelewe kwamba, mtu anapokuja kushikwa kwamba amepokea rushwa au ametenda vitendo vya rushwa ya ngono, ni kwamba anakuwa ameshatenda mara nyingi, yaani unamshika mara moja lakini akiwa mtu ana hiyo tabia, kwa sababu rushwa ni tabia, kwa hiyo, mtu ameianza siku nyingi, halafu siku anayoshikwa ni siku ya 40 ndiyo anakamatwa. Kwa hiyo, basi ahesabiwe kwamba huyu mtu tumemshika, lakini amechukua nyingi kiasi gani katika kipindi hiki cha miaka hiyo 40, au miezi 40 au siku 40 au miamala 40. Kwa hiyo, atozwe na aadhibiwe kwa kusema *okay*, tumekushika kwa hili, lakini wewe tabia yako ilikuwa ni hii na kama kweli ni mtu ambaye amechukua rushwa ya ngono, basi atakuwa ametembea na wanawake 40 akawapa vyeo. Kwa hiyo, naomba sana turudie kwenye hiyo ili tuweze kufanya kitu ambacho kitatusaidia kuogopesha watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana sana na wale wanamtandao wanaopinga rushwa ya ngono. Wamesema huwezi kulinganisha yule mwanamke ambaye ameshawishiwa kutoa rushwa ya ngono ukasema naye ana dhambi. Kwa hiyo, naye lazima aingizwe kwenye ule mtego.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hivi, unajua ni kama binadamu. Sisi binadamu ni *subjects* wa shetani. Shetani anakuja anatushawishi kila siku, anataka tufanye dhambi. Sasa sisi tuna maamuzi ya kusema tunataka tufanye ile dhambi au tusifanye. Kama tukienda na ushawishi wa shetani, mtu anayepata dhambi siyo shetani, ni wewe. Sasa, wewe ndio mwenye mamlaka, umemshawishi au haujamshawishi mwanamke au mwanaume *the other way round* ukafaya mambo hayo, ina maana kweli kwamba hatuwezi kumhusisha yule ambaye ameshawishiwa? Yule aliyeshawishi hatuwezi kumwingiza kwenye mtego. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, shetani anabaki hana dhambi, wewe unabaki una dhambi na kwa hiyo, *subject* ni mwenye mamlaka na mtu anayetakiwa ashtakiwe ni yule mwenye mamlaka, siyo yule ambaye amelazimishwa au amefanya kwa namna ile, anajikuta kwamba amejiingiza kwenye haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri hivi, ili kuweza kuonyesha ni kitu gani kinafanyika kwenye suala zima la rushwa, tujaribu kuomba mamlaka. Ile Ripoti ya TAKUKURU inayokwenda kwake ya mwaka kama ile ya *CAG*, basi ije kwenye Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili waijadili na waonyeshe watu kwamba tunapokea na katika mwaka huu kuna kesi za namna hii za rushwa zimepatikana na watu wamepata adhabu hizi na Bunge tumesikia na watu wakaanikwa, kwa sababu ukifichaficha haisaidii kwenye mambo haya ya rushwa. Njia tu ya kupunguza ni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi kwenye Muswada, mimi ninafikiri kuna neno moja linaitwa *instrumentalities Section number seven na number eight* zipo na maeneo mengine kwenye Muswada huu imetumika, lakini kusema ukweli ni watu wachache wanaelewa *instrumentalities* hizo ni nini? Ni kitu gani? Kwa hiyo, tunaomba hiyo iwe *defined*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye maeneo mengine mengi tunaona kuna *issue* hii ya *advantage*; thamani ya *advantage*

ambayo mtu amepata kwamba, kama kwa mfano mtu umepandishwa cheo bila kustahili kwa sababu umetoa ngono, ina maana kwamba kuna *advantage*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo utai-*measure* namna gani na *advantage* ya mtu ambaye amepata cheo kwa kutumia rushwa ya ngono au kitu kama hicho? *How do you measure it*? Yaani inaacha mwanya mkubwa sana na *discretion* kubwa sana kwa yule Hakimu atakayeamua, yaani inampa *discretion* ambayo haina mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri pengine tujaribu zaidi ku-*define* hiyo *advantage* itakuwaje? Itakuwa kwa sababu kitu kama kile ambacho kusema kweli *advantage* uliyopata unaweza ukai-*measure* kwa mwaka mmoja, kwa mshahara wa mwaka mmoja ulioongezeka, unaweza uka-*measure* kwa miaka 10 ijayo ukafanya *net present value* ukasema wewe hii kazi uliongezewa cheo kwa sababu ulitumia ngono, basi unapiga *Net Present Value* ya lile ongezeko ambalo amepata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima uji-*define better* ili mtu ajue ni kitu gani unazungumza unaposema kwamba, ni thamani "*advantage*." Kwenye upande wa *election*, narukaruka kwa sababu, naona muda unakwenda. Upande wa *election,* wanasema ni rushwa kwenye *election,* kwenye chaguzi na wanasema *election* ni *process*. Hebu niambie *process* ya uchaguzi inaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kule majimboni kwetu wanapita watu wanashawishi watu kwamba wawe kwenye timu zao, wanahonga. Sasa *election process* haijaanza kwa sababu, tume haijatangaza. Sasa mtu huyo utamkamata kwa sheria hii, ni jambo gumu sana. Lazima u-*define process* ya uchaguzi inaanza lini na inaisha lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tungeomba ninyi wanasheria mwangalie, mweze ku-*define* kwa sababu, kweli

uchaguzi kabla mchakato haujatangazwa na tume kwamba unaanza unakuwa haujaanza, lakini watu wameanza, watu wanaanza mapema, wanatoa vishawishi vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo nimeliona hapa kwenye hii sheria ni kwamba ime-*define* vitu vingi, ila haijasema ile takrima. Zamani kulikuwa na mjadala ulipita Bungeni hapa, unatofautisha rushwa na takrima. Sasa kwenye hii takrima inaanzia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliitisha mkutano pale kwenye Jimbo langu la Vunjo, watu hawaji kama hawajui kwamba nitatoa mbege kidogo, wanaita kitochi. Kama hamna kile, utapata leo watu 200, kesho utapata watu 20. Kwa hiyo, lazima kuwe na hiyo takrima. Sasa watu wengine wanaogopa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani, nilivyokuwa nafanya kwenye mikutano yangu, nilikuwa naogopa kabisa kuwapa watu mbege kidogo au maji. Kuna wengine hawanywi. Kama wale waislamu kule kwenye upande wangu wa tambarare wao hawanywi, wanakunywa maji. Sasa ukiwapa maji, ukawapa mbege inakuwa mambo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini hamja-*define* vizuri huku ikaeleweka kwenye mambo yale…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kimei. Muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema, ajiandae Mheshimiwa Edward Olelekaita.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa ya kuchangia. Nami nitaelekeza mchango wangu kwenye Muswada huu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika eneo la rushwa ya ngono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo amekuwa mstari wa mbele kusemea na kukemea vitendo vya aina zote vya ukatili wa kijinsia, hususan, eneo hili la rushwa ya ngono ambapo amesema mara kadhaa katika mikutano tofauti kuhusiana na rushwa ya ngono maofisini, vyuoni na hata kwenye vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ya ngono ni lazima tutambue kwamba ni tofauti na biashara ya ngono. Kwa hiyo, tunapojadili rushwa ya ngono, hatupaswi kufungamanisha kana kwamba, nayo ni biashara ya ngono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu, kwa mfano kwenye nchi ya Finland wenyewe kwenye Sheria yao ya Biashara ya Ngono wanachofanya ni wanamwadhibu yule anayenunua ile biashara na siyo anayeuza. Kwa sababu, wanaamini ya kwamba, pale kwenye biashara, yule anayenunua ana uhuru na mamlaka ya maamuzi ya kununua au kutokununua. Kwa hiyo, ni kwa muktadha huo huo pia tunapojadili suala la rushwa ya ngono ni lazima tutambue na tutofautishe maeneo hayo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia muda, nitatoa tu kwa ufupi. Katika miaka ya 2000 mpaka 2007 Majaji wanawake walifanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa suala la rushwa ya ngono itatambulika na itawekwa katika sheria kwa kutambua utofauti wake. Hilo lilikuwa ni jambo la msingi kwa sababu, suala la rushwa ya ngono linaendana kabisa moja kwa moja na mahusiano ya matumizi mabaya ya mamlaka na ni kwa muktadha huo Kifungu cha 25 kikawekwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali mapendekezo ya Serikali ya kuleta kile kifungu kipya cha 10(b) ambacho sasa kilikuwa kinaweka viashiria vya kana kwamba yule ambaye ni mhanga ataadhibiwa na yule ambaye ni mhalifu, kwa maana ya mhalifu wa kutaka rushwa ya ngono atakuwa anapata upenyo wa kupewa ulinzi wa namna fulani. Kwa kufanya hivyo, tutambue ya kwamba, hiki kifungu kilikuwa kinakwenda kupokonya haki ya yule ambaye ni *victim*, haki ya mhanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba, Tanzania imesaini mikataba mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda, lakini vivyo hivyo siyo kila jambo ambalo ni la Kimataifa, sisi kama nchi, ni lazima tulifuate. Lazima pia, tuangalie mazingira ya nchi yetu, na ni kwa muktadha huo kupitia sisi kuwa na Kifungu cha 25, Tanzania imekuwa ni nchi ambayo imesifika na kutambulika duniani kwa kuwa na sheria mahususi kwenye eneo la rushwa ambayo inalinda haki za wanawake, haki za wasichana, haki za watoto wa kike pamoja na watoto wa kiume. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naipongeza sana Kamati kwa kazi kubwa iliyoifanya ya kuchakata eneo hili, kusikiliza maoni ya wadau mbalimbali na kuhakikisha ya kwamba Kifungu cha 25 kinabaki kwenye sheria kwa sababu mtu mwenye mamlaka anao wajibu, amekula kiapo cha kazi, amekula pia na kiapo cha maadili. Kwa hiyo, anapaswa ajiendeshe kwa kufuata msingi wa kile kiapo kulingana na nyadhifa ile aliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hapaswi yeye tena kupewa ulinzi wa kuhakikisha kwamba haingii kwenye mtego wa rushwa ya ngono. Ni kwa muktadha huo huo yeye mwenye mamlaka ndio anapaswa tuhakikishe ya kwamba, kila mtu mwenye mamlaka hatumii mamlaka yake vibaya, ya ama kushawishi ama kufanya watu ambao wanakuwa tayari ni *victim* wa mazingira, kwa maana ya *circumstance* zimewafanya wawe wahanga waweze

kujiingiza kwenye rushwa ya ngono, halafu sasa ghafla sheria hiyo hiyo iwe inamlinda yeye badala ya kumlinda mhanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakubaliana sana na Kamati na namna ambavyo Kamati imeshauri. Zuri zaidi ni kwamba, Kamati pia, imeshauri ile faini itoke kwenye faini ya shilingi milioni tano kwa maana ya ukomo mpaka shilingi milioni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, katika kifungo, itoke kwenye kifungo cha miaka mitatu hadi kifungo cha miaka 10, jambo hili ni la kupongeza kwa sababu, hii inaonesha namna gani ambavyo sasa, sisi kama Tanzania, tunaendelea kuhakikisha tunalinda maadili ya viongozi wote na tunalinda kwamba, mtu yoyote mwenye mamlaka, awe ni mwanaume, awe ni mwanamke asitumie mamlaka yake vibaya kusababisha kizazi chetu cha leo na cha kesho kuharibika kwa kupitia rushwa ya ngono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, naishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo imekuwa sikivu, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, hapa nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa George Simbachawene, pia nampongeze sana Mheshimiwa Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hata *Chief Whip* wetu, Mheshimiwa Lukuvi, kwa namna ambavyo wamepokea maoni ya Kamati, wamepokea maoni ya wabunge pamoja na maoni ya wadau wakayachakata, wakaona namna ya kufuta kile kifungu cha 25 na kuleta kifungu kile kilichokuwa kinapendekezwa 10(b) kilivyokuwa kinaleta tafsiri na mtazamo hasi kwamba, sasa tunataka kwenda kulinda wahalifu wa rushwa ya ngono  na kuadhibu wahanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia hayo, nawapongeza sana kwa namna ambavyo wamekuwa wasikivu. Ni kwa muktadha huo huo tuendelee kuhakikisha kwamba Serikali inakuwa mstari wa mbele kabla ya kuleta mapendekezo ndani ya Bunge kuyachakata na kuhakikisha kwamba hayana makandokando yoyote na

hayawezi kuleta taswira ambayo ina mkanganyiko, kama namna ambavyo kifungu hichi 10 (b) kilichokuwa kimeleta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, ninayo faraja kubwa sana kwamba, kwa kupitia uamuzi huu tunakwenda kuendeleza dira na dhima nzima ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kutokomeza vitendo vyote vya ukatili wa kijinsi, vya kulinda watoto wa kike, kulinda watoto wa kiume, kulinda wanawake na wanaume ili kuhakikisha kwamba pale ambapo kunakuwa na fursa, basi wote tupate fursa kwa haki na siyo kwa kuendeleza vitendo vya rushwa ya ngono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. Naunga mkono hoja kwa kufuatia mabadiliko hayo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Olelekaita, jiandae Mheshimiwa Mgalu, jiandae Mheshimiwa Kamani.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa mabadiliko haya yaliyopo mbele yetu. Ni sheria ambazo zinagusa haki na hisia za watu, kwa hiyo, tumpongeze kwa kuletea mabadiliko ya sheria hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Simbachawene na pia Mheshimiwa Naibu Waziri, tunampongeza sana kwa kuaminiwa na kuteuliwa. Pia nampongeza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu nzima, Mkurugenzi wa TAKUKURU, Katibu Mkuu na timu nzima ambayo imefanya kazi na Kamati ya Katiba na Sheria wakati wa mijadala kuhusu mabadiliko ya sheria hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Kamati, niseme tumepata nafasi ya kusikiliza wadau na kwa kweli tunapongeza wadau, wamekuja wengi sana kwenye Kamati yetu na tumejifunza mambo

mengi sana. Utungwaji wa Sheria ni mchakato, na kusikiliza wadau ni sehemu muhimu sana pia ya utungwaji wa sheria. Kwa hiyo, nawapongeza *Tanganyika Law Society* na wengine wote ambao walikuja kwenye Kamati yetu, tumejifunza mengi sana kutoka kwao na kwa kweli Kamati imenufaika kipindi hiki kusikiliza maoni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naipongeza Serikali, mijadala kati ya Kamati na Wizara kwa kweli yamekuwa ni *very impressive*. Tunazungumza kuwa ni mchakato, utungwaji wa Sheria ni *process,* lakini kila wakati tukipata jambo tukaona tuweke hivi, mmekuwa *very positive*. Kwa kweli, napongeza *Attorney General,* umekuwa *very quick* kuelewa *feelings* za Watanzania hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ni adui wa haki na tangu uhuru viongozi wetu wa Kitaifa, alivyosema Mheshimiwa Massare, Mwalimu Nyerere na viongozi wetu wa Kitaifa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, wote wamekuwa wakisisitiza madhara ya rushwa kwa Taifa letu na kwamba, kunyimwa haki kunaharibu jamii. Vilevile hasa wale waliopo madarakani na wale ambao wamepewa Madaraka na sheria wamekuwa *entrusted* na *power* ya *public* wakifanya vizuri kwa mujibu wa sheria, nadhani ndiyo kusudio hasa la Miswada hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa siyo rahisi sana, unajua hii ni Sheria ya Rushwa na Sheria ya Rushwa kama ilivyo kwenye Kifungu cha 15 cha Sheria yetu, misingi yake ni lazima kuna mpokeaji na kuna mtoaji, ndiyo *formula*, na ndiyo *standard*. Kwa hiyo, kila ukitaka kutengeneza Kifungu fulani cha Sheria ni lazima iende huko. Kwa hiyo, ndiyo maana haikuwa rahisi sana sasa kujadili rushwa inayoitwa ya ngono bila ku-*apply* ile *formula* ya mtoaji na mpokeaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi sheria inataka kuadhibu watu wote, anayetoa na anayepokea, lakini mazingira ni tofauti, inategemea sasa *focus* ni nini? *Focus* ya sheria ikiwa ni kumlinda mtoto, kwa mfano, tunaposema *rape* ama *statutory rape,* haijalishi kama mtoto akiwa ni *below 18* inakuwa ni *statutory rape* kwa

sababu, *whether* ame-*consent* au amefanya nini? Kwa sababu, mwelekeo na *focus* ya sheria ni kumlinda mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hiyo *offense* ya *sexual favor* ama ya rushwa ya ngono, baada ya kuleta haya mabadiliko madogo ya sheria, Kifungu kile cha 10, kinaleta mabadiliko Kifungu cha 25 cha Sheria ya Rushwa. Tulipokutana na wadau na baada ya mjadala mkubwa sana, ikaonekana ile (b) inalenga kumuumiza yule ambaye ni mhanga na baada ya kurejea sasa, Kifungu kile cha 25 ikawa *clear* kwamba, hapa huwezi ku-*apply* sheria ile ya mtoaji na mpokeaji, kwa sababu, hapa anayelengwa ni mtu mwenye madaraka fulani kwamba, sheria inapokupa mamlaka fulani kwamba, wewe ni Jaji, wewe ni Profesa chuoni, unasimamia misingi ya ufaulu na taratibu, sheria inakutaka ukae kwenye mstari, hata ungeletewa vishawishi vya namna gani, ndiyo *logic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hapa sisi tuna *logic* ya sheria Kifungu kile 25 ni kumzuia yule mwenye mamlaka asitumie mamlaka yake vibaya halafu akamshawishi mtu na mifano wakati wa mazungumzo ilikuja mingi sana, kama mbona sasa kuna wakati yule ambaye tunamwita *victim* ananishawishi? Sheria ya sasa kwa sababu, inamlenga yule mwenye madaraka pale ambapo ushawishi wa namna hiyo umekuja, *obligation* yako ni kusimama kwa mujibu wa sheria. Wewe ukisimama kwa mujibu wa sheria hutafungwa na kifungu hiki kwa sababu, wewe una madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kuchakata na kati ya mawasilisho tuliyopata na tumepata mengine mpaka nje ya nchi. *By the way* tukaja tukafarijika sana kwamba kumbe Kifungu cha 25 cha sheria ya sasa kinapongezwa sana na Tanzania imepongezwa sana kwamba kile kifungu kama kilivyo kilikuwa ni kizuri sana na nchi nyingine zilikuwa zinatamani kwenda njia ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya ile (b) ikaleta mtafaruku mkubwa sana, wengine wakawa wanasema, ibaki hivyo

hivyo, lakini baada ya Kamati hii kuangalia vizuri na kuangalia *feeling* za wale watu, kilichofanywa na Kamati kupitia ile *schedule of amendments* ambayo kwa kweli, Serikali imeshatoa *greenlight,* imeona kwamba, ni kitu kizuri pamoja na mazingira yote yale. Ni kwamba, Kamati imeangalia Kifungu kile cha 25 na tukagundua kwamba, pamoja na kwamba ni kizuri sana na inapongezwa sana duniani, lakini bado adhabu zile ni ndogo sana. Sheria ilikuwa haijaweka *minimum*, imesema tu kama ni faini isizidi shilingi milioni tano na kama ni kufungwa isizidi miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haijaweka *minimum,* kiwango cha chini, kwa hiyo, maana yake mtu angeweza kupigwa faini hata ya shilingi 500,000 kwa sababu, hakuna *minimum* na angeweza kufungwa hata miezi sita kwa sababu, sheria imesema ile *maximum* peke yake. Kwa hiyo, kilichofanywa na Kamati baada ya kupata *feeling* za wadau wale ni kujaribu na ni utungwaji mzuri wa sheria kusema *minimum* na kusema *maximum* nadhani pia tutakuwa tumeisaidia na Mahakama namna ya kutatua hiyo kesi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichofanya sasa Kamati ni kuweka *minimum* ya ile faini isiwe chini ya shilingi milioni mbili, lakini isizidi shilingi milioni 10. Kwa hiyo, imeongezeka na kifungo kisiwe chini ya miaka mitano, lakini isizidi miaka 10. Kwa hiyo, kwa kweli, kama ilivyo tu ilikuwa inapongezwa huko duniani, maana yake Mheshimiwa *Attorney General* na Mheshimiwa Waziri, hapa mmekwenda vizuri sana zaidi kwa sababu, *feeling* za wale watu ilikuwa ni kwamba, tufanyeje ili kumlinda huyu *victim?* Pia ilikuwa inaonekana labda faini na *convictions* zilizokuwa zinatolewa zilikuwa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini tukienda na hii ya Kamati ambayo tuna-*improve* ile *Section* 25 na kuongeza adhabu hizo nadhani ndiyo itakuwa bora tena zaidi kuliko zote. Kwa hiyo, kama Tanzania ilikuwa ni namba ya kadhaa hivi itakuwa imepanda tena juu zaidi kwa sababu ya *improvement* hiyo ambayo tumefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Kamati kwa jedwali hilo ambalo tumeleta tukasema hiki Kifungu cha 25 kikipita kama ilivyopendekezwa na Kamati, kwa kweli tutakuwa tumeondokana na zile changamoto ambazo tulikuwanazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine tunajua Taasisi ya Kupambana na Rushwa ipo kwenye mazingira magumu sana. Kuna wakati mwingine inakosa ku-*react* haraka kwa makosa yale ambayo yana-*involve* pesa nyingi sana, hasa hizi za mitandao. Tunajua *logic* ya kwa nini mmependekeza kifungu kile cha 38A.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano, kwa sababu sisi tulikuwa tunawaambia kifungu cha 38 kimeweka *a very elaborative process* ya kwenda Mahakamani kwa sababu ndiyo *good practice,* ninyi ni ofisi inayoangalia utawala bora na utawala bora ni kwenda kwenye taasisi nyingine kuondoa *powers* kwa mtu mmoja mmoja na kwenda kwenye taasisi kama ya Mahakama. Ndiyo *good practice* na ndiyo mantiki ya kifungu cha 38.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mantiki ya hii 38A tunaelewa kwamba pale ambapo kuna mazingira hayo ambayo *transactions* zinatokea *electronically* na ni *very fast* kwenda *the court process* inaweza ika-*delay* na ukashindwa kuzuia kile ambacho ulitaka kuzuia. Kwa hiyo, tunaelewa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano kupunguza zile siku, lakini hata wakati wa majadiliano, nilifurahi sana ninyi timu yenu mlikuwa mpo tayari kusema hata wiki moja, lakini tukasema kwa sababu ya *conformity* na sheria nyingine zilivyo maeneo mengine tukasema *fourteen days* ni *better*. Tunachotaka tu ni kwamba, sasa msikimbilie hii tu kwa sababu ipo, kwa sababu hii *intention* yake ilikuwa ni *for very difficult circumstances*, zile ambazo hamkuweza kwenda wakati hakukuwa na hiyo *option*. Kwa hiyo, nasi hatutegemei kwa sababu 38A ipo, basi mnakuwa mnatumia hiyo tu *all the time*, hiyo siyo *intention* ya Bunge kwamba kwenye

mazingira yale ambayo ni *special circumstances* mtumie hii na ionekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri wa sheria, haki ionekane ikitendeka, isiwe inatumika kama *loophole,* lakini kwa sababu ya *intention* ambayo imeonesha hata kwa kukubali siku saba, naamini kabisa kwamba kuna *intention* nzuri ya kufuata sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia asitokee mtu kwa sababu ya *loophole* ambayo ipo kwenye Sheria akafanya *transaction* ambayo ingeweza kuliumiza Taifa. Kwa hiyo, kwa kweli vifungu hivi viwili ni muhimu sana, nadhani itafanya Taasisi yetu ya Kupambana na Rushwa iwe *active* zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunataka rushwa ikome, rushwa ya kila aina, na *spirit* ni kwamba, unajua utungwaji wa sheria kila ikitokea jambo ambalo linaleta mtafaruku kwenye jamii kama ilivyo *sexual,* kwenye *advantage sexual* haikuwepo lakini mmeona tuweke, lakini baada ya mazungumzo yale tukafanya. Nia ni kwamba ikitokea mbinu nyingine mpya ya kirushwa rushwa wala msisite kuleta marekebisho ya sheria ili mtu asiende bila kuwa *punished. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sisi kwa kweli tunawatakieni kila la heri, mabadiliko haya yatawasaidia TAKUKURU na Serikali kupambana na rushwa na huo ndiyo msingi, ndiyo maana tupo hapa. Baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mgalu, hayupo. Yupo!

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo.

**NAIBU SPIKA:** Huku umehama? Sawa, karibu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami jioni ya leo nitoe mchango wangu mdogo kwenye maboresho mbalimbali ya sheria yaliyowasilishwa ndani ya Bunge letu. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ya pekee kwa kutupendelea zawadi ya uhai na kutuwezesha kutimiza majukumu yetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, hii Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, vilevile nampongeza Naibu Waziri kwa kuteuliwa. Pia kipekee nampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uteuzi na kazi nzuri aliyofanya ndani ya Bunge hili. Nampongeza sana Mkurugenzi wa TAKUKURU kwa kuteuliwa na kuanza kazi pamoja na Taasisi hii ya TAKUKURU na maboresho mbalimbali yaliyowasilishwa mchana wa leo na sasa hivi tunayajadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijielekeze kwenye maboresho au sheria hii ya Kupambana Rushwa kwamba kwanza naunga mkono maboresho ya vifungu mbalimbali ambavyo vimesemwa hapa kwenye wasilisho hili mchana wa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee natambua Waheshimiwa wenzangu wamesema vizuri sana kwenye mapendekezo ya mabadiliko ya kifungu hiki 25 iliyotarajiwa kwenda kwenye Kifungu cha 10(b), nami nataka niseme nakubaliana na kazi nzuri iliyofanywa na Kamati. Hongereni sana Kamati, mmeturahisishia kazi. Pia, napongeza maoni yaliyowasilishwa kwenye Kamati hususan kwenye mtandao huu wa kupinga rushwa ya ngono, wamefanya kazi nzuri na wadau mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotaka kuchangia tu hapa, kwa kuwa Serikali imeonesha dhamira ya kukubaliana na maoni ya Kamati na pengine na ya Wabunge tunayoendelea kutoa hapa, ni hili suala la rushwa ya ngono. Kwanza nakipongeza Chama cha Majaji Wanawake, wakati huo 2007 walivyoingiza kwa mara ya kwanza Kifungu cha 25 imesemwa hapa Bungeni, jitihada

mbalimbali za kupambana na rushwa kwa awamu tofauti tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ilipofika 2007 kwa kuingiza Kifungu hiki ambacho kinatambua sasa utu wa mwanamke au kwa mhanga yeyote wa masuala ya ngono unazingatiwa, napenda kuipongeza sana hatua hiyo ambayo sasa tumeona kwa miaka ya hivi karibuni kasi ya kuripoti kwa matukio ya rushwa ya ngono.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mahakama pia tumeona kesi mbalimbali zikiwasilishwa, tumeona wahanga mbalimbali wakitoa ushirikiano wa kuyasemea matukio hayo ya rushwa ya ngono, na pia tumeona jitihada za Serikali na Ofisi yenyewe ya TAKUKURU wakitoa semina, wakitoa elimu kwa makundi mbalimbali juu ya madhara ya rushwa hii ya ngono na kutoa ushawishi kwa wale wahanga waweze kutoa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini Kifungu hiki kiliendelea kutoa ulinzi, na kwa sababu bado hakuna tafiti ya kutosha kuonesha kwamba upande mwingine katika dhana hiyo hiyo ya mtoaji na mpokeaji, au aliyeridhia kufanya hilo tendo kwamba pengine kuna athari kubwa, napendekeza na kukubaliana na mapendekezo kwamba kifungu hiki kibaki kama kilivyo kwa sababu tumeona athari ya rushwa hii ya ngono kwa kweli inamfanya hata yule mhanga kuwa mtumwa wa ngono, inadhalilisha na wakati mwingine inaua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wale wanaolazimika kutoa rushwa ya ngono siyo kwamba wanapenda, lakini yapo mazingira ya unyanyasi, yapo mazingira ya vitisho, yapo mazingira ya ukandamizaji, yapo mazingira ambayo wenye mamlaka ndio mara nyingi wamekuwa wakitumia mazingira hayo ambayo yanapelekea hata mtu ambaye hapendi kufanya hicho kitendo kwa sababu kwanza ni dhambi katika vitabu vyetu vya dini, lakini inapelekea na kumlazimisha kutokana na hali halisi ya maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa yametajwa hapa na nimeona wakati Kamati inawasilisha, hata Serikali imejaribu kutaja mikataba ya Kimataifa ambayo tumeingia nayo, lakini nataka nikubaliane na Mheshimiwa Neema kwamba mazingira pia yanatofautiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nampongeza kwa dhati Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ameendelea kupambana, kuongoza Serikali na kuleta Miswada mbalimbali hapa Bungeni ambayo ina nia ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa namna yoyote ile uwe wa watoto, uwe wanawake, uwe wa watoto wa jinsia mbalimbali lakini uwe pia na makundi mengine ikiwemo hata wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme, kwa kuwa bado Serikali inaendelea kupambana, kwa sababu kama nilivyosema wahanga wa changamoto hizi wengine hali zao ni tete, pengine kipato, mtu anafanya kwa sababu ametishiwa kupunguziwa kipato au kutopanda cheo, lakini pengine hali ya kiuchumi; lakini kwa sababu Serikali yetu inajitahidi na inaendelea kuweka mazingira wezeshi na maendeleo ni mchakato, sasa tusilinganishe sana na mikataba hii ya Kimataifa kwa sababu inawezekana kuna tofauti ya *level* ya kimaendeleo katika hizo nchi ambazo pengine zinawajengea uwezo sasa hata wale wahanga kulazimika kupambana na kutoshiriki katika hii rushwa ya ngono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimalizie kwa kuomba wahanga (wanawake wenzangu hata wanaume) hasa sisi wenye mamlaka kutekeleza sheria hii na kuishi viapo vyetu, kwa sababu inawezekana kabisa tukatekeleza kwa kuwa tumeaminiwa, na uongozi ni dhamana pia uongozi ni ibada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, zile dhamana zetu, pia hata kwenye ngazi ya jamii kwa sababu rushwa hii ya ngono ipo ndani ya jamii, mfano ndani ya familia zetu wapo wale wadada wa

kazi nao wanapata changamoto katika maeneo haya, kwa hiyo, sisi kama jamii nayo tuone jambo hili, tuunge mkono Serikali, tuunge mkono wadau wa kupambana na hii rushwa ya ngono kwa sababu mwisho wa siku inailetea Taifa kupata pengine hata watumishi wasiokuwa na staha au wasiostahiki kupewa huo upendeleo kwa sababu tu ya rushwa ya ngono na hivyo kuchelewesha maendeleo kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimalize kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta sheria hii ambayo sasa imetupa fursa na wadau wote wa Mtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono kupata fursa ya kuchambua na kutoa maoni mapya, pia kuelimisha na kuendelea kutoa msisitizo kwa jamii ya vyuo, shule, taasisi za Kiserikali, vyama vya siasa kwamba vita hii ni endelevu, tuendelee kupambana na tuhakikishe ipo siku rushwa ya aina yoyote hapa nchini itakuwa haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa kama nilivyosema, naipongeza pia Taasisi ya Kupambana na Rushwa, lakini naiomba kasi zaidi. Tunamwaamini Mkurugenzi aliyeteuliwa pamoja na wafanyakazi wote wa Taasisi hii lakini kwa wakati huu tuna matarajio kwa sababu hata Sheria, kwa mfano, inavyowasilishwa, Taarifa ya *CAG* inataka ipelekwe kwenye vyombo mfano TAKUKURU ili tuone hatua zinazoendelea kuchukuliwa. Kwa hiyo, tunaomba sana, Taifa linawategemea na tunaamini Tanzania bila rushwa inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja na mapendekezo ya Kamati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Kamani, jiandae Mheshimiwa Maganga, Mheshimiwa Jesca na tutamalizia na Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Miswada hii muhimu,

lakini mchango wangu wa leo nitajielekeza zaidi katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuteuliwa na kuaminiwa na Mheshimiwa Rais, kutumikia katika Wizara hii muhimu. Pia, nampongeza sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na viongozi wengine wote ambao wameendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuhudumu katika kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze pia kwa kuipongeza Serikali kwa sababu lengo la Muswada huu ni kuhakikisha kwamba inaendelea kuipa nguvu *PCCB* kulingana na malengo kabisa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha kwamba anaondoa rushwa katika nchi yetu. Naipongeza Serikali kwa sababu kuna vifungu ambavyo leo hii mimi naliomba Bunge lako Tukufu litusaidie kupitisha marekebisho haya ili kuiongezea nguvu *PCCB* kwenda kufanya kazi nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Saba kinarekebishwa ili kuongeza wigo wa *PCCB* katika kufanya kazi zake. Sheria iliyokuwepo ilikuwa inaipa mamlaka *PCCB* kufuatilia makosa yale yaliyo chini ya sheria hiyo pekee. Sasa tunaomba Bunge hili lipitishe marekebisho haya ili kuongeza wigo wa makosa ambayo Taasisi hii ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inakwenda kushughulikia kuunganisha makosa mengine ambayo yapo katika sheria nyingine zote. Hii itaendelea kuiongezea mikono na kuipa nguvu taasisi hii muhimu ili iendelee kutusaidia kuondokana na adui rushwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia kwa marekebisho haya kwa sababu Kifungu cha 10 kinalenga kuharakisha utaratibu wa kushughulikia kwa misingi ya Kimahakama watu wanaokutwa au wanaoshitakiwa na makosa haya ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua kwamba kuna muda mrefu ambao kesi zinakaa Mahakamani kwa sababu tu ya *technicalities,* kesi inakaa miaka mingi sana. Huku nje jamii inajua kwamba kuna mtu anashitakiwa kwa makosa ya rushwa labda hata ushahidi wake ulikuwa ni wazi na kila mmoja ana ufahamu lakini kwa sababu ya *technicalities* kesi hizi zinakaa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba tunapunguza hizi *technicalities* ili makosa haya yaweze kufanyiwa kazi kwa haraka na kukamilika. Kwa hiyo, hii itatusaidia pia kuongeza imani ya wananchi wetu kwa Serikali yetu, lakini pia kwa Mahakama zetu kwa sababu wananchi wanapenda kuona pale ambapo kuna makosa yanafanyika hata ya ubadhirifu na rushwa yanafanyiwa kazi kwa haraka. Naipongeze sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Serikali kwa mapendekezo ya mabadiliko ya kifungu cha 15, 16, 17, 18 na 20 katika sheria tuliyokuwanayo. Lengo pia la vifungu hivi ni kuhakikisha kwamba tunaongeza wigo wa kuwapa adhabu wale wanaokutwa na makosa haya ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria iliyokuwepo ilikuwa inaruhusu mtu anapokutwa na hatia ya makosa haya ya rushwa, chini ya sheria hii faida zozote zile ziwe ni za fedha au za kinamna nyingine yoyote kutokana na rushwa, basi kama ni fedha zinataifishwa na kurudishwa Serikalini katika mamlaka husika ili asiweze kunufaika kwa namna yoyote na vitendo vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mabadiliko ya sheria yanaongeza wigo sasa wa namna Serikali inapoweza kushughulikia *proceeds* hizi za uhalifu huu ambao mtu anaweza kuwa amefanya, na kimsingi kama nilivyosema mwanzo inaongeza imani kubwa sana ya wananchi kwa Serikali hata kwa Mahakama zetu na vyombo vya haki kuona kwamba mtu anapokutwa na makosa haya, basi asiweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jamii zetu, watu wanaamini kwamba wanaweza wakafanya kosa, ukikamatwa utatumikia kama ni kifungo cha miaka mitatu, minne, mitano na ukitoka, basi utazikuta fedha zako zile ulizozipata kwenye ubadhilifu au rushwa. Sasa Sheria hii imezidi kutuonesha kwamba pale unapokutwa na makosa haya, basi yale manufaa unayoyapata yataondolewa kwako na kurudishwa katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wale waliochangia mwanzo katika maoni katika Kifungu hiki cha 25 kinachozungumziwa kuhusu rushwa ya ngono. Mapendekezo yaliyokuwa yameletwa na Serikali yetu kimsingi yalikuwa yanakwenda kumkandamiza na kumnyamazisha kabisa mhanga wa rushwa hii ya ngono. Wote tunafahamu kwamba ili mtu atoe rushwa anajikuta hana *option* nyingine yoyote na anaamini kwamba bila kutoa hiyo au bila kulazimika kufanya hivyo, basi anaweza asifanikiwe kile anachokihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wanaotoa rushwa hizi za ngono kitakwimu ni wanawake na hii pia ni *form* nyingine ya ukatili wa kijinsia. Leo hii tukiweka vifungu ambavyo vinanyamazisha au vinampa adhabu mhanga wa rushwa ya ngono anapokuja kutoa taarifa kwa namna moja au nyingine tunahalalisha vitendo hivi vya rushwa ya ngono kwa sababu watu hawatakuja tena kutoa taarifa wanapotendewa vitendo kama hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi au zaidi ya 99% yeyote anayekubali kutoa rushwa ya ngono sio kwamba anapenda, hapendi, ni udhalilishaji uliopitiliza. Rushwa ya ngono ina hasara nyingi kuliko hata rushwa ya fedha. Kuna uwezekano wa kupata maradhi. Mtu anaweza akapata ujauzito, mtu anaweza kupata *emotional torture* ambayo atakaa nayo kwa miaka mingi, lakini ni udhalilishaji wa utu na uvunjifu wa haki za binadamu uliopitiliza. Kwa hiyo, siamini kwamba kama mtu analazimika kufanya kitendo hiki naye basi tumpe adhabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, pamoja na kuona *spirit* ya Kamati ambayo naipongeza sana kwa kweli imetoa maoni ambayo Watanzania wengi tunayo vichwani mwetu, pia, naipongeza Serikali kwa sababu imeonesha nia ya kukubaliana na maoni ya Kamati ambayo pia naamini ni maoni ya Wabunge wengi na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu nafikiri ni wakati sasa wa kuendelea kuimarisha au kuboresha mifumo ya utoaji wa taarifa katika vitendo hivi vya rushwa ya ngono ili kuwalinda sasa hawa wahanga. Pia tuendelee kuhakikisha kwamba wale wanaotolewa taarifa za vitendo hivi vya rushwa ya ngono wanafanyiwa kazi au kushughulikiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwepo na mara kadhaa kuna *clip* hata za watu fulani zinavuja kwenye mitandao ambao wanakuwa wanahitaji rushwa ya ngono kwa watu ambao wanahitaji kitu kutoka kwao, lakini jamii haijulishwi namna gani vitu vinafanyiwa kazi. Inashusha pia imani ya watu kwamba hata nikienda kuripoti vitendo hivi labda havifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kama ushauri, kuangalia namna ya kuendelea kuvishughulikia vitendo hivi ili kuvipunguza na ikiwezekana kuviondoa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naipongeza sana Serikali kwa sababu naamini kupitishwa kwa mabadiliko haya itakuwa ni mwanzo mzuri sana pia wa kupunguza ubadhirifu wa fedha na mali za umma lakini kuongeza uadilifu katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naliomba Bunge hili Tukufu kupitisha mabadiliko haya kwa kura zote ili twende kuyafanyia kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Maganga, jiandae Mheshimiwa Jesca na tutamalizia na Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa siku ya leo nami niweze kuchangia Muswada huu wa marekebisho ya Sheria masuala la rushwa. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Nchi, kwa siku ya leo tena kuweza kupata nafasi na fursa hii kuweza kulihutubia Taifa kwa njia ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Pia nawapongeza viongozi wote walioaminiwa na Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwemo babu yangu ambaye ni Mwalimu wangu wa Sheria, Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi. Pia, nampongeza babu yangu Mheshimiwa Lukuvi, amepata nafasi; vile vile nampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ameaminiwa na Mama kuja kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia nachukua fursa hii kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa Wizara hii, Bwana Chalamila ambaye ameaminiwa kabisa na hii Sheria ambayo tunaipitia leo upya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwa ujumla jumla kwa sababu Mwanasheria Mheshimiwa Olelekaita amenifundisha vizuri hapa kwamba nisifuate Vifungu sana. Nimevisoma vifungu vyote na kwa kweli mawazo yote ni mazuri isipokuwa labda watumishi wanaweza sasa watuangushe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia, Muswada umegusia maeneo mengi. Imegusia upande wa madini, hapa mwanzoni kulikuwa kuna ripoti inaonekana zilikuwa zinadanganya, hivyo inatufanya kuwa matapeli katika nchi kwamba kunakuwa na ripoti ambayo ni hewa, ambapo mwekezaji hata akija kuwekeza mabilioni yake anakuta ni tofauti na ripoti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa nimeona huu Muswada umezungumzia, lakini Wabunge wenzangu wamezungumzia suala la ngono, nami nilizungumzie kidogo. Hili suala la ngono kwa kweli ukifikiria na ukikuta mtu aliyetendewa hayo, naweza nikasema kwamba kifungu hiki cha saba, kwanza hii faini ni kidogo, ya shilingi milioni mbili au isizidi shilingi milioni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, kiujumla kwamba hii faini ni kidogo mno, kwa sababu unakuta mtu kafanyiwa unyama na mwajiri wake. Kwanza amemfanyia kitendo mpaka amepata na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, ina maana ameharibu kabisa maisha yake, lakini faini yake ni shilingi milioni mbili mpaka shilingi milioni 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali hapa iongeze faini ikiwezekana iwe shilingi milioni 100 na kuendelea kwa sababu mtoto wangu akitendewa suala kama hili sitampata tena. Kwa hiyo, ushauri wangu ni huo kwamba hii shilingi milioni mbili mpaka shilingi milioni 10 ni kidogo sana. Hata mimi ni-*declare interest,* ukiangalia hata faini zetu tu za mafuta faini zake huwa ni shilingi milioni 20 na kuendelea. Sasa inakuwaje mtu amefanyiwa unyama, amedanganywa labda ili nikuajiri lazima kwanza nipite na wewe, tofauti hapo ina maana anaweza akafanya hesabu hata kama likibumburuka shilingi milioni 10 siyo kitu!

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta kwanza hawa mabosi huwa wana pesa nyingi sana. Kwa hiyo, anaweza akafanya kwa kujua kwamba shilingi milioni 10 tu au shilingi milioni mbili nitazitoa na akafanya. Kwa hiyo, ikiwezekana hii iongezwe kidogo faini ili kusudi itamke kuanzia shilingi milioni 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, mimi ni mdau wa michezo, na toka nizaliwe tumekuwa tukisikia Simba na Yanga. Ina maana hakuna timu nyingine? Nikiangalia kwa sisi tunaoishi vijijini tunao wachezaji wazuri sana. Huwa tunajitahidi hata kupandisha

timu zinapofika *rank* ya juu waamuzi wanazitendea vitu vya kinyama sana hasa ikifika huko kwenu huko Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na timu nyingi tu, mfano, tulikuwa na Geita, tulikuwa na Gwambina, mwamuzi tu anaamua kupuliza kipenga, bwana faini ielekee vile, lakini hili suala kwa vile na humu limeguswa, labda sasa kutakuwa kidogo na heshima. Tunatamani na sisi kwenye maeneo yetu tuwe na timu nzuri ambazo zitakuwa zaidi ya Simba na Yanga kwa sababu sisi ni wadau wa mikoani na huko tunaishi na wachezaji wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lingine ambalo limezungumzwa kwenye mabadiliko haya kuhusu ya mambo ya uchaguzi. Ukiangalia hii faini mliyoiweka hapa, kwa mfano, mtu unaenda kugombea Udiwani ama Ubunge, umeniwekea faini ya shilingi milioni mbili tu, naweza nikafanya faulo yoyote ile kwa kujua kwamba hesabu yake ni shilingi milioni mbili au milioni kumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na penyewe hapa iangaliwe vizuri ili kusudi kuhakikisha inapandishwa faini kwamba ikibainika mtu alishinda kwa kutumia rushwa, ikiwezekana apigwe hata shilingi milioni 500, kwa sababu unakuta mtu kumbe hakuchaguliwa na wananchi. Anawaongoza wananchi kwa nguvu kutokana na pesa zake. Kwa kuwa ana pesa tu ameamua kumnunua Mkurugenzi wa Uchaguzi pamoja na viongozi wengine lakini wananchi hawamhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, anaangalia kwamba naenda Bungeni, mimi naenda kupata posho kiasi gani? Kwa hiyo, nikitoa faini ya shilingi milioni 10 au shilingi milioni mbili inatosha, mtu anafanya faulo kivyovyote. Kwa hiyo, Kamati inawapongeza sana kwa kweli, mmepitia vifungu vingi lakini kwenye hii faini tu mimi ndiyo naona hapajakaa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maombi yangu kwamba ikiwezekana vitu vingine vichambuliwe ili kuhakikisha faini

zinaongezeka ili watu wajenge heshima kwenye eneo hili la rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne ni kwenye mikataba ya madini. Hizi leseni za madini, watu wamekuwa wajanja wengi sana wana-*apply* kwenye mitandao wanapata leseni za madini, wana-*temper* wakati mwingine na *GST,* wanaandika ripoti ambazo siyo sahihi, wawekezaji wanakuja kutoka huko na pesa zao wengine wamekopa kutoka kwenye mabenki, tumeshuhudia wakija kufuatilia hizi ripoti, anakuta hakuna kitu, ripoti imedanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa faini kama hizi mtu hawezi kuacha kufanya makosa kama haya. Kwa hiyo, na lenyewe ikiwezekana kwenye upande wa madini hapa faini iongezeke ikiwezekana iwe ni shilingi milioni 500 na kuendelea kwa sababu ni suala la matrilioni, siyo suala la kimzaha mzaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine namwomba sana aliyeaminiwa kwenye hii sekta, hii sekta Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU akisimama imara kiukweli kwanza atatusaidia sana katika nchi yetu. Zipo nchi nyingi, mimi ni shahidi, ukiangalia Rwanda wanasimamia vizuri sana haya masuala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona sheria za Rwanda hata kama ni dereva, yaani utaendesha kwa heshima kwa kuzingatia vitu ambavyo vimeandikwa humo kisheria. Ila sisi kwa kuwa hii sheria ilikuwa haijafanyiwa marekebisho muda mrefu, ni matumaini yangu sasa kwa vile leo ndiyo tunafanya mchakato na Mheshimiwa Rais aharakishe kuipitisha ili kusudi iweze kusimamiwa vizuri tuweze kupiga hatua katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kuweza kunipa nafasi. Pia mambo mengi ambayo yameongelewa humu na wenzangu niseme kwa 100% nayaunga mkono isipokuwa tu hapa kwenye faini mwangalie upya ili kusudi maeneo mengine yapande faini ili kuhakikisha kwamba tunasimamia vizuri nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nampongeza Mheshimiwa Simbachawene ambaye ni Waziri wa Sekta hii pamoja na Naibu Waziri, rafiki yangu kabisa Mungu amekufungulia, kwa hiyo, simama Mungu akusaidie uendelee kuwahudumia wananchi. Pia uendelee kutusikiliza sisi Wabunge kwa sababu, wewe sasa hivi tunakuangalia na sisi tuna wananchi wengi ambao wanaitegemea Wizara hii, wanapoomba maombi yao walio na sifa waweze kuajiriwa bila kupitia haya masuala ya kirushwa rushwa. Walio na haki ya kuajiriwa waweze kuajiriwa kwa kufuata haki, kwa sababu hawa watu wamesota, wamesoma na wana sifa ya kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi huwa tunaumia sana kuona viongozi wanatoka sehemu za mijini tu, hata siku moja sijawahi kuona Mkurugenzi ametoka Mbogwe ama Mkuu wa Wilaya ametoka Mbogwe ama *DAS* ametoka Mbogwe. Kwa maana hiyo, hili suala huwa linaniumiza sana. Nikiangalia, nina wasomi wengi wenye uwezo, hata kama wanajeshi wapo vijana wengi ambao wamepitia hatua za kijeshi na wana sifa za kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia sheria hizi sasa kwa vile mmeziletea mabadiliko, namwomba tu Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU nami nitakuwa bega kwa bega naye kuhakikisha kwamba watu wetu ambao wana sifa za kuajiriwa bila kutoa rushwa waweze kuingia kwenye mfumo ili kuweza kuitumikia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jesca, ajiandae Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia. Napi pia nitachangia kwenye huu Muswada wa Kupambana na Rushwa na niungane na wenzangu kuwapongeza Wizara kwa kazi kubwa

waliyoifanya na Kamati pia kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa ajili ya kuchambua vipengele hivi ambavyo tunakwenda kufanyia marekebisho hasa kwenye *issue* ya kupambana na rushwa. *Interest* yangu kubwa pia itakuwa katika kipengele kile kile cha 25 na nitakuwa na mambo mawili ya muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuomba kipengele kile kibaki kama kilivyokuwa kwa sababu zipo sababu za msingi, lakini pia nitaongelea na suala linahusu adhabu. Kwanza kabisa, niungane na Mbunge ambaye amemaliza kwamba ahadi hizi ambazo tunapenda ziwekwe katika sheria hii ya Kupambana na Rushwa hasa kwenye rushwa za ngono ziwe ni adhabu ambazo zinakwenda kuzuia lile jambo lisiendelee tena, zisiwe ni zile adhabu ambazo tuna-*intend* kwamba iende ikamrekebishe mtu. Iwe ni adhabu inayokwenda kuzuia mtu aone kabisa kwamba hatakiwi kufanya hiki kitendo kwa sababu ya madhara yanayotokana na tendo lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wameongelea sana hapa masuala ya afya ambapo kama kutatolewa hiyo rushwa ya ngono mtu gani anaweza akaathirika kisaikolojia, lakini pia na afya yake. Mimi nitakwenda mbali zaidi kuona ambavyo madhara yanaweza yakatokea kwenye jamii. Ni kwamba unakwenda kumpa mtu kazi kwa sababu alitoa rushwa ya ngono, na unakwenda kumpa mtu kazi labda tuchukulie ya udaktari, haujaangalia *professional* yake, hujaangalia uwezo wake, uelewa wake na unyeti wa ile kazi anayokwenda kufanya ila wewe umeangalia *professional* yake katika *performance* katika suala la mapenzi au kwenye rushwa ya ngono, halafu huyu mtu anakwenda kuhudumia watu na hiyo kazi ameshaipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu fikiria! Ndiyo maana unakuta sasa hivi ukiangalia katika tafiti za dunia zinasema 43% ya watu wanaokufa duniani ni kwa sababu ya matibabu yasiyo sahihi yaliyotolewa na wauguzi. Watu zaidi ya 40% wanapoteza maisha kwa sababu muuguzi hakumpa tiba sahihi yule mgonjwa. Sasa ndiyo

tunasema hapo, ndiyo hao watu sasa wanaweza kuwepo wengi wao wapo katika makundi kama haya *especially* kwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anapewa nafasi ile lakini uwezo wake wa ku-*perform* kwenye ile nafasi haupo. Kwa hiyo, anatusababishia vifo, lakini anaweza kutusababishia madhara, anaweza kutusababishia ulemavu kwa watu kwa sababu hana hiyo *skill* ya kufanya ile kazi, kwa sababu hakupata kwa vigezo vya kwamba ana uwezo huo, bali alipata kwa vigezo vya kwamba alitoa rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana tunasema adhabu hii haitoshi. Inabidi iwe ni adhabu ambayo inakwenda kuzuia kwa sababu madhara yake yanakuwa ni makubwa yanakwenda mpaka kwenye jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ameongelea Mheshimiwa Mbunge pia, tunapoongelea hii sheria itakwenda kufanya kazi siyo tu kwenye masuala ya kazi, inaweza kwenda kufanya kazi pia hata kwenye masuala mengine, kwa mfano kwenye shule au kwenye vyuo. Kuna malalamiko mengi ya kwamba hata watoto wanapokwenda kwenye vyuo ili kufaulu anadaiwa rushwa ya ngono ili apate maksi za kuridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukienda kusema huyu mtoto au huyu mwanafunzi alienda akamshawishi mwalimu wake ili ampe rushwa, ampe maksi nzuri inakuwa haileti maana. Sisi tunategemea kwamba yule mwalimu aliyepo pale Chuo Kikuu yeye ni mlezi. Kwa hiyo, hatutegemei kwamba ushawishi wa mwanafunzi utamzidi *Lecturer* mpaka ashawishike, akubali kumpa mwanafunzi maksi kwa rushwa ya ngono eti kwa sababu mwanafunzi amemshauri, hapana!

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutegemei kwamba mwanafunzi aliyemaliza chuo kikuu anakwenda kuomba kazi mahali, yeye ndiye mwenye shida ya kazi akawa ana nguvu kuliko yule bosi mwenye *power* ya kumpa kazi. Moja ya uwezo wa hawa viongozi

wanaokuwepo kwenye hizo nafasi wawe na uwezo wa kukabiliana na masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama yeye atakuwa ni mdhaifu kwa mtu tu anayekuja kufanya *interview* kwa muda mfupi, huyu ndiyo bosi tumemkabidhi labda kitengo, wakina dada wengi mle, tuna binti zetu wanaajiriwa mle, kuna wake za watu wanaajiriwa mle, kama ni mdhaifu namna hivyo kwenye *interview* tu anavutika kimapenzi, wale wake za watu walio chini yake! Wakija naye kumshawishi atavutika pia! Hao mabinti zetu wadogo wadogo wanaokuwa wameajiriwa ni wachumba za watu, yeye kama bosi ni mdhaifu wa kuathirika kiasi hicho, si nao watamvuta na yeye nao ataathirika nao, atataka afanye nao mapenzi!

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea a-*demonstrate* nguvu ya kupambana na hiyo rushwa kwenye *interview,* lakini apambane na hiyo rushwa hata anapokuwa katika mazingira ya kazi ili watu wawe na uhakika wa usalama wa wake zao wanaofanya kazi kwenye ofisi mbalilmbali. Kama ndiyo hivyo, mabosi watakuwa wadhaifu tu kwenye rushwa za ngono wanapofanya *interview,* huko maofisini itakuwaje? Wafanyakazi wa kike watakuwaje salama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunadhani kipengele kile cha 25 kibaki kama kilivyokuwa mwanzo ili kiendelee kumbana yule yule mwajiri, yule bosi ambaye ndiye mwenye nguvu; hasa tunasema aliyeshika mpini ili yeye, ajue namna ya kupambana asianguke kwenye ule mtego wa majaribu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine tukishasema tena hapa kwamba na yule anayeomba kazi naye aonekane na yeye alimshawishi, hapa itatuwia ngumu sana kumkamata yupi ndiyo mwenye makosa kwa sababu mosi, atamkandamiza bwana unataka kazi eeh! Leta rushwa ya ngono, huleti rushwa ya ngono ukienda kuniambia mimi nimekupa rushwa ya ngono nakwambia na

wewe ulinishawishi. Sasa hapo itatokea *contradiction,* lazima atokee mmoja ambaye atakuwa anakamatwa na sheria …

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji. Mheshimiwa Mbunge anachangia vizuri sana, lakini nataka nimpe taarifa tu kwamba jambo lenyewe hili lipo *very subjective* kwa sababu ni jambo linalohusiana na mambo ya makubaliano. Sasa kwenda kuli-*justify* kwenda kwenye ngono bado kidogo lina utata utata lakini ni makubaliano inakuwa kati ya pande mbili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa yake. Ni makubaliano ambayo mtu mwingine anasema amekubaliana kutokukubaliana. Nafikiri Mheshimiwa Twaha amewahi kusikia hicho kitu. Tunakubaliana kutokukubaliana. Huyu mazingira; turejee jana. Jamani tulikuwa tunapitisha hapa sheria kuhusiana na kuwalinda watoto, kwamba mtu yEyote asiwatumie watoto kwa sababu tu yule mtoto ana uhitaji, basi mtu amtumie vibaya kwenye shughuli za uhalifu.

MHESHIMIWA Naibu Spika, sasa kwa sababu huyu; awe ni mama au ni kaka labda anahitaji kazi, amekwenda pale amekutana na bosi mwanamke, kwa sababu yule kijana wa kiume anahitaji tu kazi, basi yule mama anamfanyia vituko kumshawishi kwanza mpaka wafanye mapenzi ili aruhusu kumpa ile kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, au hivyo hivyo kwa mwanaume ambaye naye anataka kazi, na yule anakubaliana kwa sababu ya

mazingira, hana *option*. Huyu ni *inferior* lakini yule mwingine ni *superior.* Huyu mwingine sisi tuna-*assume* yeye bosi ni mlezi na ndiyo tumemwajiri, amechukuwa dhamana ya kusimamia sheria na maadili ya kazi. Kwa hiyo, hatutegemei yeye awe *part and parcel* ya kuungana na yule ambaye ni *inferior* katika kuvunja maadili na sheria zilizowekwa. Kwa hiyo, yeye ili aonekane wa maana, lazima a-*demonstrate* uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana tunasema kile kifungu kibaki kama vile kilivyokuwa ili wenzetu waliopo kwenye zile nafasi wasitumie zile nafasi kwa ajili ya kutuharibia vijana wetu, wawe wa kiume au mabinti zetu ambao ni wa kike, ambao wanakuwa *inferior* wanapokwenda kutafuta kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena, adhabu hizi kwa mfano tunapokwenda kwenye ngono za watoto wetu na zitakwenda mpaka kwenye vyuo vikuu, kwa sababu unafikiria huyu mtoto aliyepata maksi kutoka chuo kikuu kwa kutoa rushwa ya ngono amefaulu, ana *first class GPA* anatakiwa kuajiriwa kuwa daktari wa binadamu. Amekuja huku anajua anayo silaha tena ni ile ile anakutana na rushwa naye anaajiriwa anaonekana ana maksi nyingi, amefaulu vizuri, nako anatoa ngono anapata kazi. Huyu mtu *performance* kwenye *industry* inakwenda kuwa ni *very poor. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana zisiwekwe adhabu hizi za shilingi milioni mbili. Shilingi milioni mbili ni kitu gani? Bosi atashindwa nini? Ndiyo maana tunakubaliana na Kamati kwamba hizi adhabu ziongezwe. Mtu atashindwa kutoa shilingi milioni mbili? Kama tu hiyo rushwa yenyewe ya ngono mtu mwingine anaweza akanunua hiyo ngono zaidi ya shilingi milioni mbili kwa mara moja tu. Sasa atashindwa kusema kwamba nikalipe hiyo adhabu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba, hii adhabu kwanza ipande kama Kamati ambavyo imeshauri na ikiwezekana wanasheria wetu mpo humu mweke adhabu ambayo inakwenda

kukomesha vitendo hivi ili tuwasaidie watoto wetu, vijana wetu wawe salama ili tuwasaidie wanafunzi wetu huko kwenye vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii tunaulizana wakati mwingine unamchukuwa mtu ambaye ni *graduate* unamwajiri kwenye kampuni, unamchukua mtu ambaye ni *certificate graduate* unakuta yule wa *certificate* ana-*perform* vizuri kuliko hata yule *graduate*. Unajiuliza, huyu na *flying colors* za 'A' zote hizi, *GPA* kubwa namna hii anashindwaje ku-*perform* kwenye kitu hiki? Kumbe hata siyo *performance* za kweli, ni viini macho. Kumbe wewe unamwona ana *professional* ya 'A' kwenye somo lile la sayansi kumbe ana *professional* ya ngono, ana 'A' kwenye mapenzi. Sasa anapokuja ku-*perform* kwenye *field* inashindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndiyo maana tunasema adhabu lazima ziongezwe ziwe zinakwenda kuzuia ili tupate watu ambao wana uwezo watakapokwenda kwenye *industry* waweze ku-*perform*. Tukiwa na ma-*engineer* waweze ku-*perform*.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa tunakwenda kukagua miradi ya Serikali, unakuta kweli tumepeleka *engineer,* lakini unajiuliza, hata mimi nisiye *engineer,* kweli ninge-*propose* nijenge msingi wa nyumba ndefu namna hii, hela yote iliyotakiwa kumaliza madarasa nane imeishia kwenye msingi wa darasa moja. Huyu ni *engineer* aliyesoma wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unakuta yale madhara yanatoka kule yanakuja moja kwa moja mpaka kwenye jamii, yanakuja yanaendelea kututia umaskini, yanakuja yanazuia *innovation.* Tuna watu wengine inawezekana kabisa kumbe na wao ni walimu wanafundisha watoto wetu, kumbe nao wamepewa zile nafasi za ualimu kwa sababu ya kuonekana ali-*perform* vizuri kwenye mapenzi na siyo kwenye *skills.* Sasa huyu anakwenda kuzalisha tunda gani? *As a results* ndiyo maana sasa hivi ukitaka kuongelea rushwa za mapenzi kwenye vyuo unaweza ukapata upinzani mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja mpaka nilijiuliza, mama mmoja amesimama, ni *lecturer* wa Chuo Kikuu kimoja hapa nchini, anapinga rushwa ya mapenzi chuoni, yeye akiwa ni mwalimu wa pale, wenzie walim-*punch* vibaya mno. Nikaona aah, kumbe *this is the system* kwenye shule na kwenye vyuo vyetu! Sasa tunalalamika, kwa nini watoto wetu hawaajiriki? Kwa nini watoto wakienda kupambana kwenye *East Africa* na duniani wakifanya *interview* hawa-*perform?* Sasa ni namna gani wanapata hizo 'A' wanazozipata?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba adhabu iongezwe, lakini kipengele kile Na. 25 kibaki kama kilivyokuwa na yule mwingine ambaye ni *victim* kifutwe kabisa atolewe, yeye asiwe anaweza kuhukumiwa, ahukumiwe yule mkubwa ambaye sisi tunaamini kwamba tumempa ile nafasi kama mlezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa. Bila kupoteza muda, nitajielekeza kwenye Kifungu cha 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mwaka 2017 Mheshimiwa Rais wa kipindi hicho akiwa Makamu wa Rais, tarehe 8 mwezi Januari akizungumza na Chama cha Majaji Wanawake Tanzania aliwasisitiza, sitanukuu maneno yake, lakini aliwasisitiza kwa namna moja au nyingine kuendelea kusimamia mapambano dhidi ya rushwa, sana sana rushwa ya ngono.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Rais akiwa Rais mwaka 2021 tarehe 28 Machi, akizungumza wakati anapokea ripoti ya *CAG* na TAKUKURU pia ameendelea kusisitiza kuhusiana na

mapambano ya rushwa ya ngono na alitaka wajipambanue zaidi kwenda mpaka kwenye masuala ya uvujishaji wa mitihani. Nafikiri wote tunakumbuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kwa sababu nami nafuatilia sana, mimi ni miongoni mwa watu ambao napenda sana haki na kwa kweli jambo ambalo linahusiana na rushwa ya ngono ni jambo ambalo linatweza utu wa mwanadamu. Nazungumza hivi kwa sababu mimi pia katika wanaharakati katika upambanaji kwenye maisha tumepitia maeneo mbalimbali ambayo tumeshuhudia kwa namna yoyote ile kwa wenzetu wakiwekwa kwenye mazingira ya kuombwa rushwa au kutoa au mazingira kama hayo, kwa namna moja au nyingine. Wengi humu tupo *exposed* kwa namna moja au nyingine katika harakati zetu za kutafuta maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu rushwa ya ngono inaweza ikatolewa kwenye masuala ya biashara, kwenye masuala ya sanaa, *News Room,* watu wa habari wanajua hata hao watu wengine mnaowaona kwenye *media* huko wakikusimulia *story* zao mnaweza hata mkashangaa mtu kafikaje? Pia kwenye siasa, sisi wote humu ni wanasiasa, kuna mazingira hayo sana. Nasema nisingezungumza hili pengine ningedaiwa na wanasiasa vijana wa kike ambao wanapambana leo kushiriki kuonesha uwezo wao kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangaa sana na ninatamani leo humu tungejua pengine *story* iliyosababisha Serikali ilete marekibisho ya kile kifungu cha 10(b) ambacho kina-*criminalize*, kinamfanya mhalifu aliyefanyiwa uhalifu wa kuombwa kutoa rushwa ya ngono ili atendewe haki kwa namna moja au nyingine kuwa na yeye ni mhalifu. Nimeshangaa mno!

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mashaka sana kama Mheshimiwa Rais anajua kwamba hiki kitu Serikali imekileta. *With due respect,* sina maana kwamba Serikali inafanya kazi tofauti tofauti,

lakini nina mashaka sana, inawezekana kuna namna moja au nyingine hili jambo limekuja *premature*, limekuja kabla ya kupitia michakato yote, kwa sababu wanaharakati wamezungumza na Kamati wamefanya kazi kubwa, Kamati imepokea maoni ya watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ninasikitika kwa sababu tumeona, nami naomba tena kifungu hiki kinachoongezwa kiondolewe kwa sababu kifungu hiki kinaturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikukumbushe, mwaka 2017 Bunge hili lilitunga Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa, na ninazungumza hili mimi natambua masuala ya kijinsia na sitaki kulifanya liwe jambo la wanawake. Ni jambo la jamii nzima kwa maana ya jinsia zote, wanawake na wanaume. Waliosababisha tukapata kifungu cha 25 ambacho kinazungumzia rushwa ya ngono ni wanawake Majaji ambao walikutana na vielelezo katika Mahakama zetu zikionesha namna ambavyo kuna wahanga wa rushwa na rushwa ya ngono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki lengo lake lilikuwa ni kumlinda mhalifu anayekutana na changamoto kwenye kutafuta kwake maisha na michakato yake ya maisha ambaye kimsingi ndiye tunatakiwa tumlinde.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Serikali yoyote ni kulinda wananchi wake. Kama kuna mazingira ya watu kutokutendewa haki kwa kuombwa rushwa ya ngono, kwa sababu jamani rushwa ya ngono ni tufauti na rushwa nyingine. Naona kama tunachanganya haya mambo, kwa sababu msingi wa Serikali nafikiri walikuwa wanaona kwamba kwa sababu kwenye mazingira ya rushwa kuna mtoaji na mpokeaji, lakini rushwa ya ngono ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuelewane, yaani mimi siwezi kwenda kuomba kazi halafu nikafika nikamwambia, bwana mimi nipe kazi, unaniona mtu mwenyewe pisi kali. Yaani ukinipa kazi

unajua jinsi mambo yataenda. Yaani haiendi hivyo. Siyo kama rushwa nyingine, kwa sababu nikiwa nina pesa sana, nikaja nikamwomba mwenye mamlaka anipe mimi nafasi ninayoitaka nikampa hela, tunakuwa *equals* kwa namna fulani hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwe kwenye *sense* na tutumie tu uelewa wa kawaida wa kibinadamu. Kwa namna fulani nikija na mzigo wa hela hapa, labda shilingi milioni 100 au shilingi milioni 200, nikasema bwana mimi nataka hiyo kazi, hebu chukua hii hela, yaani kuna namna fulani hivi ni jambo tu la kimichakato. Siyo halali, lakini mtu kuvua nguo zake au mtu kwenda kufanya jambo ambalo linahusiana na utu wake ili apate nafasi, jamani huo ni udhalilishaji. Yaani mtu anaweza akajichukia maisha yake yote kwa sababu akikaa mwenyewe akajitafakari, ukijiangalia mwenyewe unasema, kweli mimi nafasi hii nimepata. Kweli niko kwenye nafasi nzuri, lakini niliipataje? Sijui mnaelewa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana natamani tulijadili jambo hili kwenye kifungu hiki kwa kuangalia utofauti. Wale wanawake Majaji walioleta kufungu cha 25 cha kudhibiti na kupamba na rushwa cha kwenye sheria, walitofautisha kati ya rushwa ya ngono na rushwa nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza naomba Mheshimiwa Rais asisaini kupengele hiki, na ninatambua kwamba kuna mikataba ya kimataifa tumeisaini na bado siyo sababu ya kutufanya tutunge kifungu hiki kwani kinaturudisha nyuma kwenye harakati za kudhibiti na kupambana na rushwa ya ngono.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbona *declaration of human right* kuna nchi nyingine ambao wanakubali *abortion*. Labda nitoe mfano mmoja, lakini mbona sisi nchi yetu hatukubali *abortion!* Kwamba kila kitu kinachotoka huko *conventions* zilizokubaliwa huko tutazikubali kama zilivyo? Kuna mazingira tofauti sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana, hili jambo hakuna haja ya kuliwahi. Halafu nimeshangaa, ni kama vile kuna namna kuna watu wanalindwa. Kwa sababu gani? Mbona kuna mikataba mingine mikubwa ambayo tumeisaini na hatujawahi kutekeleza na hakuna *rush* kama hivi kwenye hili? Yaani kuna changamoto gani kwenye hili? Yaani ni kama vile kuna mtu fulani mnataka kumwahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hoja ambazo zinazungumzwa, naomba nisome ili mwelewe kwa nini nazungumza hivi. "Mtu yeyote ambaye amemsababishia mwenye mamlaka kufanya kosa hili kwa kumwahidi, kumshawishi, kwa kutoa rushwa ya ngono ili apendelewe, apewe cheo, ajira au kupandishwa cheo, atakuwa hatiani kwa kosa la rushwa ya ngono na kustahili adhabu ya fedha za Kitanzania." Tunajua hilo jambo la adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wewe unajua kabisa uko chini ya kiapo cha maadili, kuna mtu anatoka huko anakushawishi eti akupe mwili wake ili umpe nafasi. Anakushawishije? Amekuwekea bastola kichwani! Yaani amekuwekea silaha kichwani kwamba anakushawishi sasa hamna namna inabidi ukubali! Yaani ni kama tunaenda mbele, tunarudi nyuma. Tulisema tunamlinda huyu kwa sababu mazingira yake ni magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya mtu mwenye mamlaka, mwenye madaraka ambaye anaombwa, ni rahisi yeye kuomba kwamba, mbona wewe unahangaika bure, wewe ni mtoto mzuri. Hebu njoo uongee na mimi vizuri. Yaani hiyo ni *story* ambayo inaeleweka inaenda, unaona kuna namna inaweza kuishia sehemu, lakini huyu ambaye eti mimi ndiyo naomba hiyo kazi, halafu mimi nakwambia bwana mimi usijali.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani ndiyo maana nikasema natamani nijue *story behind* kuleta hiki kufungu. Kuna namna nyingine ambayo mnaweza kudhibiti hili jambo kama ni kweli kuna mazingira ambayo yametokea hivyo na ninajua kwa sababu kuna *dynamics* nyingi, inawezekana kuna watu ambao waliripotiwa

wameomba rushwa ya ngono, lakini kumbe walitengenezewa mazingira kwa sababu na sisi tunajua jamii yetu ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafute namna nyingine ya kuona tunawawajibisha vipi watu ambao...

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanaonekana wameshawishi kwa namna yoyote...

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Kuna Taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ile kwa sababu kuna *codes of conduct*, mtu anaruhusiwa kukataa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, anayoyajadili, Kamati ilishakataa hicho kifungu na kinaondolewa kwa mujibu wa *schedule of amendment* ambayo imekuwa *moved* na Kamati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina kifungu kile cha mwanzo na ni kitu kizuri kama wamefanya hivyo, wametoa kweli. Sasa kwenye nukta hiyo, kama ni hivyo kweli, tutasubiri na nitaomba Mheshimiwa Waziri labda wakati anakuja kujibu tutakavyokuwa tunahitimisha tuone kimeondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shida ni kwenye kifungu hicho tu. Ukiachana na vingine ambavyo wamevizungumza kwenye kutoa adhabu, ukomo, kima cha chini na cha juu, hilo wala halina shida, lakini siyo kwenye kipengele hiki. Kwa hiyo, hiyo ni taarifa ambayo tutaiona baadaye kwa sababu nami nachangia kwa jinsi ambavyo ilikuja mwanzo na tulivyoisoma na pia kwa sababu huu mchakato ulikuwa mrefu sana. Kama itakuwa hivyo, basi nawapongeza sana wanaharakati wote na Watanzania wote kwa ujumla ambao waliona kuna mushkeli kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama ni hivyo tunaomba wenzetu wa upande wa pili wa Muungano wakafute kile kifungu cha 52 cha kwenye sheria ambacho wao wanasababisha na sisi tuonekane kwamba tunatakiwa tuingize kwenye sheria yetu kwa sababu wao walishaingiza. Kwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati amezungumza na kwenye taarifa kwamba wenzetu wa Muungano upande wa pili wameshaingiza na nimekisoma kile kifungu. Tunawaomba na wao kwa sababu nchi yetu ni moja, ni vizuri kutokuwa kwenye *double standard* kwenye sheria. Basi na wao wakakifute ili tuje tujadili namna gani nyingine ya kudhibiti hayo mambo kama kunaonekana kuna shida kweli lakini siyo kwa mtindo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tena watu watatushangaa na hata taasisi za kimataifa zitatushangaa. Walishatupongeza tumefanya vizuri, halafu leo tena tunakuja tunavuruga. Ni kama vile kuna namna tunatafutana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mtoa hoja wa kwanza, Mtoa hoja wa pili ujiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe kwa kusimamia mjadala huu. Pia nawashukuru sana

Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri. Ni kwa muda mfupi, lakini tumepata wachangiaji wengi, takribani tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mawili yamezungumzwa. Eneo la kwanza, ni ukubwa wa adhabu, kwamba adhabu hizi zinazotolewa ni ndogo kwa makosa haya ya rushwa ya ngono kwenye michezo na hasa kwenye ngono hapa ndipo pametumika kama mfano mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zetu zina kanuni zake za adhabu, nami nawapongeza sana Wajumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria kwamba, hata pale ambapo sisi upande wa Serikali tulikuwa tumeshusha kidogo, wao wamezipandisha zile adhabu. Kwa hiyo, sisi upande wa Serikali hatuna kipingamizi na *position* hiyo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni hili, *clause 10* ambayo ilikuwa inafanya *amendment* kwenye *section 25* ya sheria. *Clause* hii ilikuwa inapendekeza kwamba kati ya mtu mwenye madaraka na yule ambaye hana Madaraka, na mfano mzuri ni mfano wa mwalimu na mwanafunzi na hasa kwenye vyuo vikuu ambako ndiko hata *study* imefanyika; *study* ilipofanyika ikatuletea mapendekezo kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kama yalivyosemwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba pia kumekuwa kuna makubaliano ya kikanda na kimataifa ambayo yamesababisha ku-*coin* sasa kutengeneza ili sheria hii iweze kumbana kiongozi au mtu mwenye madaraka anayeshawishi kupata rushwa ili atoe huduma au aache kutoa huduma. Pia kumbana yule mnufaika atakayefanya mbinu za kumshawishi mwenye mamlaka kuweza kupata fedha ile anayoitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi upande wa Serikali hatukufika tu hapo, ilitokana na *study*, *literature* mbalimbali na dunia inavyokwenda. Hapa ilionekana ni unyanyasaji kwa wakina mama

lakini siyo kweli. Hawa wenye madaraka wako wanawake wenye madaraka ambao nao pia wanawashawishi vijana wa kiume wawape rushwa ya ngono ili waweze kuwasaidia kuwapa huduma. Kwa hiyo, *study* inaonesha hivyo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwenye *study* inaonesha kwamba imetokea mahali pengine, wanafunzi kikundi, mwalimu huyu hatoi *marks*. Wewe fulani ni mrembo mzuri kabisa, tufanye mbinu tuungane tushirikiane tunakutoa wewe sadaka tukimpata huyu, *marks* zake tumepata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi huo upo na hata kwenye kesi *proceedings* za mambo haya mawakili wetu mahali pengine katika kufanya ile *proceeding* Mahakamani, wamekutana na kizingiti kwamba loh, sasa ushahidi unahamia kwamba huyu mtu anayeonekana dhaifu amemshawishi mtu mwenye *powers* kwa ushahidi ingawa yule mwenye *powers* hata kama amekataa.

Mheshimiwa Naibu Spika, itafika hatua ushahidi wa namna hiyo utahitaji kufanyika. Kwa mfano, ikitokea kwamba huyo mwenye madaraka ameikataa hiyo na ushahidi wa kutongozwa anao ili ampe fedha, tukifika hapo uamuzi wa Mahakama utakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa michango hii ina nguvu. Waheshimiwa Wabunge ni wengi wamesema, wakati huo ukifika sheria zitaendelea kutungwa kwa sababu Bunge lipo hapa kwa ajili ya kutunga sheria, inawezekana leo tusione uzito wa aina hiyo ya kifungo ambacho kilitakiwa ku-*balance* huku na huku, lakini sisi kama Serikali tumekubaliana na Kamati na nawapongeza sana Wajumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge waliochangia. Sisi tunakubaliana kuchukua marekebisho *schedule* iliyotolewa na Kamati na kwa hiyo tume-*drop* kifungu kizima, ile *clause ten* yote na tumechukua marekebisho yaliyojikita

kwenye adhabu kama yalivyokuwa yameandikwa na Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kwa Muswada huu wa marekebisho ya sheria ya *PCCB*, hatuna tatizo, tumekubaliana yote. Kuna *schedule* mbili; iko *Schedule* ya Kamati na iko *Schedule* ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Mtoa hoja wa pili.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Bill 2024)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama kwa uongozi wake mzuri wakati wa Kamati na ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri ambayo tuliifanya wakati tunajadili Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema vizuri Mheshimiwa Olelekaita ambaye ni Mjumbe wa Kamati kwamba, sheria nzuri ni ile ambayo inashirikisha wadau ipasavyo. Kwa kufanya hivyo, ukishirikisha wadau utakuja kuwa na sheria nzuri ambayo inaakisi hali halisi huko sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunawapongeza sana kwani walishirikisha wadau wengi na hata tulipokaa nao katika vikao vile vya Kamati utajiri wa mawazo ulikuwa ni mwingi na matokeo yake ni kwamba leo tumekuja mbele ya Bunge lako Tukufu tukiwa wamoja kwa maana ya kwamba yale mambo yote ya msingi yanayohusu mabadiliko ya sheria ile inayosimamia maendeleo ya uvuvi wa Bahari Kuu kwa maana ya Sura ya 388, Sheria ya Madini Sura ya 123 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi, Sura ya 280, tuliweza kujadiliana vizuri na kukubaliana karibu mambo yote ya msingi. Kwa hiyo basi, tutashuhudia katika Bunge lako Tukufu leo hii, tumekuwa na hoja chache katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza, mchangiaji Mheshimiwa Yahaya Massare ambaye alirudia yale mambo ambayo tulikubaliana wakati wa Kamati, juu ya umuhimu wa mabadiliko tuliyoyafanya kupitia ibara ya tisa ambayo ilikuwa inalenga kuboresha kifungu cha nne na kifungu cha 123 ambapo kwa sasa tumeuondoa ule mwingiliano hasa katika mitaji kwa wale wachimbaji wadogo wa madini, wachimbaji wa kati pamoja na wachimbaji wakubwa. Kwa hiyo, sasa mwingiliano huo hautokuwepo tena na hivyo kutekeleza azma na madhumuni ya Sheria yetu ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, mchangiaji Mheshimiwa Nicodemas Maganga, yeye pia alirudia yale ambayo tulizungumza kwenye Kamati na kukubaliana hasa kuhusiana na wale wachimbaji au wafanyaji biashara wa madini ambao wanatoa taarifa zisizokuwa sahihi, taarifa za uongo, za upotoshaji au kutowasilisha kabisa taarifa zile, na kwamba kwa kufanya hivyo wanaikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumefanya mabadiliko ambayo kifungu kile cha 27(f) kimehakikisha sasa tunaweka adhabu kali kwa watu ambao wanafanya tabia hiyo ambayo inatuletea madhara. Kwa hiyo, kwenye kifungu hiki cha 27(f) sasa tumeweka

adhabu kwa wamiliki wa haki za madini ambao watatoa hizo taarifa za uongo za upotoshaji au kutowasilisha taarifa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, kutokana na muktadha na *spirit* hiyo tuliyokuwanayo ya maridhiano wakati wa Kamati, matokeo yake ni kwamba ni jumla ya Waheshimiwa Wabunge wawili tu wamechangia Muswada huu kwa njia ya kuzungumza na hakuna Mheshimiwa Mbunge aliyechangia kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa kama nilivyosema ni kwamba tulijadiliana sana wakati wa Kamati na yale yote tuliyoyaona ni ya msingi, tuliyachukua na kukubaliana. Ninafikiri kwa kufanya hivyo ndiyo msingi ulio bora wa utungaji na uandishi wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwamba sheria zetu zikiandikwa kwa umakini na hasa kwa kushirikisha wadau wote muhimu hasa Kamati za Bunge, tutaweza kuwa na sheria zilizo nzuri zinazoakisi soko, na kwa kufanya hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kazi yangu imekuwa ndogo sana. Sina la kuongeza zaidi ya kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hujatoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

*Hapa, Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption (Amendments) Bill, 2024)***

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 9

**MWENYEKITI:** Ibara ya Tisa Mheshimiwa Waziri, hii *instrumentalities* imeingiaje hapo? Kwenye Ibara ya Tisa kinachorekebisha Ibara ya 20(4)(a)(i) hapa chini; "*proceeds instrumentalities or pecuniary penalty,*" hiyo "*instrumentalities*" imeingiaje hapa? Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinalenga kutoa adhabu. Moja kati ya adhabu hizo ni pamoja na kutaifisha vitu vyote vinavyoweza kuwa vimetumika katika kufanya *transaction* hiyo ya *corruption*. Kwa "*instrumentalities*" ni neno linalo-*connote* vitu vyovyote vile vitakavyoweza kuwa vimetumika kutengeneza hiyo *transaction,* kama nime...

**MWENYEKITI:** Nilijaribu kutazama, maana wote tunajifunza hapa. Hii "*instrumentalities*" mimi sijui wao walikusudia maana gani, kwa sababu ukisema "*pecuniary penalty*" itajulikana. Ukisema "*proceeds*" zitajulikana lakini hii "*instrumentalities*" kwenye *legal terms* inasema, "*something used to accomplish an action*" ama "*a method used to accomplish an action*" ama "*to achieve an end.*"

Sasa hapa ukisoma vyote vilivyoandikwa hapa, hii ni kama vile, kwa sababu ni lazima viendane vyote ulivyoviweka, yaani unavyovi-*enumerate,* lazima viwe vina maana zile zinazofanana. Ama na yenyewe ina maana tofauti na hii ya kawaida ambayo imeandikwa kwamba inamaanisha hivi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira hapa, pamoja na kutafuta neno hili, ilikuwa ni kuchukua vile ambavyo vilikuwa haviwezi kushikika kwa sheria ilivyokuwa. Kwa mfano, katika *transaction* ya uhalifu wa rushwa kunaweza kukawa kumetumika gari au kusafirisha kitu fulani kikafika kwa mtu fulani. Yaani hakijafika kwenye faida, hakijafika kwenye *proceed,* ni kimetumikatumika, tukasema labda likiwepo hilo neno lita-*capture* hivi vitu vilivyotumika kama tulivyo na ile Sheria ya Uhamiaji ambapo ukiwakamata wale, kila kitu walichokuwa nacho, hata ikiwa ni simu au ni nini, vyote hivyo vinaweza vikawa ni *instrumentalities* zilizosababisha kutekelezwa kwa hiyo *transaction* ya uhalifu wa rushwa.

**MWENYEKITI:** Sasa hili neno "*instrumentalities*" haimaanishi *instruments*? Halipo kabisa kwenye *instrument,* linamanisha *either method,* yaani nawaza, ile unai-*confiscate* vipi? Ndiyo shida yangu. Sina shida na kuliacha hapa lakini kwamba limefuata nini? Ukiangalia huu mlolongo wa haya maneno matatu yaliyoongozana, lenyewe yaani limefuata nini? Kwa sababu haya mengine yanajulikana. Ukisema "*proceed*" zinajulikana, ukisema "*pecuniary penalty*", inajulikana maana yake kuna mambo ya pesa hapa. Sasa hii *instrumentalities* ni *method* ama *something*? Sasa ndiyo sijajua.

Basi *instrumentalities* limetumika tofauti, tutakapopitisha hapa mkalitafute hili neno kwa sababu hapa lilipoingia halimaanishi *instrument,* ni kitu ambacho *not tangible,* kwa sababu inasema *a method used to accomplish an action or a method used to achieve an end*. Sasa ile *method* utai... *I don't know*. Sijui kama nimeeleweka! Eti Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nimeeleweka,

japokuwa hii itakuwa imetoka kule kwa watu wa *PCCB?* Sawa mtaleta marekebisho.

Haya, naona Mjumbe wa Kamati huenda walielezwa maana huko. Mheshimiwa Abdullah Mwinyi.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nisome *definition* ya *instrumentality of crime. Instrumentality of a crime means any property other than real property and any building fixtures and improves thereon whose use contributes directly and materially to the commission of a crime or to the commission of any criminal transaction of which a crime is a party, instrumentality of crime.*

**MWENYEKITI:** Sawa, ahsante sana. Sasa hiyo tukiiweka peke yake bila neno *crime* italeta maana moja au tuongezee hapa neno *crime* au italeta maana moja?

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

**MWENYEKITI:** Haitalea maana hiyo?

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *in my opinion* lazima iwe *instrumentality of crime* ndiyo ina-*define* hivi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuiache hivi ilivyo au tuongeze neno *crime?* Maana yule kasoma pamoja na hili neno. Italeta maana hiyo hiyo tukiiacha *instrumentalities* peke yake bila *crime?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, naona kama tutakuwa tunafanya *repetition* kwa sababu sheria yenyewe ni sheria inayo-*deal* na jinai. Kwa hiyo, *whether* tukiweka au hatujaweka, lakini kusema ukweli ina-*capture* kile

ambacho kimetakiwa, kwamba ni vifaa vilivyotumika nje ya vile ambavyo ni *intangible,* sioni kama inaweza ikawa inatofautiana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaiacha namna ilivyo ama italeta changamoto ikiongezewa hilo neno *instrumentalities of crime*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 10

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dogo tu hapa Kifungu cha Tisa pale, 4(a)(i) mstari ule wa *last but one,* ya *Roman* inasema hivi, *"value of any advantage received by him or any part of it proceeds..." It must be "its proceeds." The amount of money or...*

**MWENYEKITI:** Haya *part of its proceed,* si ndiyo. Mmepaona? Hata hii (b) pia nilisahau kidogo, *"is an agent 'or.' Not "order that amount or value of any advantage received."* Kuna kama neno "*the*" linakosekana *somewhere.* Mtakavyopata muda, kwa sababu hilo ni jambo dogo, *AG* anaruhusiwa kuliweka hapo. Mtatazama kuna mahali neno "*the*" linakosekana. Kwa hiyo, kidogo *something like that, that the amount, unless* kama mimi nimesoma haraka lakini kuna neno "*the*" linakosekana.

Hii "*its*", sasa hii kuongezea "*s*" kwenye "*it*", kwa sababu imetoka kwa Mjumbe pale inakwenda kwa *AG* ndiye atafanya marekebisho. Hii "*the*" pia kwa sababu nilikuwa nimeshahoji, itakuja kwako. Kwa hiyo, Bunge litakuwa limetunga kifungu kama walivyohojiwa kabla mimi na Mheshimiwa Kimei hatujaleta haya ya kuongeza "*s*" na kusema "*the*". Si ndiyo eh! Mheshimiwa Simbachawene anacheka. Ndiyo utaratibu, kwa sababu Bunge lilishahojiwa kwenye kifungu hiki.

**MWENYEKITI:** Kifungu cha kumi marekebisho ya Kamati na ni ana-*move* Mwenyekiti wa Kamati. Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 10 ya Muswada mapendekezo ya Serikali yalikusudia kufuta Kifungu cha 25 cha Sheria ya sasa ya Kupambana na Rushwa kwa kuongeza sehemu ya (i) sehemu (a), (b); na sehemu (b) ilikuwa inakusudia kumwadhibu yule ambaye anamshawishi mtu mwenye mamlaka kutenda tendo la rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati baada ya kupitia na kujadiliana sana na Serikali na kupata maoni ya wadau, Kamati imeleta *schedule* ya *amendment* ya kutaka Kifungu Na. 25 kifanyiwe marekebisho kwa kuongeza adhabu pekee kwa maana ya kuweka ukomo wa chini na wa juu wa adhabu ya fedha na ya kifungo kama ambavyo imewasilishwa huko na siyo yale mapendekezo ya awali ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kuna jambo hapo kwenye marekebisho yanayopendekezwa na Kamati.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunaishukuru sana Kamati, tumeshirikiana nao katika kujadiliana na hili. Ingawa lilikuja pia nyakati za mwisho, lakini sisi upande wa Serikali tumekubaliana. Nimezungumzia hili wakati nina*wind-up,* kwa hiyo, sisi hatuna maneno, tunachukua na tuna-*adopt* hii ya upande wa Kamati. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 25 cha muswada kifungu cha 25(1)(a) na (b); sasa sijui kwa nini moja, halafu kikawekwa (a) na (b) kwa sababu katika utaratibu wa utungaji wa

sheria kilipaswa kiwe 25(1)(a) haiwezi kuwa (1) wakati (2) hakuna. Huwezi kuwa na moja tu halafu ikawa na (a) na (b), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, si ndivyo hivyo? Unaweza ukawa na *subsection* (1)(a) na (b) wakati hakuna *subsection* (2), kwenye *legal draft?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Ngoja. Hii hapa ni *minor,* Mheshimiwa Waziri kaa tu kwa sasa, kwa sababu hii (b) kwa maelezo waliyoyatoa Kamati ni kana kwamba Serikali inaendelea na kifungu kilichopo kwenye sheria na kwa hiyo 25 hii inakuwa haipo. Nimeelewa vizuri. Kama hivyo ndivyo, nani aliyeleta mabadiliko hayo? Aliyeleta hiyo *schedule* ya kukiondoa kifungu cha 25 kilichopo kwenye Muswada na sasa kuleta mapendekezo haya ya kubadilisha kile kilichopo ni nani? Kwa sababu napitia hapa marekebisho mliyoyaleta Serikali, hiyo ya kuondoa kifungu cha 25 kibaki kile kingine haimo na wala Kamati pia haijaleta kwamba kibaki kile kilichopo. Hilo ndiyo wanapendekeza mabadiliko.

Wao wamependekeza mabadiliko moja kwa moja kwenda kule. Aah, *no, no,* samahani. Kamati wamesema wanataka kiwe *deleted.* Samahani, samahani. Kwa hiyo, Kamati wako sahihi, wamefuta hiki ili kibaki kile cha kwenye sheria. Sawa. Kwa hiyo, sasa Kamati wameleta mabadiliko mapya kabisa ambavyo Mheshimiwa Waziri ndiyo uliyokuwa umesimama ili utoe maelezo. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati walichokifanya wamefuta kabisa ile *clause* ya kwenye *bill,* halafu wakaenda *straight* waka-*cite* ya kwenye sheria. Kwa hiyo, wamepiga *shortcut,* lakini maudhui ni yale yale, kwamba inabakia 25 ile ya kwenye sheria ila isi-*deal* na chochote, yachomekwe tu yale maneno ya adhabu.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa upande wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati tukitunga ile sheria, Ijumaa ama Alhamisi, kuhusu hizi *fines* na zile *custodial sentences,* kwa sababu hapa hawa hawa Kamati wanasema, yaani sasa hivi ile adhabu iliyopo kwenye sheria mama tuite, iwe *fine of not less than two million shillings but not exceeding 10 million shillings or to imprisonment for a term not less than five years.* Maana yake ni kwamba hii *two million* na *five years halafu 10 years* inakaa, na *to imprisonment for a term of not less than five years but not exceeding 10 years.* Kwa hiyo, *10 million* inakaa na *10 years.*

Ukihesabu hizi adhabu maana yake huyu mwingine anapata, yaani adhabu haiendani. Ukihesabu ya kutokea hapa kwenye *two million* mpaka *10 million,* kutoka kwenye *five years* mpaka *10 years* havioani. Sijui nimeeleweka? Ama nirejee tena? Ni kwamba, ukichukua *two million* ndiyo unailinganisha na *five years,* si ndiyo? Kwa sababu umesema *not less than,* halafu ukichukua *10 million* unailinganisha na *10 years,* hizi adhabu zinafanana? Kwa nini huyu mwenye *two million* kapewa *five* na kwa nini huyu mwenye 10 kapewa pia *10 years* badala ya *25 years?* Sijui kama nimeeleweka!

Hii sawa imetoka kwenye Kamati, lakini hata nyie Muswada wenu wa wiki iliyopita niliona hiki kitu. Yaani zile adhabu zinapendekezwa ni kama vile tukikutana kwenye Kamati tunaona kwamba kosa hili kwa kweli hapa tungeweka tu *five,* yaani ni kama vile hatuna *guidance* ambayo sitaki kuamini kama hatuna; na kama hatuna, tuitengeneze ili mwelekeo wa hizi sheria ambazo zina *criminal, I don't know,* zina *criminality* ama zina *criminal something to it*. Lazima zile adhabu ukisema miaka miwili ifanane na ile adhabu ya faini. Huwezi kuwa una faini inayotofautiana. Sasa *two million* atakuwa ameadhibiwa pakubwa sana kwa *five years.* Huyu wa *10 million* atakuwa amepewa *10 years,* yaani *10 to 10; 2 to 5* si ndiyo hata ile kawaida tu.

Mheshimiwa Waziri, haya naona, hili ni la jumla tunaweza tusilibadilishe hapa, lakini nililisema juzi nalirejea tena leo kwa sababu lazima zile hesabu ziwe zinaenda kwa kuoana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mara ya kwanza nitamke kitu ambacho siyo cha kawaida, kwamba mimi ninaunga mkono hoja ya Kamati. Kwa nini naunga mkono hoja ya Kamati? Kwanza uwiano wa adhabu ya *fine* na kifungo cha jela ni vitu viwili tofauti, haviwezi vikawa vinahusianishwa kwa namba kama huku ni *five million,* basi na huku iwe *five years.* Yaani miaka ya kifungo haiwezi kuwianishwa na fedha.

**MWENYEKITI:** Mimi nataka tu *justification,* kwa nini huyu mwenye *10 years* umeweka *10 million*? Huyu mwenye *two million,* ukaweka *five years*? Hizo *minimum* zako yaani hizo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitokea tu Wajumbe walifikiri.

**MWENYEKITI:** Sasa huko kutokea ndiyo lazima kuwe na *guidance* Mheshimiwa. Ukisema tu watu wamekaa mahali wakafikiria kwamba hii naona tufanye 10, hii tufanye *five*, lazima tuwe na *guidance* ambayo inatu-*guide*. Kwa sababu la sivyo mimi nikiingia kwenye Kamati pengine nafikiria *25 years* ama *30 years* wataweka. Mwingine anafikiria *two years* ama *three months* inawekwa. Sasa lazima tuwe na namna ya kupiga hesabu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mwenyekiti kwamba ni lazima tuwe na utaratibu kwa sababu sheria tunazozitunga ni nyingi, sasa tukiwa na sheria zinatungwa...

**MWENYEKITI:** Kila mtu, huyu miezi miwili, huyu mitatu. Sasa hiyo haipendezi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwishoni pale kuna neno limetumika *or both*.

**MWENYEKITI:** Sasa hilo *it is even more serious.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, "*or both,*" kwa hiyo, sijui itasemaje, lakini kimsingi tulikubaliana kwa sababu tuliona kwa kweli hata hapa mjadala ulikuwa mkubwa, Waheshimiwa Wabunge wanalalamika kwamba adhabu ni ndogo.

**MWENYEKITI:** Kwanza kwenye Kamati, "*both*" itakuwa haipo. Hebu ile *main act*. Fungua hiyo *25*, kwa sababu wameifuta ile mliyokuwa mmeileta kwenye *bill,* wamerudi kwenye ile *main*. Sasa ngoja tuone haya maneno yanapoingizwa kama maneno *both* yanabaki ama hayapo. *(Deleting the word to a fine not exceeding three years appearing)*, yanabaki kwa sababu hawa wamefuta yale maneno ambayo yanahusu miezi na faini, kwa hiyo, haya ya hapa mbele hawajayafuta, wameishia kwenye *three years.* Kwa hiyo, "*or both*" inabaki.

Haya ahsante sana, nadhani hili limeeleweka, kama hatuna *guidance* tutengeneze. Kama *guidance* ni lazima ije kwa sheria, nadhani tulikuwa na hiyo sheria. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, eti, nadhani tunayo sheria hiyo ya *Sentencing.* Sina hakika ina-*cover* na mambo kama haya, lakini ni muhimu kwa kweli ili ijulikane, yaani adhabu ikishafikirika kwamba huyu anatakiwa apewe *ten years,* ijue *fine* yake itakuwa inapigwa kwa sura gani? Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, Kifungu cha 10 kimefutwa na Kamati lakini. Ngoja kwanza, lakini wameleta kama kifungu kipya cha *bill* ambacho kinarekebisha ile *section 25* ya kwenye *main Act*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 11

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wazo, pale 11(b) wanasema "*possesses or owns property,* ina-*assume* kwamba fedha ya rushwa inapelekwa kwenye *property* lakini fedha ya rushwa inaweza ikaenda kwenye magari, ikawekwa kwenye *bank account* au ikawekwa kwenye *assets* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza badala ya kuandika *property,* waandike *assets* hiyo itakuwa ni *neutral,* yaani ina-*cover everything,* siyo tu iwe *property* ya nyumba au wengine wanaenda kunywa tu inakuwa ni rushwa.

**MWENYEKITI:** Kwa vile tumezoea kwenye *property* ni nyumba, lakini *property* kwa maana ya lugha ya kisheria inamaanisha umiliki. Sasa labda sina hakika sana kama *possesses or owns property disproportionate owns assets*, sijaangalia maana ya haya maneno mawili, lakini *property* kwenye sheria inamaanisha hivyo vyote, yaani hata *bank* imo humo ndani, ni sehemu ya *property*.

Hata hivyo ni jambo ambalo linafanya msamiati unaendelea kukua. Basi mnatakiwa kufanyia utafiti haya maneno mawili ya *assets* na *property,* ipi itakuwa *more appropriate* kwa kuangalia muda ambao tunaitunga hii sheria. Si ndiyo jamani. Haya, Bunge lilikuwa limeshahojiwa. Tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajawa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Linarejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi. Mtoa hoja, taarifa.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2023, napenda kuliarifu Bunge lako kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption Amendment, Bill 2024)* ibara kwa ibara na imekubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption Amendment, Bill 2024)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, na sasa nitawahoji.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki, ahsanteni sana.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa ajili ya Kuondoa Mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa Utekelezaji wa baadhi ya Masharti ya Sheria hiyo *(The Bill for an Act to Amend the Prevention and Combating of Corruption Act with the View of Making Better Provision for its Effective Implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Muswada wa Sheria kusomwa mara ya tatu, nitumie fursa hii kutangaza kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption Amendment Bill 2024)* umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunawashukuru sana Kamati yetu kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya, lakini pia tunawashukuru upande wa Serikali kwa ushirikiano ambao mmeuonesha kwa kufanya kazi kwa ukaribu na Kamati na kwa kusikiliza maoni ya Kamati, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ZAINABU ISSA - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna marekebisho kwenye *Table of Contents*. Tunatunga sheria ya Kiingereza, nimesikia watu wakisema Mheshimiwa Kiswahili vipi leo? Haya tuendelee, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajawa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

**MWENYEKITI:** Wanabadilisha kichwa cha sehemu au ni kichwa cha habari? Ni kichwa cha sehemu, si ndiyo? Sasa mbona Waziri, ananicheka! Wanabadilisha kichwa cha sehemu, jamani. Ni kichwa cha sehemu au kichwa cha habari? Haya sawa badala ya kuwa sehemu ya pili inaitwa *"The Deep-Sea Fisheries Management and Development Act",* itakuwa inaitwa *"Amendment of the Deep-Sea and the rest." (Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajawa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 6

**MWENYEKITI:** Kifungu cha Sita, kwanza ile sheria yangu nani kaitoa hapa? Nani amenihujumu? Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kifungu cha Nne na cha Tano tumeshahoji. Kifungu cha 4(4) *"The Tenure of Office for members referred two in sub section 2 shall be three years but shall be eligible."* Hii hapa *"shall be eligible,"* sidhani kama ni sawa, maana yake inakulazimisha na usipomteua huyo mtu maana yake mtakutana kwa *Court.*

Ni kwa sababu *appointment* hawaja-*point* wao, ni mtu mwingine. Anaweza kuwa amefikiri kubadilisha, lakini wale walioko anayetaka aendelee nao anaweza, na siyo kwamba analazimika kuendelea nao. Kifungu hapa badala ya kutumia neno *"but may be eligible",* kinasema *"shall,"* maana yake lazima uwateue *as long as they alive*. Ama siku hizi neno *"shall"* linamaanisha nini? Nilikuwa nimeweka hapa, naona hawa baada ya kuhamisha kidogo…

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri jinsi ilivyo hapa ilikuwa ni kuweka msingi kwamba hao Wajumbe baada ya ku-*serve* ile miaka mitatu ya mwanzo wanaweza kuendelea miaka ile…

**MWENYEKITI**: "Wanaweza." Kwa hiyo, siyo neno *"shall",* inabidi iwe "*may*."

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado haimuondolei uwaziri hata kama tukiweka *"shall."*

**MWENYEKITI:** Hapana, inamwondolea kwa sababu, si maana yake Bunge limekuagiza? Sasa wewe utatokaje wakati umeagizwa na Bunge hapa, sheria imeshatungwa? Kwa sababu umesema *"but shall be eligible,"* ama!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado utaangalia vile vigezo vingine kama bado ana sifa ya kuendelea ama la.

**MWENYEKITI:** Jamani kwani sheria nyingine huwa tunaweka neno *"shall,"* kweli kwenye *eligibility?* Hebu nitafutieni moja. Nyie wanasheria wawili mnatingisha vichwa hapo, nitafutieni moja ambayo tumelazimisha yule anayeteua lazima *"shall,"* kwa sababu unavyosema *"may be"* maana yake ni kwamba anaweza, kama ulivyosema; lakini ukisema hivi, maana yake ateuliwe au; au mimi nimesoma vibaya? Wewe wa nyuma tafuta sheria, huyu anataka kutoa maelezo, sijui kama ni sheria ananisomea. Mheshimiwa, nisomee mojawapo tuliyosema *"shall."*

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *"shall"* inaenda ku-*qualify eligibility* ambapo *eligibility* sasa ni *optional,* haisemi *"shall be appointment,"* inasema, *"shall be eligible*,*"* kwa hiyo, imekaa vizuri.

**MWENYEKITI:** Hapana. Hujanishawishi. Nitafutie sheria ambayo tumesema hivyo, kwa sababu sisi pia si tumeshatunga sheria hapa ili tusitoke pia kwenye mstari? Kwa sababu tukisema *"shall*,*"* kwani ungesema *"may"* ungemaanisha nini? Ungemaanisha kwamba ametupwa nje? Ungesema *"may be eligible*,*"* ile tunayosema *re-election* sijui nini nini, huwa tunasemaje? Tafuta hata kwenye Katiba basi; kwa Rais tunasemaje *"shall be…"*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo.

**MWENYEKITI:** Hebu endelea, tunatumia neno *"shall"?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI***:* Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria zote kama unataka, kwa sababu *root* ni *eligibility…*

**MWENYEKITI:** Umeshapata? Mheshimiwa Jerry uko na mtandao hapa, na nimekuona umeinama muda mrefu huwezi kusema hujapata. Tafuta sheria ya Bodi yoyote hapo tupate mfano. Mwanasheria Mkuu, endelea.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zote zinatumia "*shall,*" kwa sababu ni *eligibility*.

**MWENYEKITI:** Lazima nitajiwe mfano. Si unajua kuna matomaso? Kwa hiyo, na wewe nitafutie mfano, tuendelee kwa sababu kifungu hiki nilikuwa nimeshahoji hata hivyo, lakini nilitaka kupata hiyo *attention* ya *AG* kwenye matumizi ya haya maneno, Kifungu cha Sita kilikuwa kimeshasomwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajawa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 10

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mmeshahojiwa Kifungu cha 10, lakini Serikali ilileta marekebisho hapa, naona Katibu alipitiwa kuyaweka, kwa hiyo, inabidi tukirejee.

Kifungu cha 10 Serikali inafanya mabadiliko ya haya maneno yaliyotumika hapa na kwa namna taarifa ilivyokuwa imesomwa,

nadhani yalikuwa ni maoni ya Kamati ama kitu kama hicho. Kwa hiyo, Kamati yetu ya Bunge ilipendekeza mabadiliko katika Kifungu hiki cha 10 ambapo Serikali iliafiki. Kwa hiyo, inabidi tukirejee Kifungu cha 10.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajawa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22

*(Vifungu vilivyotajawa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne Jina la Muswada lina marekebisho kama lilivyo *appear* kwenye *Table of Content*.

**MWENYEKITI:** Sawa. Kwa hiyo, haya mabadiliko kwa sababu tulishayataja kule kwenye *Table of Contents* yanaingia hapa pia. Tuendelee.

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25

*(Vifungu vilivyotajawa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Soma kwenye kisemeo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *act* nimeipata.

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, dhana zaidi ni kwenye ile *eligibility* na uteuzi. Kwa hiyo, sheria zote huwa ziko hivyo. Sasa nikusomee *Planting Health Act* ya mwaka 2020 kifungu cha nne; *"Tenure of the office of members of board, every member of the board shall hold office for a term of not exceeding three years and shall be eligible for reappointment for one further term."* Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI**: *One, what?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** *"One further term."*

**MWENYEKITI:** Shukrani. Hiyo inatuisaidia. Sasa ulivyosoma hapa na ukisoma hiki kingine tunarudi pale nilipokuwa nasema. Vifungu hivi vyote vinahusu jambo hili moja. Ukikisoma hiki kinazungumza lugha tofauti ukienda kile kingine kinazungumza lugha tofauti. Kwa hiyo, kuna haja ya ku-*synchronize* ili ile lugha yetu ya kisheria iwe inaenda kwa sura hiyo. Huku wanasema *"re-appointment for*

*another term",* kule kwingine *"for a further term*." Kwa hiyo, ahsante sana, hilo linatusaidia.

Waheshimiwa Wabunge, kuna karatasi yangu nyingine hapa naona imepotelea sijui wapi? Nikiipata pia nitakujulisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ahsante sana. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi, ahsante sana, mtoa hoja, taarifa.

**T A AR I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments Bill 2024)* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Law (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)* kama ulivyorekebishwa kwenye Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, na sasa nitawahoji, wanaoafiki hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali ya Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments) Bill, 2024.*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki, ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Zipatazo Tatu kwa lengo la Kuondoa Mapungufu ambayo Yamebainika Wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti katika Sheria Hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in Order to Keep the Laws Updated with Some Challenges Observed in its Implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusoma mara ya tatu huu Muswada maana yake Bunge tumemaliza kazi yetu. Kwa maana hiyo nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments) Bill 2024)* umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama Katiba inavyotutaka Miswada hii miwili ambayo tumeipitisha hapa tutampelekea Mheshimiwa Rais ili naye aifanyie kazi kwa sehemu yake kisha utekelezaji utaanza baada ya yeye kuweka saini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Naibu Waziri, lakini pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta Miswada hii ambayo imefanyiwa kazi na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Tunawashukuru sana kwa kazi nzuri, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya na upande wa Serikali tunawashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmeuonesha kwenye hizi Kamati mmefanya kazi kwa kushirikiana na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote, kila mmoja alivyoshiriki, hii ni kazi yetu ya msingi sana. Tunawashukuru sana kwa kila mmoja wenu namna alivyoshiriki mpaka tumefika mwisho wa maboresho kwenye Miswada hii. Upande wa Serikali tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa haya yote, na Waheshimiwa Wabunge, pia kila la heri kwa Miswada inayoendelea hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninalo tangazo moja, tangazo linatoka kwa Mwenyekiti wa *Caucus* ya Chama Cha Mapinduzi, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi kwamba mkitoka hapa mrejee *White House*. Mkitoka tu hapa mwelekee *White House* kuna kikao cha muhimu sana.

Baada ya tangazo hilo, nawatakia jioni njema. Ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.23 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 3 Septemba, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*